

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Nne - Tarehe 14 Juni, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2002 (*The Annual Report and Accounts of the Small Industries Development Organization (SIDO) for the Year Ended 30th June, 2002*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania kwa Mwaka 2001/2002 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Bureau of Standards (TBS) for the Year 2001/2002*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

Madaktari Bingwa - Hospitali ya Mkoa na Wilaya Shinyanga

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga ni wa tatu Kitaifa kuwa na idadi kubwa ya watu kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 na kwa kuwa magonjwa mengi kama vile saratani ya chembe nyeupe za damu (*leukemia*), *asthma* na kadhalika yameanza kujitokeza katika jamii:-

- (a) Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa wa kutosha katika Mkoa wa Shinyanga?

(b) Je, kila Hospitali ya Wilaya inatakiwa kuwa na Madaktari Bingwa wangapi?

(c) Je, Hospitali ya Wilaya ya Meatu ina upungufu wa madaktari wangapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Afya, Mkoa unatakiwa kuwa na Madaktari Bingwa wapatao 6 wa fani mbalimbali za upasuaji, macho, magonjwa ya akili, magonjwa ya akina mama, watoto na *physician*. Aidha, wote hawa wanatakiwa kuwa katika Hospitali ya Mkoa kwa kuwa ndiyo kituo cha mwisho cha rufaa mkoani. Kwa sasa Mkoa wa Shinyanga una Madaktari Bingwa wa upasuaji wawili. Ili kukabiliana na upungufu uliopo, Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga, imeomba madaktari (*Medical Doctors*) katika makadirio yake ya mwaka 2004/2005 lakini kwa bahati mbaya hawakuweza kupatikana hivyo maombi hayo yamerudiwa tena katika mwaka huu wa fedha. Ofisi yangu itaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Afya na Serikali ya Mkoa wa Shinyanga ili kuhakikisha kibali hicho kinapatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Afya, Hospitali ya Wilaya haina ikama ya Madaktari Bingwa. Wanaotakiwa ni madaktari wa kawaida (*Medical Officers*) wawili, Madaktari Wasaidizi (*Assistant Medical Officers*) 10 na Matabibu (*Clinical Officers*) 13.

(c) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Meatu ina upungufu wa madaktari walioainishwa katika sehemu (b) ya swali hili 19. Idadi ya madaktari wanaotakiwa ni 25 kwa hiyo, waliopo ni 6. Hata hivyo, naomba tu kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, suala hili kwa Wilaya ya Meatu linaendelea kufuutiliwa na ofisi yangu kwa kushirikiana na sekta zinazohusika.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniruhusu ili niweze kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali inafahamu matatizo ya wananchi kuhusu suala la afya, lakini inakuwa kimya kwa muda mrefu kitu ambacho kinasababisha wananchi wasielewe jitihada za Serikali kuhusu suala la afya. Hii inapelekea kwa mfano Wilaya ya Meatu kuwa na waganga wachache kiasi kwamba wanashindwa kuhudumia ipasavyo. Je, Serikali haioni kwamba inafanya makosa ya wazi kwamba inashindwa kupeleka mapema madaktari hao hadi Waheshimiwa Wabunge, waulize maswali na waombwe na mikakati mbalimbali na ahadi zisizokuwa na utekelezaji? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI

ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali imelifumbua macho jambo hili au kwamba imelinyamazia jambo hili, mimi nina hakika Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, pengine anazungumza tu kutoka kwenye mtazamo wa Wilaya ya Meatu. Lakini kama unataka kulitazama suala hili Kitaifa, juhudhi ambazo Serikali inafanya katika eneo hili ni kubwa na ndiyo maana maeneo mengi yanaendelea kupata madaktari kadri nafasi inavyopatikana. Kwa hiyo, hatusubiri mpaka tuulizwe Bungeni, lakini suala la kuuliza Bungeni ni wajibu wako kwa sababu lazima wananchi wako wapate maelezo na ndiyo maana tunajitahidi kuyatoa.

MHE. MARGARETH J. BWANA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ikizingatiwa swal la msingi lililoulizwa, upungufu huo upo mpaka katika maeneo mbalimbali, Mkoa wa Rukwa ikiwa ni mionganoni mwa mkoa ambao unaongoza kwa kuwa na upungufu mkubwa sana wa madaktari.

Je, Serikali inaandaa mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha kwamba tatizo la upungufu huo wa madaktari karibu nchi nzima, linapata ufumbuzi ikizingatiwa kwamba kuna madaktari wengine ambao pia wanapangwa kwenye maeneo magumu kama hayo ya Mkoa wa Rukwa lakini hawaendi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI

ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, mara nydingi tumekuwa tunatoa maelezo hapa kuonyesha ukubwa wa tatizo la wataalam hawa katika sekta hii ya afya. Lakini vile vile tungependa kusisitiza kwamba, pamoja na kutambua kuwepo kwa tatizo hilo, Serikali nayo inaendelea kufanya maandalizi makubwa tu kwa sababu tatizo la madaktari liko katika sura mbili, moja ni idadi yao wenyewe kwamba hawatoshi, lakini pili hata pale wanapopatikana katika hali ya soko huria tulilonalo sasa, wengi wanakimbilia katika maeneo ambayo ni mazuri zaidi kuliko huko Serikalini. Tatuhii, ni mazingira katika vituo vyetu ambapo wanafanya kazi, vingine havikuzingatia mazingira magumu. Kwa hiyo, kwa mtazamo huu, Serikali inatazama sasa ni jambo gani lifanyike kwa maana ya kujaribu kuona kama tunaweza tukawatazama *as a special case* ili wawze pengine kuvutiwa zaidi katika fani hiyo. (*Makofi*)

Na. 31

Hospitali ya Matema

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Matema iliyojengwa kwenye fukwe za Ziwa Nyasa inaendeshwa na Kanisa la KKKT Dayosisi ya Konde na kwa kuwa hospitali hiyo inatoa huduma nzuri sana na muhimu kwa zaidi ya wakazi 80,000 wa Tarafa ya Ntebelia na wengine zaidi kutoka katika Wilaya jirani za Makete na Ludewa:-

(a) Je, kwa mujibu wa Sera ya Afya, Serikali Kuu inatoa msaada gani kwa hospitali hiyo ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri zaidi na rahisi kwa wagonjwa ambao karibu wote ni maskini sana?

(b) Je, ili hospitali binafsi iweze kupata msaada au ruzuku kutoka Serikali Kuu inatakiwa ifanye nini au iwe na sifa gani na ni hospitali ngapi chini ya madhehebu ya dini zinapata ruzuku kutoka Serikalini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nakubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Hospitali ya Matema, inatoa huduma nzuri sana na muhimu kwa wakazi wapatao 80,000 wa Tarafa ya Ntebelia na wale wanaotoka Wilaya jirani za Makete na Ludewa. (*Makofi*)

Napenda kuupongeza Uongozi wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Konde, kwa kutoa huduma hii na kuiomba iendelee kutoa mchango huo. Aidha, mara zote Serikali imekuwa ikitoa mchango wake kusaidia Hospitali zinazoendeshwa na Mashirika ya Dini ili yaweze kutoa huduma hizo kwa wananchi wengi na kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchango huo wa Serikali kwa Hospitali hii ni kama ifuatavyo: Kwanza, mwaka 2002/2003, Serikali ilitoa ruzuku kwa ajili ya vitanda na wafanyakazi (*bed/staff grant*) kupitia Hospitali ya Kanisa la KKKT - Itete Tukuyu yenye jumla ya Sh. 14,748,520/=. Pili, kwa mwaka huo huo walipata vile vile mgao wa asilimia 15 kutoka mfuko wa pamoja wa Afya (*Health Basket Fund*) uliokuwa na thamani ya Sh. 4,451,250/=. Kwa Mwaka 2003/2004, Hospitali hiyo pia imepata mgao toka Mfuko wa pamoja wa Afya wa Sh. 9,137,000. Aidha, Serikali inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa Hospitali ya Matema kupitia Mfuko wa Afya na kusimamia viwango vya utoaji wa huduma za afya katika hospitali hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ili hospitali binafsi iweze kupata ruzuku kutoka Serikalini, haina budi kuzingatia yafuatayo: Kuandika barua ya maombi kwa Katibu Mkoo Wizara ya Afya, iwe ni hospitali binafsi hasa ya madhehebu ya dini inayotoa huduma za afya bila faida na Hospitali iwe katika maeneo ya vijiji wanapoishi watu wengi watakaonufaika na huduma ya afya ya msingi. Kwa Mkoa wa Mbeya baadhi ya hospitali za ina hiyo ni pamoja na Hospitali ya KKKT - Itete - Tukuyu, Hospitali ya Igogwe - Tukuyu, Hospitali Teule ya Wilaya (*Designated District Hospital*) Isoko - Ilete na Hospitali Teule ya Wilaya Mwambani - Chunya. Hospitali Teule za Wilaya zinapata ruzuku kwa asilimia 100 kwa ajili ya uendeshaji (*Recurrent Cost*) na hospitali hizi nyingine zinapata *Bed Grant* ya 60% kila moja na asilimia 60 kwa ajili ya wafanyakazi (*Staff Grant*).

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Hospitali ya Matema ilikwishawasilisha maombi yake Wizara ya Afya, ili iweze kupatiwa ruzuku moja kwa moja. Maombi hayo yanaendelea kushughulikiwa na Wizara na ni matumaini yangu kwamba, pengine wanaweza kufanikiwa katika maombi yao. (*Makofii*)

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE: Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kyela ni moja ya Wilaya chache zilizoathirika sana na Ugonjwa wa Ukimwi, je, Serikali haioni umuhimu wa kuiteua Hospitali hii ya Matema kuwa moja ya hospitali ambazo zinaweza kupewa madawa ya Ukimwi na kuwatibu wananchi ambao wengi sana wanatumia hospitali hii? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba, Serikali imeshaanda utaratibu wa namna ya kusambaza madawa haya katika mahospitali mbalimbali. Lakini pengine kwa hoja ya Hospitali ya Matema, hili tutajaribu kuliwasilisha Wizara ya Afya, kwa sababu haliko katika hospitali zile ambazo ni *designated* ili tuone kama nalo linaweza kukubalika. (*Makofii*)

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa kodi ni mojawapo ya sababu zinazowazuia madaktari kuanzisha zahanati vijijini, je, isingekuwa ni busara kwa Serikali kuwaondolea kodi hao madaktari ambao wanajitolea kuanzisha zahanati vijijini? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, ameuliza swali hili wakati muafaka, wakati bajeti imeshawasilishwa hapa, pengine ni jambo ambalo mnaweza mkachangia mawazo ili Waziri wa Fedha aone kama hilo linaweza likachukuliwa. (*Makofii*)

Na. 32

Lower Moshi Irrigation Project

MHE. THOMAS NGAWAIYA aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu; na kwa kuwa tunayo ardhi kubwa sana yenye rutuba na sehemu kubwa ya ardhi hiyo inahitaji maji ya umwagiliaji ili iweze kuwa ya manufaa kwa kilimo; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, aliiona haja hiyo huko Moshi Vijijini, katika Kituo cha Kilimo cha Mpunga kijulikanacho kama *Lower Moshi Irrigation* na aliahidi kutatua matatizo yaliyojitekeza kuhusu upatikanaji wa maji ya uhakika kuendeshea kilimo cha umwagiliaji katika mashamba ya mpunga:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais, aliahidi kutoa ufumbuzi wa tatizo la maji na kwamba ufumbuzi huo angeupeleka mwenyewe huko Mabogini, *Lower Moshi Irrigation*, mapema iwezekanavyo; je, kwa nini ahadi hiyo hajatekelezwa hadi leo hii?

(b) Je, ni nani anayepaswa kufuatilia ahadi za Rais, ili aweze kuhojiwa juu ya ahadi hiyo ambayo ni zaidi ya miaka miwili tangu itolewe?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya habari za kuwepo kwa mvutano kati ya Mradi wa Umeme Pangani na Nyumba ya Mungu, unaosababisha mradi huo wa umwagiliaji kutopata maji ya kutosha kwa shughuli za umwagiliaji katika mashamba ya mpunga ambao ni chakula kinachoweza kuondoa baa la njaa kwa Watanzania na kuondokana na aibu ya kukosa chakula?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalí la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Rais alipotembelea Mradi wa *Lower Moshi Irrigation* tarehe 20 Februari, 2002 aliarifiwa na wakulima juu ya upungufu mkubwa wa maji kutoka kwenye vyanzo vinavyopeleka maji kwenye skimu hiyo ya umwagiliaji. Serikali ilibaini kwamba, ili kutatua tatizo hilo, maji ya nyongeza kiasi cha mita tano za ujazo kwa sekunde, yangethajika kutoka kwenye Mto Kikuletwa. Hata hivyo, uchunguzi wa kitaalam ulionyesha kwamba, kama kiwango hicho cha maji kingechukuliwa, uzalishaji wa umeme katika Vituo vya Nyumba ya Mungu na Pangani ungeathirika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, alikwishatoa uamuzi kwamba, maji ya Mto Kikuletwa yagawiwe kwa uwiano kati ya kilimo na uzalishaji wa umeme kwa kuwa kila moja ya mahitaji hayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Kutokana na agizo hilo la Rais, tarehe 26 Februari, 2000, Serikali ilitoa hati ya kumiliki maji ya meta za ujazo 3.71 kwa sekunde kutoka kwenye Mto Kikuletwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika skimu ya *Lower Moshi*. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba, siyo kweli kwamba, ahadi ya Mheshimiwa Rais hajatekelezwa

(b) Ni jukumu la ngazi za Serikali zinazohusika kufuatilia utekelezaji wa maagizo anayotoa Mheshimiwa Rais, anapokuwa kwenye ziara mikoani. Kuhusiana na ahadi ya Rais ya kuupatia Mradi wa *Lower Moshi* maji ya nyongeza kutoka Mto Kikuletwa, utekelezaji umeshakamilika na Serikali inastahili kupongezwa badala ya kuhojiwa. (*Makofit*)

(c) Uchunguzi wa kitaalam unaonyesha kwamba, miradi ya umeme inahitaji maji na pia kilimo cha umwagiliaji cha *Lower Moshi* kinahitaji maji hayo hayo. Kulikuwepo ulazima wa kugawa maji hayo ili miradi ya kuzalisha umeme na ule wa kilimo cha umwagiliaji usiathirike. Kazi hiyo, imeshafanyika na hivi sasa hakuna mvutano kati ya miradi hiyo. (*Makofit*)

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nataka niweke sawa kwamba *water right* ya asilimia 3.71 ilikwishatolewa kabla ya ahadi ya Rais. Nilitaka niweke sawa hilo. Kwa hiyo Rais, alikuja kutoa ahadi baada ya hiyo *water right* kutolewa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niulize swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa njia pekee ya kuwanusuru Watanzania katika baa la njaa ni kilimo cha umwagiliaji maji katika mashamba yetu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kujitahidi kulipa kipaumbele suala hilo la umwagiliaji kuliko mambo mengine yoyote?

(b) Kwa kuwa tuna Kiwanda cha *TANALEC* Arusha kinachoshughulikia mitambo kama hiyo ya kusukuma maji kwenye mito na kwa kuwa tuna mito mingi; je, Serikali ina mpango gani wa kukipa fedha za kutosha kiwanda hicho ili tuweze kutumia nyenzo zile kwa ajili ya kumwagilia mashamba yetu na kujinurusu katika baa hili? Ahsante. (*Makofî/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, uamuzi wa *water right* wa 3.7 ultolewa na Serikali, suala lilikuwa walitaka ibadilishwe hiyo, iwe juu zaidi. Mheshimiwa Rais, baada ya kuwasiliana na watalalam ikagundulika kuwa kiasi hicho hakiwezi kubadilika, ukibadili umeme utaathirika katika kituo cha uzalishaji cha Nyumba ya Mungu na vile vile hali hiyo ndiyo sababu ya jibu la msingi kuhusu swali lako.

La pili kuhusu Kiwanda cha *TANALEC*, suala hili limekuja wakati huu, siwezi kulitoa jibu mpaka kwanza niwasiliane na watalalam nisije nikatoa jibu la paparapara. (*Makofî/Kicheko*)

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Spika, ni lini huu mpango kamambe wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani utaanza?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, mpango ulishaanza tamgu 2002 kwa sababu ni mpango mkubwa, kamambe na mzito, kwa hiyo, unakwenda kwa awamu awamu. Kwa hiyo, naomba subira Mheshimiwa Mbunge tutafika hata huko. (*Makofî/Kicheko*)

Na. 33

Chakula Kilichonunuliwa kwa Ajili ya Njaa

MHE. STEPHEN M. KAZI (k.n.y. MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA) aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge (Februari, 2004), Serikali ililetia mapendekezo ya kupata fedha za ziada kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya njaa na kupungua kwa umeme vilivyosababishwa na uhaba wa maji unaotokana na kutonyesha kwa mvua kama ilivytarajiwa na kwamba fedha nyingi sana zimetumika kwa ajili hiyo:-

(a) Je, Serikali, imetumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kununua chakula cha njaa na ni kiasi gani cha chakula kiliagizwa kutoka nje ya nchi na wapi?

(b) Kwa kuwa suala la njaa limekuwa ni tatizo sugu hapa nchini kwa baadhi ya maeneo yakiwemo yaliyoko katika Ukanda wa Ziwa kama vile Kata za Kiloleli, Mwamanyili, Nyaluhande, Badugu, Shighala, Kabita, Igalukilo, Malili, Ngasamo, Kalemera na Mkula, zilizopo katika Jimbo la Busega. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha kilimo cha zao la muhogo ambalo linalostahimili ukame sambamba na mazao mengine kama mtama?

(c) Kwa kuwa miradi ya umwagiliaji ya Nyakaboja na Kalemera (Mwabujose) iliyopo katika Jimbo la Busega, bado haijakamilika kama ilivypangwa; je, Serikali inategemea kuikamilisha lini miradi hiyo ili iwe kichocheo cha Kilimo cha Umwagiliaji kwa ukanda huo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula uliotokea katika maeneo mengi ya nchi katika msimu wa 2003/2004, Serikali ilinunua tani 23,925 kutoka kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa Sh. 2,871,000,000/=. Chakula hicho kiliuzwa kwa wananchi wenye uwezo mdogo wa kununua chakula kwa shilingi 50/= tu kwa kilo moja. Ofisi ya Waziri Mkuu, ilitoa shilingi bilioni moja na milioni mia sita kwa Wilaya zilizohusika kwa ajili ya kusambaza chakula hicho. Katika kipindi hicho, Serikali ilinunua tani 10,000 za mahindi kutoka Bodi ya Nafaka ya Kenya kwa shilingi 2,099,556,432/=. Mahindi hayo yalisafirishwa hadi Musoma na Shinyanga kwa shilingi 1,264,576,000/=.

Namshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye alifanya mpango wa kupatikana kwa mahindi hayo alipotembelea Jamhuri ya Kenya mwezi Desemba, 2003. (*Makof*)

Katika mwezi wa Machi, 2004, Serikali ilinunua tani 22,000 za mahindi kwa tenda kwa shilingi 6,568,165,862/=. Mahindi hayo yalitoka Zambia tani 4,067.8, Ethiopia tani 1,660.7 na India tani 16,271.5. Serikali iligharamia usafirishaji wa mahindi hayo kutoka bandarini hadi kwenye maghala ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa iliyoko Kipawa kwa shilingi 114,161,400/=.

Serikali iligharamia uhamishaji wa tani 7,902 za mahindi kutoka Sumbawanga kwenda Shinyanga na Tabora kwa shilingi 225,360,000/=, tani 4,972 kutoka Songea kwenda Dodoma kwa shilingi milioni 200 na tani 9,064 kutoka Makambako kwenda Kipawa kwa shilingi 233,831,724/=, tani 2,006 kutoka Kipawa kwenda Dodoma kwa shilingi 120,465,753/= na tani 4,500 kutoka Kipawa kwenda Arusha kwa shilingi 317,197,630/. Hii ina maana kwamba, Serikali ilitumia jumla ya shilingi 15,614,314,801/= kununulia chakula kutoka ndani na nje ya nchi na kusafirisha chakula kutoka kwenye vituo vya ununuzi kwenda kwenye vituo vya usambazaji ambavyo ni Kipawa, Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Tabora na Shinyanga.

Vituo vya utafiti wa Kilimo vya Naliendele, Kibaha, Hombolo, Ukariguru, Maruku na Ilonga, vimekuwa vikifanya utafiti wa mbegu zinazostahimili ukame na magonjwa, zinazokomaa mapema na zinazotoa mazao mengi na kuzisambaza kwa wakulima. Kwa upande wa muhogo, vituo hivyo vimetafiti njia mbalimbali rahisi za kuandaa muhogo na kuutumia kuandaa vyakula vya aina mbalimbali vyenye ladha nzuri.

Mikoa na Wilaya mbalimbali zimekuwa zikihimiza kilimo cha muhogo na mazao mengine yanayovumilia ukame. Ningependa kuchukua nafasi hii kuzipongeza Wilaya za Mkoa wa Singida, Wilaya ya Serengeti, Wilaya ya Ukerewe, Wilaya za Mkoa wa Kigoma na baadhi ya viji vya Mkoa wa Dodoma, kwa kuitikia wito wa kulima muhogo na mazao mengine yanayoendana na hali ya hewa ya maeneo hayo. Maeneo yote yanayolima muhogo kwa wingi hayakuathirika na njaa.

Aidha, Idara ya Magereza imekuwa ikianzisha mashamba ya mfano ya kilimo cha muhogo kwa lengo la kupata chakula cha kulisha wafungwa, kuonyesha kilimo hicho kinavyopasa kufanywa na kuzalisha mbegu kwa matumizi yao na kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi. Nawapongeza sana Idara ya Magereza kwa kazi hiyo nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, miradi ya umwagiliaji ya Nyakaboja hekta 150 na Kalemela hekta 20, inatarajiwa kukamilika baadaye mwaka huu baada ya kuwasili kwa pampu zinazotumia nishati ya upemo zilizoagizwa kutoka Eldoret Kenya. (*Makof*)

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo: Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusiana na suala zima hili lakini hoja inabaki kwamba sasa Taifa linakua na watu wanakuwa wengi na njaa inakuwa ni hatari sana kama tunakwenda nayo kwa utaratibu alioueleza Naibu Waziri wa kukimbilia chakula hapa na pale wakati tuna ardhi ya kutosha. Mpaka sasa mpango wa umwagiliaji maji haujapewa dira sahihi ya namna gani tuendeshe kilimo cha umwagiliaji katika Taifa letu. Je, Wizara inaeleza nini sasa kwamba tuna mpango gani wa uhakika kuhusiana na suala la umwagiliaji? (*Makof*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane kuwa kuna tatizo la njaa, lakini papo hapo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali inatambua hilo alilolieza na ndiyo maana kutoka mwaka 2001 mkazo ulitiliwa katika kuandaa mpango kamambe wa umwagiliaji maji mashamba. Mpango huo unatekelezwa katika kila mkoa na wakati wa Bajeti atakayotoa

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, mtaona mtawanyo huo wa harakati za kufukuza njaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini kwa awamu. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Nawaona Waheshimiwa Wabunge wengi wana hamu ya kuuliza maswali ya nyongeza, lakini kikao kilichopita cha alhamisi maswali ya msingi ya mwisho mawili hayakupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, leo najitahidi kugawa muda ili kusudi maswali yote yaweze kujibiwa. Kwa hiyo, natoa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza katika swali hili nani anataka, wako wengi. Mheshimiwa Job Ndugai. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na pongezi kwa Serikali kwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni 15 kuwaokoa Watanzania na janga la njaa. Najua Serikali inafahamu kwamba Mkoa wa Dodoma na Singida ulipata mvua chini ya wastani na mvua yenyewe ilichelewa. Sasa Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba *SGR* Dodoma ambayo inahudumia Mikoa ya Singida na Dodoma mwaka huu litakuwa na chakula cha kutosha? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie kuwa *SGR* pamoja na madhara yote, yenyewe siyo Ghala la Taifa. Suala la kila mtu kuwa na chakula cha kutosha kulisha familia yake liko katika ngazi ya Kaya. Kwa hiyo, ninaomba tushirikiane naye Mheshimiwa Mbunge, tuwahimize wananchi kuweka akiba hiyo kwenye majumba na Kaya na kokote inakowezekana.

Lakini pamoja na hayo, Serikali ina mikakati mingi tu, kuna miradi mingi tu ya kutegeshea maji ya mvua, kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya *irrigation*. Sasa hivi nisingeweza kutaja miradi yote mara moja. Lakini zaidi ya hayo, kilimo cha muhogo ndiyo ukombozi. Tumegundua Dodoma ukiwa na mihogo njaa inakimbia. Tushirikiane kwa hilo. (*Kicheko*)

Na. 34

Kuvuja kwa Mitihani ya Kidato cha Nne

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (k.n.y. MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR) aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka mingi iliyopita hadi hivi sasa mitihani ya mwisho ya Kidato cha Nne ambayo huandaliwa na kutolewa na Baraza la Mitihani huwa inavuja (inakuwa kwenye mikono ya watahiniwa kabla ya wakati uliokusudiwa):-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge na wananchi wote kuhusu ukweli wa jambo hilo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inashindwa kabisa kudhibiti uvujaji wa mitihani husika?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dk. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Mikunguni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali Na. 25 la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, katika Mkutano wa 13 wa Bunge hili kuwa, kufuatia uvujaji wa kupita kiasi uliotokea mwaka 1998 ambapo Serikali ililazimika kufuta Mtihani wote wa Kidato cha Nne, hatua madhubuti zilichukuliwa ili kudhibiti hali hiyo isitokee tena. Kwa hiyo, tangu mwaka 1999 hadi sasa hakuna tukio lolote au haujapatikana ushahidi wowote wala dalili kuonyesha kuwa kumekuwa na tukio lolote la uvujaji wa Mitihani inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa maana ya Mitihani kuwa kwenye mikono ya Watahiniwa au watu wengine wasiohusika kabla ya wakati wake.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tangu mwaka 1999 hadi sasa hapajajiteza tukio lolote la kuvuja kwa mitihani ya Kidato cha Nne na Mitihani mingine inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania, ni dhahiri kuwa hatua zilizochukuliwa na Serikali, zimefanikiwa kudhibiti uvujaji wa Mitihani ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge, azingatie kuwa uvujaji wa mtihani ni mtihani au maana yake ni mtihani kuonwa na watahiniwa kabla ya muda wake. Kasoro hii imedhibitiwa vizuri. Makosa ambayo bado yanatokea ni yale ya udanganyifu kama vile watahiniwa kusaidiwa au kusadiana wakati wa kufanya mtihani, ambapo hatua kali pia huchukuliwa dhidi ya wahusika pindi wanapothibitika kufanya udanganyifu wa aina hiyo.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Tatizo lingine la uvujaji wa Mitihani inaelekeea ni usafirishaji au usambazaji wa mitihani na hili ni tatizo ambalo linatokana na kukosekana kwa pesa za kusafirishia mitihani. Je, Mheshimiwa Waziri, kwa hili analizungumzaje, ambalo ni tatizo linalolikabili Baraza la Mitihani?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na ufinyu wa Bajeti pamekuwa na tatizo katika usafirishaji wa mitihani na Kamati ya Huduma za Jamii tulipotembelea Baraza la Mitihani tulipata maeleo kwa ukamilifu na tumekubaliana na Kamati hiyo ya Bunge pamoja na Baraza la Mitihani Tanzania kuchukua hatua ili kuhakikisha kazi hiyo inafanywa kwa ufanisi. Kwa hiyo, katika Bajeti ya mwaka huu, ambayo iko tayari inajadiliwa hapa Bungeni, nitafafanua hatua mbalimbali ambazo tumezichukua kuhakikisha kwamba tatizo hili tunaondokana nalo kabisa.

MHE. NJELU E.M. KASAKA: Mheshimiwa Spika, pamoja na maeleo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, katika hatua walizochukua ili kukomesha hali hiyo, je, kuna Maofisa wa Wizara hiyo au wa Baraza hilo waliochukuliwa hatua na kuadhibiwa?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, pale mwaka 1998 ilipochukuliwa hatua ya kufuta mitihani, hatua kali sana zilichukuliwa kwa wahusika, hususan viongozi na uongozi mzima wa Baraza la Mitihani ulibadilishwa na uongozi wa sasa ndio ambao umesimamia jambo hili vizuri pamoja na kutumia teknolojia za kisasa zaidi katika kuchapisha mitihani na usimamiaji wake.

Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii, niwapongeze sana viongozi wa sasa wa Baraza la Mitihani kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makofî*)

Na. 35

Elimu ya Msingi iwe Miaka Kumi na Mbili

MHE. SOPHIA M. SIMBA aliuliza:-

Kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha na kwa kuwa elimu hiyo haikidhi hali ya kuwafungulia maisha vijana wetu kwani watoto wetu hawapati nafasi ya kuendelea na shule wakiwa bado wadogo sana. Je, Serikali haioni kwamba huu ni wakati muafaka wa kuangalia upya uwezekano wa kuongeza muda wa elimu ya msingi ili ufikie miaka kumi na mbili?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalî la Mheshimiwa Sophia Simba, naomba nitoe maelezo ya kiujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, elimu kwa watoto hutolewa katika asasi maalumu za utoaji wa elimu zinazoitwa shule kwa kufuata mitaala iliyoadaliwa kwa ajili ya ngazi mbili za elimu kwa kuzingatia umri. Ngazi ya kwanza ni elimu ya msingi ambayo hapa Tanzania hutolewa kwa watoto wa miaka 7 hadi 13. Kwa hiyo na mitaala yake imeandaliwa kwa kuzingatia umri huo. Ngazi ya pili ni elimu ya Sekondari Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Sita, ambayo hutolewa kwa miaka 6 kwa ajili ya watoto wa umri wa miaka 14 hadi 19. Kwa hiyo na mitaala yake imeandaliwa kwa kuzingatia umri huo. Elimu ya msingi huwafundisha watoto kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, pamoja na stadi za maisha ili waweze kujitegemea na aidha huwaandaa wawe tayari kupokea elimu ya sekondari. Elimu ya Sekondari huwaongeza ujuzi wa masomo ya Lugha, Hisabati, Sayansi na Maarifa pamoja na kuwaandaa waweze kupokea Elimu ya Juu, yaani Elimu ya Chuo Kikuu pamoja na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swalî la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Sophia Simba kuwa, baada ya mafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa MMEM (2002 - 2006) sasa ni wakati muafaka wa kuanza kuongeza elimu ya lazima kwa watoto wote iwe ya miaka angalau

kumi na moja ikijumuisha elimu ya msingi miaka 7, Dasara la I - VII na elimu ya sekondari ya kawaida miaka 4 Kidato cha I - IV. Katika hatua ya kwanza kuelekea kwenye lengo hilo, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004 -2009, utakaowafikisha kwenye lengo hilo angalau nusu ya wahitimu wa Darasa la VII ili watakapofika Kidato cha IV hawa wa mwaka wa kwanza wawemo shuleni Kidato cha I - IV angalau 50% ya rika lengwa kwa ngazi hiyo ya elimu (miaka 14 - 17). Mpango huo unaanza kutekelezwa kifedha katika Bajeti hii ya 2004/2005, lakini nafurahi kulitaarifu Bunge kuwa, tayari uandikishaji wa mwaka wa kwanza wa (MMES) 2004 - 2009 umefanywa mwanzoni mwa mwaka huu wa shule kwa kuwaandikisha Kidato cha 1 wanafunzi 147,011 sawa na 65% zaidi kuliko mwaka 2003 walipoandikishwa wanafunzi 99,744.

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na yanayotia matumaini ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza yafuatayo: Kwa kuwa pamoja na utaratibu ambao anausema bado tutakuwa na watoto wanaomaliza darasa la saba na wanakuwa mzigo kwa kushindwa kujitegemea. Je, haoni kwamba hawa watoto wa darasa la saba wanakuwa hawajapata elimu ya kutosha kwa vile wanamaliza shule wakiwa na miaka 14 au 15 tu?

Swali la pili, kwa kuwa walimu wa shule za msingi wanakosa motisha ya kufundisha masomo kisasa, masomo ambayo yanaweza kuwafanya watoto wamalize shule wakiwa wanajiamini. Je, kuna utaratibu wowote ambao Wizara inao wa kutengeneza *crash program* ya kuwapa walimu hao wa shule za msingi masomo ili wabadirilishe utaratibu wao wa kuwfundisha watoto masomo wakati watoto wanakuwa wanaogopa mashuleni? Ahsante. (*Makofit*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba, mpango huu wa elimu ya sekondari utawapokea nusu ya wale wanaohitimu darasa na tunategemea kufikia *Net Enrolment Ratial* ya asilimia 50. Kwa hiyo, kutakuwa na asilimia 50 ambao watakuwa hawakuendelea na elimu. Sasa hawa kwanza katika elimu ya msingi tumeiangalia upya mitaala.

Sehemu mojawapo ya mpango ule wa MMEM ilikuwa kuiangalia upya mitaala ili tuzingatie zaidi ndani ya mitaala ya elimu ya msingi na pia elimu ya sekondari tuzingatie zaidi katika kila somo elimu ya kujitegemea. Hilo linafanywa ndani ya shule za msingi. Lakini pia Serikali baada ya kuandaa MMEM na sasa MMES, sasa hatua inayofuata itakuwa ni kuandaa *Vocational Education Development Plan*, pamoja na *Higher Education Development Plan*. *Vocational Education Development Plan* ni mpango wa mafunzo ya elimu ya ufundi. Yaani kupanua hizi sekta ili ziweze kuwapokea wale vijana wanaomaliza darasa la saba wapate mafunzo ya ufundi.

Kuhusu sehemu ya pili, kwamba tunawaimarishaje walimu, hili ni suala la mafunzo kazini (*In-Service Training*), ambalo tumelipa uzito mkubwa katika mipango hii ya MMEM na MMES ili waweze kumudu kufundisha mitaala hii ambayo tumeirekebisha iwe na elimu ya kujitegemea, ili watoto badala ya kujifunza Hisabati tu moja kwa moja, wajifunze pia kitu kinachoitwa *Commercial Arithmetic* ndani ya Hisabati, yaani hesabu

ambazo ndani yake zinawafundisha biashara, hata wakimaliza elimu wanaweza wakatunza mahesabu yao ya biashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, Mafunzo ya Walimu Kazini (*In-Service Training*), tumeimarisha kwa kuzingatia jukumu hilo.

Na. 36

Cheo cha Major General katika Jeshi la Ulinzi

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Ulinzi wa Tanzania (JWTZ) ni chombo muhimu kilichoanzishwa mara tu baada ya Muungano wa Jamhuri yetu ya Tanzania hapo tarehe 26 Aprili, 1964 na kwa kuwa mionganoni mwa vyeo vya juu wanavyopewa walinzi wetu hawa ni cheo cha *Major General*:-

- (a) Je, katika kipindi cha miaka arobaini ya Muungano wetu ni Wanzanzibari wangapi waliofikia cheo hicho?
- (b) Je, katika muda huo ni Watanzania wangapi hadi sasa wameshafikia vyeo hivyo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, napenda kutoa maelezo ya ufanuzi kama ifuatavyo:-

Kulingana na Kanuni za Majeshi ya Ulinzi (*Defence Force Regulation*) Sura ya 7.02 Kifungu cha kwanza, Juzuu ya Kwanza, Utawala, iliyofafanuliwa na Sheria ya Ulinzi wa Taifa (Ibara ya 37) na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 148, Mamlaka ya kuwapandisha vyeo Maafisa wa Jeshi ni ya Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, kutokana na mapendelekezo ya Mkuu wa Majeshi, ambayo lazima yathibitishwe na Halmashauri Kuu ya Majeshi ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Kanuni hizi za Majeshi ya Ulinzi, Afisa wa Jeshi au Mpiganaji, atapandishwa cheo iwapo tu ipo nafasi ya kufanya kazi kwa cheo hicho kipyaa, amependekezwa na mamlaka husika na awe na sifa za kutosheleza kulingana na kanuni.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania Mwaka 1964, ambacho ni chombo cha Muungano, Maafisa wa Jeshi wapatao 38 wamepandishwa vyeo na kufikia cheo cha Meja Jeneral na wachache wamevuka na kufikia Luteni Jeneral na Jeneral. Vyeo hivyo vilitolewa kwa kufuata Kanuni za

Majeshi ya Ulinzi na si kufuata upande gani au sehemu gani ya Muungano anakotoka Afisa husika. Katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, hakuna sheria/utaratibu wa kugawana vyeo kutokana na Afisa mhusika anakotoka. Sheria hii ya Jeshi ndiyo msingi uliopelekeea Jeshi letu kuwa Jeshi lenye nidhamu, utii kwa Amiri Jeshi Mkuu, utii kwa Taifa, Viongozi na Wananchi, bila kujali itikadi ya kisiasa, dini, kabila au sehemu anakotoka mpiganaji. (*Makofî*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Katika maelezo yake amesema kuwa, Afisa ataweza kufanya kazi popote bila ya kuangalia wapi anatoka. Sasa je, katika maelezo yake naona sikupata majibu ni wangapi hasa wametoka Zanzibar, kwa sababu sidhani kuwa kutojibu ni wangapi wanatoka Zanzibar kunasaidia kunifanya mimi nielewe suala hilo?

Ningependa pamoja na hizo Kanuni za Kijeshi lakini siyo siri kwa sababu askari ni askari na anajulikana. Naomba nipate angalau ni wangapi waliotokea huko Zanzibar na ikiwa uwiano ni mdogo kwa nini inakuwa hivyo kwa sababu nchi hizi kiasili ni mbili? (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, sijui kama unazo takwimu sasa hivi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Khalifa hakunielewa, sikusema kwamba atafanya kazi popote katika Jamhuri, lakini kupandishwa cheo, kwa sababu kuna Sheria na Kanuni ambazo hatuwezi kuzibadilisha kwa hisia tu kwa sababu kwa kusema kwamba wangapi wametoka Zanzibar, tukianza kufanya hivyo, tutafikia mahali tutasema kwamba wangapi wametoka Arusha, wangapi wametoka Tanga, wangapi wametoka Pemba. (*Makofî*)

Hili ni jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, ambalo linafanya kazi kwa niaba ya Watanzania wote, kulinda Taifa letu bila kujali itikadi ya dini. (*Makofî*)

Na. 37

Vijana wa Zanzibar Kujiunga na JKT

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Je, ni vijana wangapi wa Tanzania Zanzibar wamejiunga na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2002 - hadi sasa?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa Julai, 1963 likiwa na majukumu ya kuwaunganisha vijana wa Taifa ili kuwa na upendo na umoja wa Kitaifa na kusahau tofauti zao za kikabila, kidini, rangi, jinsia na viwango vyao vya elimu, kutoa mafunzo ya ukakamavu, uzalendo, moyo wa kupenda kazi za mikono, ili kuwaweka vijana tayari kulitumikia Taifa lao na kuaandaa vijana ili wawe wakakamavu na wawe tayari kutoa msaada kwa Taifa lao wakati wa maafa na kuwafundisha na kuwaendeleza vijana katika nyanja za kijamii na kiuchumi ili kuwapa ujuzi kwa lengo la kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na kazi nzuri iliyokuwa imefanywa na JKT katika kutimiza majukumu hayo, mnamo mwaka 1994, utaratibu wa kuchukua vijana kujiunga na JKT ulisimamishwa kutokana na sababu za kiuchumi. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Rais wa Jamshuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kukubali utaratibu huu urejeshwe.

Baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

(a) Mwaka 2002 vijana wapatao 2,488 walichukuliwa katika Operesheni Mkapa na kupatiwa mafunzo katika Kambi za Ruvu na Makutupora, kati yao vijana 50 ni kutoka Zanzibar.

(b) Mwaka 2003 vijana wapatao 2,600 walichukuliwa na kupatiwa mafunzo katika Makambi ya Ruvu JKT, Makutupora na Oljoro, Zanzibar ilipewa nafasi ya vijana 100.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004 vijana wapatao 2,700 wanatarajiwa kujiunga na mafunzo ya JKT kwa kujitolea katika Operesheni Utandawazi. Awamu ya kwanza ya vijana wapato 2,000 wameshajiunga na mafunzo hayo katika Kambi za Ruvu, Makutupora, Oljoro na Bulombora. Awamu ya pili ya vijana 700 watajiunga na mafunzo hayo Julai, 2004. Vijana 100 kutoka Zanzibar kati yao vijana 50 wameanza mafunzo na vijana 50 wataanza mafunzo katika awamu ya pili Julai, 2004. Hivyo, jumla ya vijana 250 kutoka Zanzibar wamejiunga na JKT. (*Makofi*)

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Jeshi hili la Kujenga Taifa (JKT) linafundisha mambo mbalimbali wanajeshi wake, ikiwemo elimu ya kuimarisha uchumi wa Taifa letu kwa njia ya kilimo na ufundi; na kwa kuwa elimu hiyo ni muhimu pia kuieneza kwa vikosi vyetu vya JKU vya kule Unguja na Pemba; je, ni mara ngapi kikosi hiki kimetoa elimu hiyo kwa vikosi vyetu vya JKU ili kuboresha sasa na kuimarisha uhusiano zaidi wa karibu?

Swali la pili, kwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa ni kiungo kizuri cha kuwaunganisha vijana wa Kitanzania katika kujiimarisha kiuchumi, ulinzi wa nchi yao na pia kujenga maadili ya kudumisha uzalendo walionao na kwa kuwa vijana wengi

wamalizapo mafunzo yao hayo huajiriwa na jeshi hilo, je Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami sasa kuwa ni wakati muafaka kuwaajiri vijana kutoka Zanzibar kwenye Jeshi la Kujenga Taifa?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kwa kuwa yeeye alipitia jeshi hili kupitia Zanzibar na inaonekana amejengwa imara sana. (*Makofit*)

Mafunzo ya Kilimo mara ngapi tumeshirikiana na JKU, ushirikiano upo karibu sana, tunabdalishana mawazo na nataka niwahakikishie kwamba, mara nyingi Maofisa kutoka JKT wamekwenda mara kwa mara Zanzibar JKU. Hata mimi nimewahi kwenda na kuona mashamba ambayo JKU wanashughulikia. Kwa hiyo, siwezi kusema ni mara ngapi, lakini kwa mwaka hata kwa mwezi wanakutana mara kwa mara. Kuhusu kuajiri vijana kutoka Zanzibar, vijana wengi baadhi yao waliomaliza JKT wameajiriwa, wamejiunga na JKT katika nyanja mbalimbali, kutokana na sifa zao, lakini si kwa sababu ya mgao ni kutokana na sifa zao.

Na. 38

Tawi la *NMB* Mbarali Kutotoa Mikopo

MHE. BENSON M. MPESYA (k.n.y. MHE. ESTHERINA KILASI) aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Mbarali haina asasi yoyote ya uhakika inayowawezesha wananchi wake kupata mikopo wanapohitaji kwa ajili ya kilimo na biashara ndogo ndogo; na kwa kuwa kuna Tawi la *NMB* ambalo lingetegemewa kutoa mikopo kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo; na kwa kuwa Tawi hilo tangu lianzishwe halijawahi kutoa mikopo yoyote kwa wananchi: Je, ni sababu zipi za msingi zilizofanya Tawi hilo la *NMB* Mbarali lisitoe mikopop kwa wananchi kama ilivyo kwa Matawi mengine ya *NMB*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Ili kupanua huduma ya mikopo inayotolewa na *NMB* matawini, matayarisho mengi yanatakiwa kukamilishwa yakiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa matawi husika, kuweka vitendea kazi hasa mtandao wa kompyuta, kuajiri maafisa mikopo na kuwapatia mafunzo kuhusu utoaji wa mikopo na mengine. Aidha, benki inatoa kipaumbele kwa sehemu ambazo zina kiwango kikubwa cha shughuli za kiuchumi pamoja na huduma ya umeme wa gridi ya Taifa, ambao ni muhimu sana katika kuunganisha matawi kwenye mtandao wa kompyuta. Uwezo wa Benki ya *NMB* katika kuweka vitendea kazi vya kimtandao na kutoa mafunzo ya jinsi ya kutoa na kusimamia mikopo ni kati ya matawi 15 hadi 20 kwa mwaka. Hadi sasa, matawi 68 ambayo ni sawa

na asilimia 63 kati ya 108 ya *NMB* yanatoa huduma ya mikopo. Benki inaendelea kutekeleza mpango wake kwa kupanua huduma ya kibenki katika matawi yake. Serikali inaamini kwamba, matawi yaliyosalia yatakuwa yamefikia kiwango cha kutoa huduma ya mikopo ifikapo mwishoni mwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, *NMB* iko mbioni kuliunganisha Tawi la Mbarali katika mfumo mpya wa teknolojia katika muda mfupi ujao. Aidha, *NMB* itashirikiana na Mradi wa *Private Enterprise Support Activities (PESA)*, unaofadhiliwa na *USAID* na ambao unaendesha shughuli zake katika mashamba ya mpunga yaliyopo Mbarali. Mradi huo wa *PESA* umeanzishwa kwa lengo la kuinua maendeleo ya shughuli ndogo ndogo za kiuchumi katika nyanja mbalimbali na hivyo, *NMB* itashirikiana na mradi huo katika kuanzisha huduma ya mikopo itakayowawezesha wakulima kupata fedha za uendeshaji wa mashamba yao ya mpunga kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa uzalishaji.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na yanayotia moyo, nina maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa suala la mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo pamoja na kilimo ni sera ambayo imebuniwa na Chama Cha Mapinduzi na kwa sababu Sera hii tulijinadi na kuitoa katika Ilani ya Mwaka 2000 na katika maelezo yake anasema *NMB* Mbarali itakuwa tayari ifikapo mwaka 2005. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba tutakuwa tumejichelewesha kwa sababu tulijinadi kwamba tutatekeleza hili?

Pili, kwa kuwa wananchi wa Mbarali ni mionganini mwa wakulima hodari katika nchi hii na tatizo lao kubwa limekuwa ni nyenzo duni na mtaji hafifu. Je, isingekuwa vema basi hata huu mfuko wa pembejeo kama jirani zao wa Mufindi wamepewa na *NMB* Mbarali nao wafikiriwe? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, jumla ya matawi yote ni 108 na kuna nyenzo mbalimbali zinazohitajika katika kuhakikisha kwamba mikopo ile inayotolewa, haitapotea bure na inatolewa kitaalam. Bila shaka tumeanza kwa bahati mbaya Mbarali ni katika wale ambao bado wako katika mambo mengine ambapo baadaye watapata mikopo ile. Lakini bila shaka na wao vile vile watapata mikopo na wengine kila mmoja atasema hivyo hivyo na nakubali kila mmoja anasema mama yangu hakuna anayelia mama yako wewe, hapana. Kwa hiyo, muwe na uhakika kwamba nyenzo zikikamilika na nyie mtapata.

Kuhusu suala la pembejeo, wakitimiza masharti yanayohitajika hakuna matatizo kwa nini wasipate mikopo hiyo ya pembejeo.

Fedha za Akiba ya Serikali

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Mkutano wa Bajeti ilieleza kuwa inazo fedha za kutosha kwenye akiba yake za kuiwezesha kulipia mahitaji yetu:-

- (a) Je, ni kiasi gani cha akiba hiyo kuanzia 1 Julai, 2003 hadi 1 Januari, 2004?
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha kati ya hizo kimetokana na usafirishaji wa bidhaa zetu nje?
- (c) Je, kiasi cha fedha kwenye sehemu (b) ya swali hili ni asilimia ngapi ya akiba yote?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni ni ziada ya mapato na matumizi ya fedha za kigeni ambazo zimelimbikizwa na kuhifadhiwa na Benki Kuu kwa niaba ya Serikali. Akiba hii hupungua pale ambapo matumizi ya fedha za kigeni yanazidi mapato na huongezeka pale ambapo mapato yanazidi matumizi. Mapato ya fedha za kigeni yanatokana na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, mikopo na misaada toka kwa Mashirika ya Fedha ya Kimataifa na nchi Wafadhili na mapato yatokanayo na uwekezaji hapa nchini. Kwa upande mwagine, matumizi ya fedha za kigeni yanatokana na malipo ya bidhaa na huduma toka nje ya nchi, malipo ya mikopo, faida na gawio kwa wawekezaji nje ya nchi, safari za nje na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya mafupi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa dola za Kimarekani 300 milioni au asilimia 18.3 kutoka dola za Kimarekani 1,638.0 milioni mwishoni mwa Juni, 2003 hadi dola za Kimarekani 1,938.0 milioni mwishoni mwa Desemba, 2003. Ongezeko hili lilitokana na misaada na mikopo kutoka nchi wafadhili na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa pamoja na mauzo ya bidhaa na huduma zetu nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni vigumu kupambanua kiasi cha akiba ya fedha za kigeni kinachotokana na fedha za mauzo ya bidhaa na huduma zetu nje kwa kuwa fedha hazina sura ya mauzo wala misaada wala mikopo. Aidha, kwa kuwa mapato yatokanayo na mauzo yetu nje ni kidogo sana kuliko mahitaji ya fedha za kigeni kulipia bidhaa na huduma tunazoagiza na kutumia kutoka nje, kiasi cha mapato yetu kinachoingia kwenye akiba ni kidogo. Kwa mfano, kati ya Julai na Desemba, 2003, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi zilifikia dola za Kimarekani 711.0, wakati huo huo malipo ya nje kwa ajili ya bidhaa na huduma yalifikia dola za Kimarekani 1,076 milioni.

(c) Mheshimiwa Spika, ni vigumu kubaini kwa uhakika mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ni asilimia ngapi ya akiba ya fedha za kigeni. Hata hivyo, kwa kutumia takwimu za fedha za kigeni zilizopatikana kati ya Julai na Desemba, 2003 ikilinganishwa na akiba ya fedha za kigeni mwishoni mwa Desemba, 2003 jibu ni kwamba, kiasi cha fedha kwenye sehemu (b) ya swali hili ni asilimia 37 ya akiba yote.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika swali langu la msingi niliuliza kipindi maalum kuanzia tarehe 1 Julai, 2003 mpaka 1 Julai, 2004 na kutoptaka na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba hakuna uchambuzi wa takwimu. Je, sisi kama Taifa tunawezaje kujua mapato yanayotokana na kila sekta kama uchambuzi huo unashindikana kupatikana kwa mujibu wa majibu yake?

(b) Kwa kuwa sehemu kubwa ya mapato yetu inatokana na misaada na mikopo, kama wahisani hawataendelea kutoa mikopo na misaada hali ya fedha na uchumi wetu itakuwaje?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU): Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, haikuwa rahisi kutoa uchambuzi huo kwa fedha zinazopatikana nje ya nchi kwa sababu zinapita katika njia mbalimbali. Lakini kwa ujumla wake zitapatikana na ndio maana katika jibu la msingi nikasema kuwa sehemu hiyo ya (b), ukichukulia fedha zilizotumika kuanzia Januari mpaka Desemba, 2003 ni 37%, uchambuzi huo upo lakini labda Mheshimiwa Mbunge, hakuupenda ule uchambuzi uliotolewa.

Nakubali kwamba kwa sasa hivi kweli tegemezi yetu sana ni wafadhili lakini kila tunavyoendelea tunajitahidi kuondoka hapo. Katika Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango, alisema kwamba ni takriban 40% ndio ambayo tulikuwa tunawenza kujikimu wenyewe, sasa hivi ni 41% ambayo tunategemea kwa wafadhili na kila tunapoongeza nyenzo mbalimbali hapo tunawenza kujitegemea wenyewe na tunataka tuondoke hapa tulipo twende katika kujitegemea.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ndio tunamaliza kipindi cha maswali. Kabla hatujaendelea, leo sina tangazo la kikao chochote cha Kamati kilichopangwa lakini nieleze tu kwamba, leo ndio tunaanza mjadala wa hotuba zile mbili zilizotolewa siku ya Alhamisi na mjadala umepangiwa siku tano kuanzia leo hadi Ijumaa na kufikia mwisho wa kipindi hiki cha maswali, nina wasemaji 86 waliokwishajandikisha. Nafikiri kwa muda uliopo hao wanatosha sasa orodha itafungwa lakini hawa wanahakikishiwa kwamba, wote watapata nafasi ya kusema. (*Makofi*)

Vile vile nikumbushe kwamba, hiyo siku ya Ijumaa ni siku ya kupiga kura ya uamuza wa hoja ya Waziri wa Fedha, hiyo ni kazi ya Kikatiba, kura zinapigwa kwa kuita jina la Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja na kutokana na mazoea ya nyuma na makubaliano yaliyokuwepo sote tunatakiwa tuwepo Bungeni wakati huo wa kupiga kura. Napenda kukumbusha hivyo tu, kama kuna wanaoomba ruksa kwa dharura fulani fulani, wahakikishe kwamba, tarehe 18 Juni, 2004 siku ya Ijumaa wanakuwepo Bungeni kwa ajili ya kupiga kura ya kupitisha au kutopitisha Bajeti.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali kwa Mwaka 2004/2005

MHE. NJELU E.M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 43(5)(b) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Sera za Fedha na Uchumi na mwelekeo wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2004/2005.

Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba, kwa hoja zao nzuri walizoziwasilisha mbele ya Bunge hili, siku ya tarehe 10 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kwa kufiwa na mzazi wake.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni ya Kamati yangu, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki, safari hii kwa tiketi ya CCM. Kwa Chama cha UDP haya ni madhara waliyosababisha wao wenye na hivyo usemi wa busara kuwa “Kinga ni bora kuliko tiba”, umetimia. (*Makofi*)

Aidha, nawapongeza Wabunge waliochaguliwa kuingia katika Bunge la Afrika mapema mwaka huu. Hawa ni Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Athumanii

Janguo, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Balozi Gertrude Mongella na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pongezi zaidi kwa Mheshimiwa Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Hii ni sifa kwake binafsi, Bunge la Tanzania na Taifa letu kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuchaguliwa kwao kuongoza Taasisi za Kimataifa na Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa *SADC Parliamentary Forum*. Wote nawatakia mafanikio katika majukumu hayo mapya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2004/2005 ni nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania walio tayari kutumia mazingira mazuri yaliyowekwa na bajeti kujiletea maendeleo yao. Suala la kutokomeza umaskini na kuleta maendeleo ni suala la Serikali kwa upande mmoja kwa kuweka mazingira mazuri ya kiuchumi na kijamii na ni la kaya au mtu binafsi kwa upande mwingine. Ni wajibu wa kila mtu binafsi au taasisi kutumia fursa na nafuu zinazowekwa na Serikali kwa kufanya kazi zenye tija na faida ili kuondoa umaskini. Bajeti ya mwaka huu wa fedha kwa kiwango fulani ina mwelekeo huo wa kutoa fursa na nafuu itakayowawezesha Watanzania wenye nia ya kuondoa umaskini kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuondoa vikwazo katika upatikanaji wa leseni za biashara, kupunguza ada ya *visa* kwa wawekezaji wanaotembelea Tanzania, kupunguza gharama kwa wawekezaji katika sekta ya kilimo, kufuta kabisa ushuru kwa pembejeo na zana za kilimo, kufuta ushuru wa stempu na kuendelea kutoa ruzuku ya kusafirisha mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Mikoa mingine yenye mvua za uhakika, ni hatua ya kupongeza, nina hakika inalenga kuwawezesha Watanzania kuondokana na umaskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inapongeza hatua za Serikali za kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza sekta ya viwanda vidogo na vyenye ukubwa wa kati. Pamoja na pongezi hizo, Kamati haikuridhika na taarifa kwamba, fedha zilizotengwa kwa sekta hii katika bajeti inayomalizika, hazikutumika kwa sababu tu mwongozo haukuwepo. Kamati inashauri Serikali ikamilishe taratibu zake mapema ili fedha zilizotengwa zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhishwa na kazi nzuri ya kukusanya mapato ya ndani ya Serikali hadi kufikia kiwango cha wastani wa Sh.108 bilioni kwa mwezi. Hapa Serikali na hasa Mamlaka ya Mapato, wanastahili pongezi. (*Makofî*)

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kulifanya zoezi la kuongeza mapato na kupanua wigo wa kodi kwa uangalifu mkubwa ili lisithiri uthumi na makusanyo yenye yawe endelevu. Iwapo jitihada za kuongeza mapato zitadumaza uthumi,

kiwango cha makusanyo ya mapato kilichofikiwa hakitakuwa endelevu. Kodi lazima itumike siyo tu kwa kuipatia Serikali mapato bali kwa kuchochea kukua kwa uchumi pia.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika na kuipongeza Serikali kwa kuwarejesha Wastaafu waliopokea mafao yao kwa mkupuo katika utaratibu wa pensheni. Kitendo hicho kimewapunguzia Wastaafu matatizo ya maisha waliyokuwa wanakabiliana nayo. Hata hivyo, Kamati haikuridhika na hatua ya Serikali kuwafanya wasubiri hadi Januari, 2005. Taratibu za malipo haya zilipaswa kufanywa mara uamuzi wa kulipa ulipofikiwa ili kuwezesha Wastaafu kuanza kulipwa Julai, 2004. Miezi sita ya kusubiri kwa mtu ambaye hana mapato mengine ni muda mrefu sana, punguzeni muda huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi toka kwa wazalishaji kuwa urejeshaji wa malipo ya *VAT* unachelewa sana na kwamba hatua zichukuliwe ili kuondokana na tatizo hilo. Kamati imefurahishwa na hatua zilizoleenza katika Ibara ya 48(ii)(a) na (b) ya hotuba ya bajeti katika kulipatia ufumbuzi suala hilo. Ni vema hatua zaidi zikachuliwa ili wenyewe stahili ya kurudishiwa *VAT*, wawe wanarudishiwa mapema. Katika nchi ambayo taratibu za kupata mikopo ya kuendeshea kampuni ni ngumu kama Tanzania, kuchelewesha marejesho ya *VAT* kunaweza kusababisha kampuni kafilisika. Makampuni yanayosambaza mafuta ya petroli yanalamika sana kuchelewesha marejesho ya *VAT*.

Mheshimiwa Spika, hatua za Serikali za kujenga uchumi mpana, imara na tulivu, kujenga miundombinu ya barabara, mawasiliano ya simu, usafiri wa anga na reli, kuimarishe na kutoa huduma za jamii kama elimu, maji na afya, zinaridhisha. Kamati inashauri Serikali kuimarishe hatua na mikakati ya usimamizi ili kutotoa mwanya wa utekelezaji kuzorota na mafanikio yaliyopatikana kutoweka. Sababu za kuzorota uchumi na maendeleo katika miaka ya 1970 na 1980, imeelezwa zilitokana na mipango na mikakati kutokuwa endelevu. Mipango hiyo haikuwa endelevu kwa kukosa mitaji na usimamizi. Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali inaelewa hivyo na kwa hiyo haitalegeza usimamizi wa utekelezaji kuepuka kuzorota kwa uchumi na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio katika kujenga uchumi mpana, misingi ya uchumi wa Tanzania bado ni dhaifu na inaweza kuporomoka wakati wowote na maendeleo kuzorota. Katika kuhakikisha mafanikio yaliyopatikana yanakuwa endelevu, sekta zifuatazo zipewe kipaumbele na kuongezewa mgao wa fedha: Hali ya kilimo cha Tanzania si ya kuridhisha. Ni kilimo cha kubahatisha, msimu wa mvua nzuri, nchi inapata mavuno ya kutosha na msimu wa mvua chache nchi inakabiliwa na uhaba wa chakula na tishio la njaa. Mfumo mbaya wa uagizaji na usambazaji pembejeo, bei kubwa ya pembejeo, kuzorota kwa huduma za ugani, kukosekana kwa vyanzo vya uhakika vya mikopo na kukosekana kwa programu nzuri za kuendeleza kilimo, kumesababisha kilimo kutozalisha kwa uwezo wake hata katika msimu wenyewe mvua nzuri.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kutia moyo kuona kuwa hotuba zote mbili zimezungumzia umuhimu wa kilimo katika uchumi wa nchi hii. Tunapenda

kutahadharisha kuwa, mpango na mkakati wa kuondoa umaskini wa kipato hautafanikiwa bila ya kuboresha sekta ya kilimo. Kwa Tanzania kilimo maana yake mkulima mdogo. Pamoja na nia njema ya Serikali kuvutia wakulima wakubwa, uchumi wa nchi hii utaimarika na umaskini kutoweka kwa kuboresha kilimo cha mkulima mdogo. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Serikali iimarishe na kuboresha taratibu za usambazaji mbolea na pembejeo nyingine. Mwaka 2003 Serikali ilitoa ruzuku kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini lakini kutokana na usimamizi mbovu na maandalizi kutofanywa mapema, mbolea zilichelewa kufika, udhibiti wa bei ukawa mdogo na mbolea zikauzwa kwa bei kubwa. Tunatumaini hilo halitatokea tena msimu huu.

(b) Serikali iboreshe huduma za ugani ili kilimo cha mkulima mdogo kiwe na tija na kitumie teknolojia ya kisasa.

(c) Benki ya kutoa mikopo ya uzalishaji na uuzaji mazao ya kilimo, ianzishwe mara moja. Taarifa za utafiti wa muda mrefu kuhusu uanzishwaji wa Benki hii ni dalili kwamba, suala hili halina kipaumbele katika mipango ya Serikali. Serikali itamke benki itaanzishwa lini. Nakumbuka suala hili limepelekwa mpaka Halmashauri Kuu ya CCM kujadiliwa na Waziri wa Kilimo na likapata baraka lakini tunashangaa kuona kwamba, bado Benki haijafikia mahali pa kuanzishwa.

(d) Uzalishaji wa mazao ya kilimo uunganishwe yaani kuwe na *linkage* ya sekta ya viwanda ambayo ndiyo mtumiaji mkubwa wa mazao ya kilimo (*Agricultural Processing Industries*). Tunafurahi Mawaziri wote wawili wamezungumzia nia ya Serikali kushughulikia matatizo haya. Tunasubiri vitendo. Aidha, Kamati inashauri Serikali iendelee kusimamia masuala yote ya utafiti wa kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kilimo katika uchumi imara mara nyingi huwa ni wa mpito, siyo wa kudumu. Msingi muhimu katika maendeleo ya uchumi imara na endelevu ni viwanda. Hivi sasa sekta ya viwanda katika uchumi wa Tanzania ni ndogo na mchango wake katika Pato la Taifa ni chini ya asilimia 10 ukilinganisha na kilimo kinachochangia asilimia 48.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa sekta ya viwanda ni muhimu kwa vile kutaanzisha ajira mpya nyingi, kutaongeza mauzo nchi za nje, kutaongeza mapato ya uhakika ya fedha za kigeni, kutaongeza mapato ya Serikali ya ndani kwa njia ya kodi na ushuru mbalimbali, kutapanua soko la ndani la mazao ya kilimo, kutaiepusha Tanzania na janga la kuwa soko la bidhaa za viwandani toka nje na kwa jinsi sekta hii ilivyo, matumizi ya teknolojia ya kisasa yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sekta hii inakabiliwa na matatizo mengi, mionganii mwa mwatatizo hayo ni ya miundombinu hafifu, upatikanaji hafifu na gharama kubwa ya umeme, upungufu wa maji, mawasiliano yasiyoridhisha na ukosefu wa mikopo ya kuanzisha viwanda na ya uendeshaji. Hotuba ya Waziri wa Fedha, imezungumzia katika mtazamo wa Bajeti ya 2004/2005, kusaidia viwanda vidogo lakini iko kimya kwa

viwanda vikubwa. Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, baada ya kutaja sekta ya viwanda katika mapitio ya 2003, haikusema lolote kuhusu viwanda katika mpango wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kutoipa kipaumbele sekta ya viwanda ni hatari kwani uchumi wa Tanzania hautaimarika bila ya kuwa na sekta imara ya viwanda. Nchi zote zenye uchumi imara msingi wake mkubwa ni viwanda, kwa hiyo, mpango wa Serikali na Bajeti ya 2004/2005 vina mapungufu kwa kutoipa umuhimu sekta ya viwanda.

Kwa hiyo, Kamati yangu inashauri Serikali kutatua vikwazo vinavyosababishwa na miundombinu hafifu, kuwa na taratibu za kodi zinazowezesha sekta hii kukua na la muhimu kabisa kuanzisha Benki ya kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kwa sekta hii. Katika nchi nyingi kuna Benki za aina hii, kwa hiyo, Kamati haioni sababu ya kuchelewesha kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ya Viwanda. Kama uamuzi ni kuibadili Benki ya Raslimali kuwa Benki ya Viwanda, basi zoezi hilo lifanywe haraka.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa umeme mwangi, wa uhakika na wa gharama nafuu ni kwa lazima kwa maendeleo ya sekta ya kilimo na sekta ya viwanda na kwa maendeleo ya uchumi kwa ujumla. Tanzania haina umeme wa kutosha na uliopo hauaminiki sana na gharama yake ni kubwa. Upatikanaji wa umeme wa aina hii unakwamisha sekta nyingine kukua hasa sekta ya viwanda na kunakatisha tamaa wawekezaji kuwekeza Tanzania. Aidha, gharama ya umeme na matatizo ya upatikanaji wake, vimesababisha kuongezeka kwa matumizi ya mkaa na hivyo kusababisha ukataji miti kwa wingi, hali inayotishia usalama wa mazingira. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, amezungumzia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ili kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, kauli kama hizi zimetamkwa mara nyingi lakini hakujawa na mkakati thabiti wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Badala yake bei ya umeme inapanda na matumizi ya kuni na mkaa yanaongezeka vijiji na mijini na kuhatarisha kutoweka misitu ya asili ya nchi hii.

Mpango wa kupeleka umeme vijiji bado uko kwenye *Drawing Board*. Kamati inaishauri Serikali, kauli zake ziambatane na vitendo makini ili kuinusuru nchi hii.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati lazima yapunguzwe. Lakini hilo linawezakana tu iwapo umeme utapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu tuliuopata umeme wa maji umeshakuwa hauaminiki kutohana na ukame wa mara kwa mara. Aidha, umeme wa dizeli ni wa ghali. Kwa hiyo, matumaini tuliyonayo ni kuzalisha umeme kwa kutumia gesi na makaa ya mawe, ambavyo vyote vinapatikana kwa wingi Tanzania. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na tangazo zuri la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kuwa Mradi wa *SONGAS* utaanaza uzalishaji umeme Julai,

2004, bado umeme wake utakuwa ni ghali sana kwa taarifa tulizonazo. Umeme wa *SONGAS* na ule wa *IPTL* utaigharimu Serikali kila mwezi siyo chini ya Sh.5.5 bilioni. Nadhani ndiyo maana Wizara ya Nishati na Madini mwaka huu imetengewa Sh.133.04 bilioni kwa Matumizi ya Kawaida katika bajeti hii. Hata hivyo, miradi yote miwili inatazamiwa kuzalisha *MW 210* tu.

Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha uzalishaji umeme kwa makaa ya mawe ya Mchuchuma. Mradi wa Mchuchuma umekadirwa kuzalisha *MW 400* na taarifa za mwanzo zinaonyesha gharama zake zitakuwa chini ya miradi hiyo miwili ya *SONGAS* na *IPTL*. Aidha, Kamati inahimiza Serikali kukamilisha taratibu zake mapema ili mradi wa kupeleka na kusambaza umeme vijijini uweze kuanza mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, msingi mwengine muhimu wa maendeleo ya uchumi wowote ule ni elimu. Ni lazima Uchumi na Utawala viendeshwe na watu wenye elimu. Kwa msingi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni na kutekeleza Mradi wa MMEM kwa Elimu ya Msingi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa na kutekeleza miradi kwa Elimu ya Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu, ambayo ni muhimu katika kuhakikisha kwamba nchi inajitegemea.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu ambalo Kamati ililijadili ni matumizi ya fedha yenye mafanikio. Ni jambo zuri kuwa Serikali imeongeza mapato na Wizara ya Fedha hupeleka fedha kwenye Wizara na Mikoa mbalimbali kwa wakati na kwa viwango vya kuridhisha. Lakini bado kuna suala la kuhakikisha kuwa, fedha zilizopelekwa zinafanya kazi iliyokusudiwa na kwa mafanikio (*Value for Money*). Kamati inaamini kuwa kama fedha zinazotolewa zingetumika kama ilivyokusudiwa, basi hali ya uchumi wa Tanzania na hali ya huduma za jamii zingekuwa bora zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa Wizara ya Afya ambayo imekuwa ikiongezewa bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa miaka ya hivi karibuni. Mwaka 2002/2003, Wizara ilipewa Shilingi 58.06 bilioni, mwaka 2003/2004 Sh.83.58 bilioni na mwaka huu Sh.104.46 bilioni. Pamoja na bajeti kuongezeka, bado katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali kuna malalamiko ya ukosefu wa madawa na baadhi ya mahitaji ya wagonjwa kama vile maji ya *drip* na kadhalika. Hapa inawezekana tatizo siyo fedha bali ni usimamizi wa fedha na uwajibikaji kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi mbovu wa utendaji na kukosekana kwa uwajibikaji ni mambo yaliyotapakaa sehemu nyingi katika Wizara na Idara za Serikali na hivyo kupunguza ufanisi wa ongezeko la bajeti ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi na ufuutiliaji wa utendaji vinginevyo ongezeko la bajeti halitaleta manufaa zaidi kwa wananchi na kwa uchumi wa Tanzania. Ufujaji wa fedha uliojitokeza katika baadhi ya maeneo kwa Mradi wa MMEM iwe ni kiashiria kwa Serikali na kwamba shughuli zake zote zisimamiwe kwa karibu kama inavyofanywa kwa MMEM.

Kamati ilijadili na Mawaziri suala la kuwa na Mpango wa Taifa unaotoa mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu. Kamati yangu inaona kuwa hivi sasa Tanzania haina mpango wa maendeleo unaoelekeza jinsi raslimali na raslimali watu

vitakavyopatikana, vitakavyotumika na matokeo yake ni nini. Hivi sasa hakuna mpango unaojaribu kuainisha kwa mfano, jinsi sekta ya viwanda itakavypanuka kutokana na tija katika sekta ya kilimo na jinsi mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa (*GDP*), unavyoweza kupungua hatua kwa hatua bila ya kupunguza umuhimu wa sekta yenewe katika uchumi wa Taifa. Hakuna mpango unaoashiria/unaoainisha mahitaji ya wataalam mathalani katika sekta za kilimo na viwanda kwa sasa na katika kipindi cha miaka mitano, sita, ijayo. Kuna haja ya kuainisha pia katika mpango uwekaji akiba, uwekezaji na ukuaji wa uchumi na suala la ongezeko la watu wasio na ajira na kupanuka kwa ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ina maoni kwamba, kazi hizi na nyingine nyingi zinaweza kufanywa vizuri na Tume ya Mipango, ambayo itakabidhiwa masuala ya kuchambua uchumi na kutoa maelekezo jinsi ya kutumia raslimali na matarajio kutokana na utumiaji huo wa raslimali hizo. Tulichonacho sasa ni programu ambazo hazina uratibu wa pamoja na ugawaji wa mapato ya Serikali kwa Wizara na Idara mbalimbali inayofanywa na Wizara ya Fedha. Tunafikiri Dira ya Taifa ya 2025, Mkakati wa Kuondoa Umaskini na Utekelezaji wa Malengo ya *Millennium*, haviwezi kuchukua nafasi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inashauri Serikali kufikiria tena kuwa na Tume ya Mipango. Tunaamini Tume itasaidia sana kuchambua uchumi, kuelekeza namna ya kukua kwa uchumi na kuainisha jinsi mafanikio katika sekta moja yatakavyosaidia kukua kwa sekta nyingine na ufuutiliaji wa aina moja. Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003 katika ukurasa wa 127 wanakiri hivi: “... imebainika kuwa mfumo wa ufuutiliaji nchini hautoshelezi matarajio kwa vile bado haujazingatia ushiriki wa sekta zote. Kila sekta ina mfumo wake wa ufuutiliaji bila kuwa na uhusiano na sekta nyingine. Hivyo, panahitajika utaratibu utakaowezesha kuratibu mifumo mbalimbali ya ufuutiliaji iliyopo”.

Kwa hiyo, tunafikiri hali kama hii au mambo kama haya yanaweza kufanywa na Tume hii ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza utegemezi wa bajeti kwa misaada ya nje kwa mwaka wa tatu mfululizo. Kiwango cha utegemezi kimeshuka toka asilimia 47 mwaka 2002/2003, hadi asilimia 41 katika bajeti hii. Hata hivyo, asilimia 41 bado ni juu mno, Kamati inashauri juhudzi zaidi zifanywe kiwango hiki kipungue zaidi. Kiwango cha utegemezi kinaweza kupungua sana iwapo Serikali itajizuia kupanua uwanja wa matumizi (*Expenditure Base*) katika mambo mbalimbali. Mfano wa kupanua uwanja wa matumizi ni pamoja na kuweka mtandao wa *PCB* hadi Wilayani wakati ufisadi na rushwa bado vinazidi kukata mbuga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali zenyе kulenga kumwezesha Mtanzania kiuchumi. Hatua hizo ni pamoja na kufuta kodi mbalimbali zinazofikiriwa kuwa ni kero, kuunda mfuko wa kuendeleza viwanda vidogo, kuanzisha *Unit Trust* na kuanzisha Mfuko wa Dhamana ya Mikopo. Hatua hizi ni nzuri lakini hazitoshi na hazieleweki kwa wananchi wengi. Elimu inahitajika ili wananchi wajue

hatua hizi za Serikali zinahusiana vipi na mkakati wa kuondoa umaskini na kuwawezesha wao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuandaliwe mpango mahususi wa kuwawezesha wananchi kiuchumi, mpango utakaojumuisha pamoja na mambo mengine, elimu ya uanzishaji na uendeshaji miradi, upakatikanaji wa mikopo na kutafuta masoko ili kuwezesha Watanzania kuingia kwenye utandawazi wakiwa washiriki katika uchumi wa nchi yao badala ya kuwa watazamaji tu. Suala hili la uwezeshaji wananchi kiuchumi ni gumu lakini linawezakana dhamira ikiwepo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Serikali ilifuta kodi mbalimbali zilizokuwa zinakusanywa na Halmashauri za Wilaya na badala yake imeweka utaratibu wa kutoa ruzuku kwa Halmashauri. Utaratibu huo unaendelea katika Bajeti ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na marekebisho ya kodi yaliyofanywa lakini inashauri kuwa, utoaji ruzuku usipofanywa kwa uangalifu unaweza kudumaza baadhi ya Halmashauri ambazo zingeweza kukua kwa kuongeza mapato kama zingeendelea na utaratibu wa zamani. Aidha, baadhi ya Halmashauri zina maeneo makubwa na utoaji ruzuku usipozingatia hilo maendeleo yake yataathirika. Kamati inashauri uchunguzi ufanywe ili ruzuku iwe kichocheo na siyo kikwazo kwa maendeleo na ufanisi wa huduma kwa baadhi ya Halmashauri. Kuna taarifa kwamba, mradi wa kuweka taa barabarani katika Jiji la Dar es Salaam umekwama baada ya kodi mbalimbali za Halmashauri kufutwa mwaka 2003. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla bajeti ni nzuri na ikitekelezwa kikamilifu na usimamzi imara itasaidia katika mkakati wa kuondoa umaskini na kujenga uchumi imara. Nawapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya katika hatua za mwanzo za bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri kwa kuzingatia ushauri wa Kamati katika mambo mengi na kwa ushirikiano wao mzuri na Kamati yangu. Aidha, nawapongeza kwa kushirikisha Wadau mbalimbali katika kuandaa bajeti kwa mwaka wa pili mfululizo. Nadhani ni nchi chache zinazofanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, Kamati inaunga mkono hoja zote mbili. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Baada ya Msemaji wa Upinzani, wasemaji wanne wa kwanza watakuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Edward Ndeka, Wabunge wapya wapya wale. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFISHAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba mpokee shukrani zetu za dhati kwa

kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) Toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwa niaba yangu na Kambi ya Upinzani, kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na familia zao, kwa kuondokewa na baba yao mzazi. Mwenyezi Mungu, ailaze pema roho ya Marehemu peponi na wafiwa awape subira, pia namwomba Mwenyezi Mungu awape subira wafiwa. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwa undani kuhusu bajeti, naomba nikumbushe kauli ya Rais Mkapa, aliyoitao hapa Bungeni 12 Februari, 2004 juu ya matatizo ya kisiasa Zanzibar kufuatia Uchaguzi Mkuu uliopita. Rais alisema: "Matukio ya Januari 26 - 27 mwaka 2001 yamebaki kama kasoro na si hulka ya Watanzania. Tunapenda mfumo endelevu wa ushindani wa kisiasa amba ni wa kistaarabu, huru na wa amani Zanzibar na Tanzania nzima". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika katika Bajeti ya Waziri wa Fedha ukurasa wa 40 anasema: "Kutokana na ongezeko la matukio ya ujambazi nchini, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka ujao na vitendo vingine vya uhalifu, Bajeti ya mwaka 2004/2005, imeongeza mgao wa fedha kwa vyombo vya ulinzi na usalama". Mwisho wa kunukuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kauli hii ya kuchanganya mambo ya uchaguzi na vitendo vya ujambazi na uhalifu, kwa lugha rahisi na kutokana na uzoefu wetu wa tarehe 26 - 27 Januari, 2001 kama alivyotukumbusha Mheshimiwa Rais na matukio ya Bariadi ya gari la CUF kuvunjwa na Viongozi wa CCM na zaidi kuanzishwa vikosi vya hiari (*Volunteers*) huko Zanzibar na moja katika kambi zao kuitwa KISAGO (*TORTURE CAMP*) ambayo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri, ni vielelezo tosha kwamba, Watanzania wasitegemee kuwa na uchaguzi ulio huru na haki. Jambo ambalo litazorotesha sana maendeleo na kazi kubwa ya kiuchumi tuliyofikia hivi sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba tukumbuke Hotuba ya Rais, kwani hakuna Mtanzania anayejua haki yake na atakayekubali kunyang'anywa kirahisi. Tunasema haya kwa kuipenda nchi yetu, iendelee kuwa ya amani na utulivu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, tuliochagua kutuwakilisha na kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika. Pongezi za pekee tunazitoa kwa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Naamini wananchi wa Ukerewe wataitunza heshima hiyo kwa maslahi ya Taifa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni ila naomba nimkumbeshe tu si Vyama vya Upinzani ndio vinavyowafukuza wanachama wao waliochaguliwa na watu, hata CCM hufukuza wanachama wake kama nilivyofukuzwa mimi mwaka 1988 wakati nikiwa Mbunge niliyechaguliwa na wananchi wa Wawi. Aidha, tuliwahi kumfukuza Makamu wa Rais na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, mradi ukivunja maadili ya Chama utafukuzwa na hata huko CCM ulipo unaweza kufukuzwa kama utavunja maadili yao. Hiyo ndio siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu na Manaibu wao pamoja na Wakuu wa Vitengo na asasi zilizo chini yao, wote tunawapongeza kwa kuratibu mipango na mwenendo wa uchumi pamoja na kukusanya mapato hadi nchi yetu kuweza kujijengea sifa ya kuwa pahali pazuri pa kuwekeza na uvunaji wa raslimali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa waelekeze nguvu zao, ujuzi wao katika kumtoa Mtanzania ndani ya dimbwi la umaskini, kwani ni kwa kufanya hivyo tu ndiyo kazi iliyokwisha fanywa na inayoendelea kufanywa itaonekena na manufaa kwa Mtanzania wa kawaida. Hivi sasa bado mifuko ya Watanzania walio wengi haina kitu. Bado Watanzania hawajaona matunda ya raslimali zao kama madini, bahari, mbuga za wanyama na kadhalika kama zipo kwa maendeleo yao au ya wageni.

Mheshimiwa Spika, Rais Mkapa katika hotuba zake za kila mwezi alisema “Bajeti ni kipimajoto cha uhai wa mtu na afya ya uchumi wa Taifa...” “Daktari mzuri wa uchumi ataitumia bajeti kutoa tiba ya kupambana na umasikini na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania, pato la wastani la Mtanzania kwa kutumia dola za Kimarekani na bei za mwaka 1992, pato la Mtanzania limekuwa likishuka mwaka hadi mwaka toka dola 85.2 mwaka 1995 mpaka dola 57.2 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika,kama nilivyosema katika bajeti ya mwaka 2003, kigezo cha Kimataifa juu ya kiwango cha chini cha mtu kuweza kuishi ni dola moja, wakati kigezo cha Serikali ni Sh.330 kwa Jiji kama Dar es Salaam. Je, kutokana na kupungua huku kwa pato la Mtanzania, Bajeti ya 2004/2005 inachangia katika kupambana na umasikini?

Mheshimiwa Waziri Kigoda katika Hotuba yake ya 2004/2005 alitaja kwa upana majukumu ya Wizara yake na kwamba yanatokana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo ndani yake kuna utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2000 hadi mwaka 2025 na Sera mbalimbali za kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, tumeona *Working Draft* ya matayarisho ya mpango wa muda wa kati na mtazamo wa bajeti kwa 2004/2005 - 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili Tukufu ni lini mpango huu utatumika rasmi, kwani kutokuwa na mpango wa muda wa kati ni sawa na kutabiri tu kwamba mpango wa muda mrefu utafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri mpango wa muda wa kati uharakishwe ili wananchi waone kama kweli wanaweza kuondokana na umasikini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tulilonalo Tanzania ni utekelezaji wa mipango yetu na maamuzi yetu. Sera zetu zote zinaelekeza katika kumtoa Mtanzania katika dimbwi la umaskini, lakini hali halisi ya utekelezaji wa azma hiyo haiendani na sera yenyewe. Kwa mfano, hatuwezi kuondoa umaskini wakati Watanzania hadi leo, ama kupitia mmoja mmoja, vikundi vyao vya ushirika au Serikali yao, hawawezi kushika raslimali ya madini. Nafurahi kwa upande wa uwindaji kidogo kuna ishara ya kuwarithisha Watanzania, lakini kuna haja ya kuongeza kasi.

Mheshimiwa Spika, raslimali ya madini ndio ungekuwa ukombozi wa haraka ili kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 kama utekelezaji wa mpango wa muda wa kati, ungekuwa unaandaliwa vema katika mtazamo wa sekta hiyo kuchangia asilimia 20 hadi 30 ya Pato la Taifa ifikapo 2025. Hivi sasa kutokana na mpango huo, Serikali imepanga hadi kufikia 2025 sekta ya madini iwe imechangia asilimia 10 tu ya Pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naelewa kwa nini Serikali imepanga hivyo, ni tatizo la *mind set*. Bado ipo imani kwamba, Tanzania hatuna utaalam wa mambo ya madini, lakini sio kweli. Kinachokosekana ni mipango ya namna ya kuvuna utajiri huu wa madini, hivi sasa wapo Watanzania waliwekeza kwenye dhahabu (akina *Two Drums*). *Two Drums* ni Kampuni iliy Chunya kwa Mheshimiwa Njelu Kasaka na almasi akina *El Hilal Minerals*, wanachohitaji ni msaada wa Serikali tu katika uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali imewekeza asilimia 50 na haikuweza kupata mgao hata siku moja katika kipindi cha miaka 35 na hatimaye kuuza hisa zake 25% kwa USD 1,000,000/- na kubakiwa na 25% kwa muda wa miaka kumi bila ya kupata mgao wowote na kuambiwa kuwa mgodi unaingiza hasara na mwekezaji anaendelea kuwekeza kwa kukopa mamilioni ya Dola za Kimarekani (24 milioni) na wala hafungi virago akaondoka na Serikali inaendelea kumwamini, hili ni tatizo. Kwa hiyo, tatizo hili ni la *mind set*. Huu ni mgodi ambao Serikali ina hisa, je, inawezekanaje Watanzania wakaambulia kitu kwenye migodi ya dhahabu ambayo kwa mujibu wa taarifa za kitaalamu migodi yetu ina uwezo wa kutoa dhahabu *25m.oz* wakati hivi sasa migodi iliyopo inatoa wastani wa *1m.oz* kwa mwaka?

Tuelewe kuwa madini ni raslimali inayomalizika kwa haraka, kwa mfano, *Geita Mines* ilianza mwaka 1938 na ilikuwa na uwezo wa kuzalisha *900,000 oz* na ilipofika 1966 (miaka 28 tu) mgodi ulifungwa. Tukumbuke kuwa miaka hiyo teknolojia ya uchimbaji ilikuwa duni. Je, leo ambapo teknolojia ni ya hali ya juu mgodi si utaendelezwa kwa miaka 10 tu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa mafuta ndio uwekezaji mgumu na wa hatari (*Risk Investment*), lakini Mikataba yake inaonyesha kuwa ni ya manufaa zaidi kwa wananchi kuliko ile ya madini kama takwimu zinavyoonyesha. Aidha, faida

inayoongezeka kwenye madini haina kodi wakati kwenye mafuta, kuna mahesabu ya kodi yanatakiwa yatumike. Kitu kinachoitwa *Profit Sharing* kwenye madini hakuna wakati kwenye mafuta inakuwepo kutegemea ongezeko la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika ukilinganisha mapato inayopata moja kwa moja Serikali na yatakayopatikana kwenye utafutaji na uchimbaji wa mafuta ni kama ifuatavyo: Kwenye madini *royalty* dhahabu ni asilimia tatu na kwenye almasi ni asilimia tano lakini kwenye petroli ni asilimia kumi na mbili na nusu pamoja na hiyo unakuwa na *share* katika mafuta.

Kwenye *Income Tax, mining* ni asilimia thelathini na kwenye *petroleum* ni asilimia thelathini.

Mheshimiwa Spika mlinganisho wa mapato ya moja kwa moja ya madini kwa nchi kama Ghana, Namibia, Cambodia, utaona angalau wenzetu wana viwango ambavyo vinalinda raslimali za nchi zao, ni tofauti na ukarimu wa nchi yetu (kwa gharama za wananchi wetu). Sisi ni wakarimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Ghana, *royalty* wanatoa asilimia tatu mpaka kumi na mbili. *Income Tax* ni asilimia thelathini na tano, *Resources Rent Tax* ni asilimia ishirini na tano na *state equity* ni asilimia kumi mpaka thelathini. Wakati Tanzania tunayo asilimia tatu kwenye dhahabu, asilimia tano kwenye almasi na kwenye *Income Tax* ni asilimia thelathini lakini hailipwi kwa sababu kwa wawekezaji wamekopa mpaka watakapolipa madeni yao ndipo wanaweza kulipa *Income Tax*. Kwa hiyo, unategemea kutokana na ile niliyoeleza ya Geita, inawezekana kabisa mwekezaji akaondoka bila kulipa *Income Tax* hata siku moja. Pamoja na Serikali kujijengea sifa ya kukusanya kodi, lakini mapato yote ya kodi ni asilimia 12.1 ya Pato la Taifa, wakati Serikali inategemea misaada na mikopo kwa zaidi ya asilimia 40, ili tupunguze kutegemea misaada, tunahitaji kukusanya angalau asilimia 20 ya Pato la Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nusu ya mauzo yetu ya nje ni madini na hasa dhahabu na almasi. Kwa nini tusiige kama Botswana, Afrika ya Kusini na Ghana, ambao mapato yao yanayotokana na madini, hayapungui asilimia 30 mpaka 40 ya mauzo kama kodi kwa Serikali?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba iechezwe ni kwa nini Serikali inashindwa kufanya utafuti wa kina kabla ya kuangalia sheria zetu nyingine kwa mfano, Sheria ya Utafutaji Mafuta ambayo kwa kiasi fulani inalinda maslahi ya Taifa na kuangalia nchi nyingine kama Ghana ambao wana dhahabu kama sisi Au tunatoa takrima? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na udanganyifu unaofanywa na Makampuni ya nje, kutokana na kutokuwa na viwanda vyetu vya uongezaji wa thamani (*Added Value*) ya madini tunayozalisha, tumejikuta tunapoteza wastani wa Dola 1,321,844.94 kutokana na kusafirisha nje madini yenye uzito wa *ounces* 4376.97 kwa ajili ya usafishaji. Hii ni kwenye dhahabu tu bado almasi na madini mengine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri ili kuondoa mianya ya udanganyifu, ni kujenga viwanda vyetu kwa ajili hiyo kama ilivyokuwa Kiwanda cha *TANCUT* Iringa cha kuchonga almasi ambacho kimeuliwa. Kuanzisha *Refinary* yetu ya dhahabu ili hatimaye tupige marufuku uuzaji wa madini ghafi. Hatua hii itaongeza thamani ya raslimali ya madini yetu na ukuaji wa Pato la Taifa katika madini utaongezeka maradufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, udanganyifu katika madini ni mkubwa mno. Kabla ya Serikali kutekeleza maamuzi yake ni bora kwanza ijiandae na kujiandaa huko ni kuwashirikisha wataalam kufanya utafiti wa kina, sio baada ya wawekezaji kufunga Mikataba na kuchukua raslimali zetu ndio tuanze kutafuta utaalamu ambao hata tukiupata wawekezaji watakuwa wamekwisha kuvuna vya kutosha. Bunge kwa kuwa lipo kwa ridhaa ya wananchi ni bora lishirikishwe ili kuepuka mambo kama ya *IPTL* na *TTCL*, ambapo Watanzania inawaongeza umaskini kwa kuwabebesha mzigo wa gharama na madeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua zifuatazo zikichukuliwa itasaidia sana kubana mianya ya udanganyifu:-

(i) Wawekezaji walazimishwe kukopa katika mabenki yetu na kama mabenki yetu hayana fedha za kutosha, Benki Kuu iingilie kati kusaidia kupatikana kwa mikopo hiyo, ili tuepukane na kuwa na mzunguko mdogo wa fedha na akiba yetu kuwa ndogo. Aidha, tutaweza kudhibiti mserereko wa fedha yetu ambayo mwaka 2002 ilikuwa Sh.966.6 kwa Dola na sasa ni Sh.1038.6 kwa Dola, sawa na upungufu wa asilimia 7.4 kwa mwaka 2003;

(ii) Makampuni mapya ya uwekezaji masharti yao yaangaliwe upya ili kulinda maslahi ya Taifa. Ni vema Serikali ikawashirikisha Wabunge kwa kuitia Kamati za Kisekta ili kupata ushauri wao; (*Makofi*)

(iii) Pale ambapo Serikali ina hisa isiishie kubaki kwenye Bodi tu, bali wawepo jikoni ili tulinde maslahi ya Taifa. Tumekwishaibiwa vya kutosha, kule Mwadui sisi kwenye jiko hatupo, wanachambua almasi wanavyotaka wao, halafu sisi tunapokea kile ambacho wao wametueleza kwa sababu sisi tuko kwenye Bodi tu; na

(iv) Utaratibu wa kuwaachia wenyewe kuwekeza kukopa bila ya kutathmini mikopo hiyo na kufuutilia vifaa vinavyonunuliwa, ni wazi kuna makampuni hayatalipa kodi hadi mgodi utakapokwisha na madeni hayaishi kama *Williamson Diamond*.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda wa kati na mpango wa mwaka huu wa fedha, unazungumzia juu ya wachimbaji wadogo wadogo ambao inakisiwa kuwa ni kati ya 500,000 - 750,000, upo wasiwasi juu ya usahihi wa takwimu hizi, lakini tuchukulie kuwa ni sahihi, lakini hadi leo Serikali imeshindwa:

(i) Kuwapimia maeneo wachimbaji hawa wadogo wadogo, matokeo yake wanavamia migodi mikubwa hasa kwenye eneo la almasi na *Tanzanite*;

(ii) Kuwapatia vifaa ambavyo vingeweza kuwasaidia kuongeza mapato katika uchimbaji; na

(iii) Kuwapatia mikopo nafuu ili waweze kuwekeza badala yake wanafadhiliwa na wafanyabiashara wasiosajiliwa na kupewa bei ndogo ya mali zao.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda wa kati na wa mwaka haielezei kama wachimbaji wadogo wadogo watapatiwa mikopo. Je, kweli tunayo mipango thabiti ya kuondoa umaskini wa kipato?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, ili kuweza kuinua mapato yatokanayo na madini na kipato kwa wachimbaji wadogo wadogo, kazi ya kwanza ya Serikali iwe ni kwa kupima maeneo yao na maeneo hayo yathaminiwe ili wakipata mwekezaji waweze kuingia nao ubia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji huu ndio maana Kambi ya Upinzani inaamini na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla wanaona kuwa maneno ni matamu lakini vitendo ni vichache mno. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nishati ni nyenzo muhimu sana katika mipango ya kukuza uchumi wetu. Ukipitia hotuba zote za Bajeti, zinazungumzia nishati mbadala, lakini hakuna hata wakati mmoja amba tulipewa takwimu za kuonyesha nishati mbadala inapunguza kwa kiasi gani matumizi ya nishati ya mafuta na maji.

Mheshimiwa Spika, nishati ya upemo ambayo inapatikana vya kutosha, Karatu kuna upemo unakimbia kwa maili 5.5 kwa sekunde na Mkumbura unakimbia maili 4.9 kwa sekunde na Pemba Kaskazini, kama zingeendelezwa tungepunguza matumizi ya mafuta na maji. Umeme huu bei yake ni 0.05 *USD* kwa *kilowatt*. Hivyo, tungeweza kupunguza watu kuzaana sana na kupunguza umaskini kutokana na urahisi wa nishati hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, suala la mkaa wa mawe limeongelewa na kuandikwa kila siku, lakini Serikali bado inaona bora kulipa *IPTL* shilingi bilioni tatu kila mwezi kuliko kusimamia kidete Mradi wa Mchuchuma! Wakati umefika kwa Serikali kuwa wazi juu ya Mchuchuma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sababu moja ya kubadilisha Uongozi *TANESCO* ni kulifanya Shirika hilo litakapobinafsishwa liwe na bei nzuri, litoe huduma bora kwa umma na lijiendeshe kibiashara ili Serikali isiendelee kutoa ruzuku.

Mheshimiwa Spika hadi kufikia Mei, 2004, *TANESCO* imekwishapokea si chini ya Sh.60 billioni. Je, ile sera ya kukataa kutoa ruzuku kwa mashirika imekufa? Je, umeme umepungua bei? Je, *TANESCO* kwa kupewa ruzuku inaongeza mtaji wake?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba Serikali itupe mchakato wa ruzuku kwa *TANESCO* na madhumuni ya kupewa *management* ya kigeni, ambayo inaongeza bei ya umeme kila kukicha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweka taasisi na mipango juu ya kupambana na rushwa lakini bado wimbi la rushwa linakuwa na nguvu zaidi, hivyo kuhatarisha uchumi wetu kuwa endelevu na hata amani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa wazi ni pale tuliposhindwa kutimiza masharti ya kupata msaada (*grant*) kutoka Serikali ya Marekani ambapo ili upate *grant* hiyo ni lazima ufikie vigezo vya kutawala kwa haki na kupambana na rushwa, kuwekeza kwa wananchi wako kwa kuboresha elimu na afya na kujenga mazingira mazuri ya kuhamasisha sekta binafsi. Mpango huu unaitwa *Millenium Challenge Account*, Tanzania haikuteuliwa kupata msaada huu kutokana na kukithiri kwa rushwa. Nchi zilizoteuliwa ni *Cape Verde*, Ghana, Senegal na *Mozambique*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, ameeleza nia ya Serikali ya kupambana na rushwa, lakini nafikiri hatua ya kwanza Serikali ingechukua kufuta sheria ya takrima, kwani sheria hii inatoa mwanya na kuipunguza nguvu Sheria ya Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ni kupambana na rushwa ya kisiasa (*Political Corruption*), kuingia madarakani kwa kutumia fedha au vyombo vya dola. Kiongozi anaeingia madarakani kwa njaa hii hawezi kupambana na rushwa hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya tatu ni kuziwezesha Kamati za Bunge na Bunge lenyewe kuwa wazi katika utendaji wake kwa kuruhusu vyombo vya habari na wananchi wakati wote wa shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya nne ni kwa asasi ya rushwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, waripoti moja kwa moja Bungeni badala ya utaratibu wa sasa wa kupeleka taarifa zao kwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kuridhia mpango wa *African Peer Review Mechanism (APRM)* na kuvishirikisha vyama vya hiari katika kufuatilia rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua zilizoelezwa na Waziri zitasaidia sana kupambana na rushwa, hivyo Kambi ya Upinzani inashauri Serikali ichukue hatua hizi kama kweli imepania kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2003/2004, tuliishauri Serikali kuwa wakati umefika kwa Serikali kuachana na utaratibu wa mapato taslimu, kwa kuwa matumizi katika sekta nyingine yanapangwa kwa kutegemea kupatikana kwa fedha na siyo kwa kufuata Bajeti. Utaratibu huu unakwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama alivyokiri Waziri katika hotuba yake na naomba kumnunguu: “Kuhusu malengo ya

matumizi, mwelekeo ni kwamba, maeneo mengi ya matumizi ya maendeleo na ya kawaida hususan matumizi mengineyo (*OC*) hayatafikia malengo”.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfumuko wa bei unadhibitiwa na Serikali, inaweza isiendelee kukopa *IMF* na kwa kuwa sasa Serikali inachohitaji *IMF* ni muhuri tu kuliko mikopo, Kambi ya Upinzani inashauri ni vema Serikali ikaachana na mtindo wa mapato taslimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wote wameeleza nia ya Serikali kuanzisha Benki ya kilimo, lakini Wabunge hasa wa Kambi ya Upinzani hawaelewii ni kwa nini Serikali ianzishe benki mpya wakati benki za Serikali zipo kwa mfano, *NMB*, *TIB* na kadhalika? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuikumbusha Serikali kuwa, kwa kawaida thamani ya mikopo ya benki huwa ni kubwa kuliko thmani ya akiba, lakini Tanzania thamani ya akiba (*deposit*) ni kubwa kuliko thmani ya mikopo (*credit*). Mwaka 2003 ilikuwa mara mbili zaidi ya mikopo na ndio maana tukashikilia kuwa ni Serikali peke yake ndio inaweza kuwahudumia wakulima na ndio maana Serikali ilianzisha *CRDB* ili itoe mikopo Vijijini na *NMB* ilitegemewa itashughulikia maendeleo ya biashara ndogo ndogo. Leo tunabinafsisha halafu tuunde nyingine, utaratibu ambao utatuchelewesha sana na hatimaye itakuwa sawa na tulivyofanya, tuliiza *NBC*, halafu leo Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo inakodi jengo la *NBC* ambalo lilikuwa mali ya Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumezuka mtindo wa Serikali Kuu kufuta kodi bila majadiliano na maandalizi na wadau hasa Halmashauri za Miji na Wilaya, kwa vianzio mbalimbali vilivyoko chini ya mamlaka hizi. Kwa upande mmoja mtindo huu unapingana na dhana nzima ya kutoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kwani kuondoa vianzio kunafanya mamlaka hizo kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu na zimeondolewa na uwezo wa kuwa na mipango endelevu. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ili mipango hiyo iwe na manufaa, utaratibu wa kukusanya kodi zote ni kuzigawa kwa *formula* inayojulikana kwa Halmashauri zote. Kwa utaratibu huu Halmashauri hazitategemea huruma na hisani ya Serikali kuu na zitapata fedha zake kwa wakati na kwa uhakika. (*Makofî*)

Mheshimiwa spika, kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, fungu 50 - *Dividend, Private and Public Financial Enterprise Sub-Vote 080402, Bank of Tanzania*, mwaka 2002/2003 walilipa gawio Serikalini la shilingi bilioni 7.6, mwaka 2003/2004, shilingi bilioni 9.5 na 2004/2005 imekisiwa shilingi bilioni 2.8, kwa nini mgao wa faida uteremke kwa kasi kutoka shilingi bilioni 9 mpaka shilingi bilioni 2.8? Tunaomba maelezo. (*Makofî*)

Zanzibar ambao wana hisa 11.5% katika *BoT* wanapata kiasi gani kila mgao wa faida unapotokea? Mheshimiwa Waziri nafikiri anafahamu kuwa mgao huu ni tofauti na ule wa 4.5% unaotokana na msaada ambao *formula* kamili unangoja Tume ya pamoja ya fedha.

Mheshimiwa Spika, *Mining Royalties* tulitegemea ingelipanda badala ya kushuka, kwa mfano mwaka 2002/2003 royalties ilikuwa bilioni 14, ambapo *mines* ndizo zilikuwa zinaanza, 2003/2004 ikapungua hadi bilioni 4.5, makisio ya mwaka huu ni bilioni 9

Mheshimiwa Spika ni kwa nini madini mchango wake si tulivu wakati migodi ndiyo inazidi kuzalisha; je, nini matumaini ya Watanzania juu ya raslimali hii kama hata hiyo *royalty* ya 3% nayo haina ukuaji wa uhakika wa kupatikana? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi inaomba kuelewa hivi hayo mabadiliko ya tofauti yamesababishwa na nini?

Mheshimiwa Spika, *Mineral Sorting Fees* haikuwekwa mwaka 2003/2004 lakini mwaka huu wa 2004/2005 imewekwa, sio makisio bali zile fedha zilizohojiwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hivyo inaonyesha Serikali haina mapato yanayotokana na *sorting fees* za almasi, je, mwaka 2005/2006 si tofauti itakuwa kubwa baada ya Serikali kupata takwimu sahihi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waziri wa Fedha kupunguza kodi kwenye kilimo na biashara ndogo ndogo lakini bajeti ya kilimo imepungua kwa kulinganisha na bajeti ya mwaka 2003, yaani mwaka 2003 ilikuwa ni bilioni 31.5 na mwaka huu ni bilioni 29 labda kuna maelezo, Kambi inaomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, eneo la Uvubi wa samaki likiendelezwa kwa kuwekwa Viwanda vya Samaki kama vile vya Ziwa Viktoria, lishe itaongezeka na mapato yataongezeka. Inasikitisha kuiona *TAFICO* ilibinafsishwa kwa Kampuni isiyojua uvubi, matokeo yake inazidi kuliwa na bahari badala ya kuzalisha samaki.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo matatizo yetu, tunasubiri mpaka ianguke ndiyo tutoe maamuzi. Sera hata iwe nzuri vipi bila ya utekelezaji haina maana.

Mheshimiwa Spika, Ukimwi ni moja kati ya kikwazo kikubwa katika kupiga hatua ya kupunguza umaskini na kufikia lengo la *Millennium Development Goals*. Serikali kwa kuelewa kuwa kuna waathirika wasiopungua milioni mbili, imeweka malengo ya kuanza kupambana na Ukimwi kwa ujumla kwa kuchukua tahadhari ya kuenea kutokana na maambukizo na kuwatibu na kuwashughulikia waathirika. Malengo yote haya ni mazuri, hata hivyo, kumekuwa na kawaida ya kutumia pesa zilizotengwa na Serikali pamoja na wahisani kwa ajili ya kupambana na Ukimwi kwa kuendesha Semina na makongamano ambayo mengine ni hewa badala ya fedha hizo kuzipeleka kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, mfano ulio hai ni matumizi ya shilingi milioni 73, mwaka 2002/2003 ambayo hayakuwa na nyaraka, yaliyotumwa katika Wilaya za Arumeru, Kiteto, Hai, Lushoto, Mkuranga, Chunya, Mbarali, Rungwe, Muleba na Bukoba. Katika matumizi haya, Semina zimeitishwa lakini orodha ya walioshiriki haipatikani na wako waliopewa *order* ya ku-supply vitu au vifaa bila ya *quotation*, kwa mfano, uchapishaji vifaa vya IEC vya shilingi 1,400,000 Wilaya ya Kiteto. Aidha, hata pale zabuni

inapotolewa hubadilishwa na kupewa kampuni iliyoshindwa kwenye zabuni kwa mfano, uchapishaji wa vitabu 5,660,000 vya shilingi 1,167,376,000/=. Mchapaji Mkuu wa Serikali, ndiye aliyepewa zabuni, lakini aliyepewa kazi ya kuchapa ni *M/S Romejas Ltd.*, vitabu ambavyo havikuweza kutumika mashulenii kutokelezea na kutokekwa kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni (*Educational Material Approval Committee*).

Mheshimiwa Spika, ubadhirifu huu wanaujua wasimamizi. Kambi ya Upinzani hairidhiki na matumizi ya Fungu 92 na kwamba itahitaji maelezo ya kina na hasa juu ya hatua zinazochukuliwa kwa wavunjaji wa sheria za Ununuzi na Fedha (*Procurement Act* na *Finance Act*), ambapo uvunjaji unaashiria rushwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapatia dawa wagonjwa wa Ukimwi, lakini tatozaji la kupata lishe bado halijaandaliwa vizuri. Kambi ya Upinzani inashauri *TACAIDS* pamoja na asasi zinazosughulikia Ukimwi, zikusanye takwimu juu ya mahitaji ya lishe ya waathirika, badala ya kuendelea na semina na makongamano hewa tu. Aidha, waathirika wapitiwe na kupewa ushauri juu ya namna wanavyoweza kujihusisha katika jamii kujipatia kipato waaswe wasikate tamaa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inazipongeza asasi za dini kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuelimisha jamii juu ya janga la Ukimwi, tunawaomba waendelee kuwaasa raia wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na *National Payment System* na kutokelezea na tathmini iliyofanywa (*Stock-Taking Exercise*) ya nchi kuitia kwenye *Five Clearing Houses* za Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Zanzibar na Mbeya, ambapo kwa siku pesa zinafikia wastani wa shilingi bilioni 7.3 na mtu au kampuni ikishapeleka hundi, malipo au kuingizwa kwenye akaunti yake ni mpaka siku 5, hivyo wastani wa shilingi bilioni 36.4 zitakuwa kwenye mzunguko wa hizo *Clearing Houses* kwa mwezi mzima yaani siku 30, maana yake wastani kwa shilingi bilioni 218.0 ambazo ni kama 10% ya *GDP* yote kuwa hewani, kitu kinachohatarisha uchumi wa nchi kwa ujumla. Hii ni hatari kwani ni rahisi kwa kutumia teknolojia ya kisasa, kuzielekeza kiasi fulani kule kusikotakiwa. Mheshimiwa Waziri, Kambi ya Upinzani inataka maelezo, tahadhari gani imewekwa kwa usalama wa fedha zetu na Serikali, hasa baada ya kuwa na matukio makubwa ya wizi wa fedha kwa kutumia silaha na utaalamu wa *computer*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha, atufafanulie ni hatua gani walizochukua *TRA* katika kuondoa kero wanazozipata wafanyakaguliwa kutoka Zanzibar, wakati mizigo yao tayari imekwishakaguliwa na kulipiwa Zanzibar lakini bado wanapata usumbufu kana kwamba Tanzania si nchi moja wala *TRA* siyo moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Waziri aliahidi kuwa, Bandari ya Mkoani Pemba, itaingizwa katika orodha ya Bandari Kuu za Tanzania, je, nini kilichochelewesha utekelezaji wa uamuzi huu?

Hivi sasa wananchi wa Pemba wanalazimika bidhaa zao kuziteremshia Tanga au Unguja, hivyo gharama za usafirishaji huwa kubwa na bidhaa zao kuwa ghali na kutokana na hali hii ya umaskini ambao kwa kiasi kikubwa unasababishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kung'ang'ania kudhibiti uuzaji wa karafuu nje, kinyume na sera ya utandawazi, je, ile ahadi ya Serikali ya kuingiza bandari ya Mkoani Pemba katika orodha ya bandari kuu za Tanzania imekwamia wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu hotuba zote mbili. Kwanza kabisa, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote, kwa hotuba zao ambazo kwa kweli zimezingatia kwa ukamilifu kabisa utekelezaji wa Sera za CCM, pamoa na Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa watu wote waliochaguliwa kwa namna mbalimbali. Lakini nataka nitoe shukrani na pongezi maalum kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mbunge katika Bunge hili. Katika suala la Mheshimiwa Danhi Makanga, sidhani kama kuna sababu ya mtu kuzua mambo mengi sana ili uelewe kwa nini Mheshimiwa Danhi Makanga amechaguliwa. Mimi nasema ziko sababu mbili tu. Ya kwanza wananchi wana imani na CCM ndiyo maana wamemchagua mgombea wake. (*Makofi*)

Ya pili, wananchi wa Jimbo hilo wanatakiwa kupongezwa kwa sababu wameheshimu na kuzingatia maadili na demokrasia ya nchi kwa sababu walimchagua Mheshimiwa Danhi Makanga, akanyanyaswa na Chama kilichohusika, sasa wamekipa adhabu kwa kumrudisha Mbunge yule yule, kwa hiyo, huwezi kutafuta mchawi hapa, maana huyu ndiye aliyekuwa Mbunge wao. Sasa watu kurudisha Mbunge wao wamekosa nini? Kwa hiyo, natoa pongezi kwake na kwa wananchi, kwa busara waliyoitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nataka vilevile nitoe pongezi kwa Serikali. Yapo mambo ya kimsingi mawili ambayo ningependa kuyasema. La kwanza, unaposifu au kutokusifu, kwanza, huwezi kusifu kitu kisichokuwepo pia huwezi kulaumu kitu kisichokuwepo. Maendeleo haya tunayosema ni kwa sababu baadhi yetu tunayaona labda kwa yule ambaye haoni. Mimi natoka kijijiini nakwenda mjini kila mtu na hata watu wa nje wanasema kwamba, Tanzania imepiga hatua sana katika kukuza uchumi wake. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali yetu. (*Makofi*)

Vilevile nataka nirudie kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwamba, mpaka sasa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoheshimiwa sana duniani katika kutekeleza mambo yake. Labda niseme hapo hapo, ni hivi, watu wengi sana wanalia kuhusu rushwa hasa viongozi. Mimi napata tabu sana kuwaelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi siku zote huwa nasema wale wanaoona kwamba, Serikali hii imejaa wala rushwa, wanaleta majina ya wanaokula rushwa humu Bungeni

ndiyo mahali pa kuwadhibiti ama watumie utaratibu wa kuiambia Serikali kwa njia moja au nyingine. Mimi leo nataka nitoe mfano, mambo mangapi nimeambia Serikali na yametekelozwa vizuri. Yapo mambo mengi sana nimekuwa naandika kwa viongozi wa Serikali ninayoyajua na ninayoyaona na wanayatekeleza.

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kweli kuna vitendo vya rushwa, lakini hatuwezi kuvimaliza kwa kuimba au kwa kupiga kelele, lazima wanaohusika wote tusaidiane kudhibiti rushwa siyo kwa kusema tu. Maana yake unaweza kusema kwa kujifurahisha tu, lakini tunafanya nini kwa vitendo hasa sisi tulio na madaraka katika kuondoa rushwa.

Sasa baada ya hayo, ningependa kusema pia jambo la jumla. Hili jambo mimi nafikiri kwanza nampongeza Mwenyekiti wa Kamati yetu amewasilisha taarifa vizuri sana na kwa kweli haya ni maoni ya Kamati. Mambo ya jumla ambayo ningependa kuyasema. La kwanza, mimi nafikiri ingekuwa vizuri kama tunganza kutazama tulikotoka, tulipo na tunapokwenda, kwa sababu zamani tuliwhi kuwa na Tume na kuna wakati ambapo Bunge hili katika Muundo lilitamka kuwa ni Tume ya Mipango. Kwa sababu ninavyoona mimi hata katika mazungumzo tukikutana na hata ukizingatia maelezo ya Waziri wa Mipango, utaona kwamba kwa kweli mimi nilikuwa nafuatilia na kusikiliza hotuba alieleza sana kuhusu mambo ya Wizara zingine, hakueleza maelekezo ya mipango kuhusu Wizara hizo. Mipango kwa maana ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, *vision* yetu ni nini?

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, tungetazama upya utaratibu wetu wa upangaji wa mipango. Kwa sababu kwa hivi sasa inavyoonekana Wizara ya Mipango nadhani wanafanya kazi kubwa zaidi ya mambo ya *Privatization* kuliko *focus*, kuelekeza nchi tunakokwenda. Huo ndiyo ukweli na lazima tutoke hapo. Kama tukibakia hapa hatuwezi kwenda, *vision* maana yake ni mipango, sasa mimi sioni *vision* katika jambo hili. Naona mipango ya mwaka wa fedha unaohusika tu. (*Makofî*)

Suala la madini mimi nina maoni kwa Serikali na nina hakika hili ni jambo linalohitaji muda. Lakini kabla sijasema hilo, nataka niipongeze Serikali kwa sababu haya madini tunayozungumzia leo hayakuwepo yalikuwa ardhini, sasa yameanza kuchimbwa, kwa hiyo, lazima tuipongeze Serikali kwa kazi nzuri hii kwamba katika kipindi hiki Sekta hii imeongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali. Madini hatuwezi kuyaacha yakaendelea kubaki ardhini, sasa ufanisi ni mkubwa na kwa taarifa nilizonazo na kwa kuwa mimi mwenyewe angalau katika sekta hii nahangaika kidogo, ingawa wanasema kwa sasa Tanzania ni ya nne kwa uchimbaji wa madini, mimi ninavyofikiri tukikazana hivi hivi tunavyokwenda, Tanzania inaweza kuja hata kuwa ya pili kwa uchimbaji wa madini kwa jumla. Kwa mfano, tukichukulia dhahabu peke yake, migodi ambayo imekwishaanza na ile ambayo mimi nadhani iko kwenye maendeleo, itakuwa mingi sana. (*Makofî*)

Kwa hiyo, hapa kwa sababu jambo hili lipo, ushauri wangu tu nilikuwa nataka kuishauri Serikali tuanze sasa sisi Wabunge kufikiri na Serikali ianzu kufikiri ili tuseme hivi mapato haya yanayotokana na madini yanaongeza vipi uwezo wa nchi kimaendeleo.

Kwa mfano, mimi nimepata nafasi ya kwenda Malaysia na mara mbili zote nilipata nafasi ya kukutana na Waziri Mkuu wa Malaysia, wao wana mafuta na tulipokuwa tukizungumza, akasema Mheshimiwa Mzindakaya, nchi yangu ina mafuta lakini fedha zote zinazopatikana nazitumia kujenga barabara, kuendeleza kilimo kwa sababu kilimo ni *renewable resources*, madini yatakwisha, kwa hiyo, nataka siku madini yatakapokwisha nchi yangu iwe imekwishapiga hatua kwa kuziendeleza sekta ambazo zitaendelea kuwepo. Sasa sekta hii ya madini haiwezi kuendelea kuwepo, hii migodi yote kila anayefanya *feasibility study*, anajua kabisa kwamba, kwenye mgodi wake dhahabu itachimbwa kwa muda gani, sasa kwa sababu itakwisha, je, itakapokwisha tutasema tulifanyi nini mapato ya dhahabu? (*Makofi*)

Wenzetu Waarabu Mungu amewapa mafuta na ukifika Uarabuni *infrastructure* kule kwenye majanga ni kubwa sana, kuna umeme na barabara, sasa sisi hatuna haja ya kulia kwa kukosa mafuta, tumshukuru Mungu kwa kuwa na dhahabu. Tunayo madini, sasa swalii na hoja yangu hapa ni kwamba, tujiandae namna ya kutumia mapato ya madini haya kuendeleza sekta hizi ambazo ni *renewable* kama kilimo. Kwa mfano, leo barabara tumeanza kuwa na mafanikio. Leo barabara zinazotengenezwa kwa fedha zetu wenyewe zinatokana na fedha za mafuta ambayo tuna *import*, tunatoza kodi. Sasa tunafanya nini kwa dhahabu yetu wenyewe, maana hizi tunazotoza ili tutengeneze barabara zetu ni mafuta kutoka Uarabuni, sasa tunapata nini kwa dhahabu yetu wenyewe ili tutengeneze barabara zetu, hiyo ndiyo hoja yangu? (*Makofi*)

Vilevile nataka niunganishe na hili kama tunavyoona kwenye takwimu inaonekana akiba ya fedha zetu za kigeni ni nzuri, kwa sababu mimi ninavyojua hapa kilimo chetu kinaendelea kudorora kwa sababu mbili. Kwanza, hatuagizi zana za kutosha za kuendeleza kilimo, sisi bado tunaagiza jembe la mkono tu. Ukienda Uganda na Kenya na katika nchi nyingine za majirani zetu, utaona uingizaji nchini wa zana za kilimo kwa maana ya matrekta na nyingine ni kubwa mno kuliko sisi. Sasa sisi bado tunaagiza majembe ya mkono, hata kiwanda cha kutengeneza plau hatuna, hata kilichopo kimekuwa na hakuna anayezungumza kukifufua. Sasa unawezaje kuendeleza kilimo kwa jembe la mkono? (*Makofi*)

Ukianza kuzungumza kilimo unaweza ukaanza na plau kisha trekta. Mimi nimefika India, India ni nchi kubwa, India ina *population* kubwa kuliko sisi, wako watu zaidi ya bilioni lakini India wanajitosheleza kwa chakula. Kwa sababu wanahangaika wanatengeneza matrekta hata kama badala ya kwenda mbele likirudi nyuma, kesho litakwenda mbele. Sisi kila kitu ni kuagiza tu, hatufikirii kutengeneza zana za kilimo, tutaendeleaje? Sasa nasema kama *reserve* yetu ni nzuri na sasa tunapata fedha kutokana na madini, tuenze kufikiria sekta hizi. Pia kwa mfano, matumizi ya fedha hizi za akiba, mimi nataka kujua, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kiasi gani kinatumika kwa fedha zetu za kigeni ku-*import capital goods* na kiasi gani kinaingiza *consumer goods* zikiwemo odorono? Maana tunaweza kuwa na fedha za kigeni kumbe zinaleta vipodozi, bazoka sasa hatuwezi kutumia fedha kwa bazoka na pipi. Ukienda Dar es Salaam maduka yanayofanya biashara kubwa sana ni ya vipodozi pamoja na kwamba ni fedha za kigeni lakini huoni matrekta, huoni plau na hakuna mbolea katika nchi hii. Sasa tunawezaje kutumia fedha hizi kuagiza *lipstick* badala ya kuagiza mbolea. Ninapenda

kuona wenye poda lakini tufikirie poda inapatikana vipi, maana haiwezi kuja poda bila kuzalisha mali? Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema hilo. (*Kicheko*)

Vilevile katika hilo, nataka niseme kwa dhati ya moyo wangu, kilimo bado kinadorora, Wizara ya Kilimo hawajafanya wajibu wao, sioni haya kwa sababu nasema kwa dhati ya moyo wangu, Wizara ya Kilimo wako likizo, miaka 9 ya awamu yetu ya tatu wako likizo ya uhakika kabisa wala hakuna sababu ya kuona haya. Mimi natoka Rukwa ambako tunalima, mimi mwenyewe si mkulima wa uhakika, ukizungumza kilimo najua hasa tena kitaalam siyo kubabaisha. Kama mwaka huu tungefanya mashindano ya Kilimo katika Mkoa Rukwa, mimi ningekuwa wa kwanza kwa utaalamu. Sasa kilimo *extension* hakuna, mbolea Waheshimiwa Wabunge mtashangaa mwaka 2003 tuliambiwa hapa habari ya mbolea, ile mbolea tulioambiwa Serikali imetoa fedha na imeagizwa haikuagizwa walikwenda kununua kwa mfanyabiashara, ambaye alinunua mbolea ya *tender*, yuko mfanyabiashara mmoja alikuwa anapendelewa kupewa mbolea ya *tender*, huko ndiko wamekwenda kununua mbolea, hawakuagiza mbolea kutoka nje. Naomba wathibitishe kama nimekosea. Hivi Mheshimiwa Rais amelihutubia Taifa kwamba kutakuwa na tani 24,000 za mbolea mwaka huu, nataka Waziri wa Fedha asimame hapa atueleze mbolea iko melini, iko bandari au iko wapi? Maana mimi nina habari kwamba hata kufungua *LC* imekuwa tatizo, kwa hiyo ndiyo nataka niseme hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kusema, mwaka 2003 kulikuwa na upungufu wa chakula, Serikali ikatenga fedha, Serikali ina chombo kinaitwa *SGR*, sasa badala ya kutumia *SGR* wakatangaza *tender* tena ya kuandikia watu binafsi waombe kuingiza mahindi ya njaa, yale mahindi ya njaa yameigharimu Serikali ukilinganisha viwango vile vilivyotumika vya *tender*, Serikali imepata hasara ya zaidi ya shilingi bilioni moja. Mimi nimefanya *study* nitawapeni Serikali mwone juu ya *tender* hii, nitakupeni vyote ili mjue kuna nini katika *tender* hii.

Pili, mchele uliosamehewa kodi, kwanza nataka kuiomba Serikali tukubaliane muache kuagiza mchele na kuusamehe kodi, mchele haujapata kuwa kwenye *item* ya kusamehe kodi, mchele siyo chakula cha njaa ni *luxury*, watu wangapi wa nchi hii mliowasamehe kodi? Kwanza, msamaha wa kodi ya mchele umeipotezea Serikali shilingi bilioni 1.3 na mchele ulisamehewa wakati meli ya mchele iko bandari. Kwa sababu muda uliotolewa kuagiza mchele ulikuwa miezi minne, sasa kufungua *LC*, uagize mchele kutoka Japan miezi mitatu haitoshi. Mimi ninayo tarehe ya msamaha na tarehe ya meli kuwa pale pale bandarini. Sasa tunafanya mchezo gani na aliyesamehewa alikuwa anajua kama atasamehewa na kwa sababu ulipofika muda tena ukaongezwa huyo alishajua kwamba kutakuwa na muda wa kuongeza, ikaongezwa miezi minne, huyo huyo ndiyo akaagiza tena mchele. Kwa hiyo, mchele wote uliosamehewa kodi wameagiza wafanyabiashara wawili tu.

Tatu, mahindi kama kuna njaa tangazeni wafanyabiashara wote, kila mtu alete mahindi tushindane kwa nini Serikali mtumie mtu na *SGR* ipo kuagiza mahindi. Nataka niiombe Serikali ikiwa itakuja kuthubutu tena kusamehe kodi, mimi nitaleta hoja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge wataipinga Serikali kwa kusamehe kodi kwenye mchele, hatuwezi kuruhusu mchele kusamehewa kodi. Kwanza, mchele ulisamehewa

kodi Wabunge wote ni mashahidi, mchele ulipanda bei au uliadimika. Kosa lililofanyika ulikuwepo mchele wa Japan uliotozwa kodi, ule uliotozwa kodi walipoingiza usiotozwa kodi hao wakashindwa kuuza mchele, wakafanya *holding*, kwa hiyo, soko likakosa mchele. Sasa waliosababisha ni wale walioagiza mchele usamehewe kodi. Kwa hiyo, nataka jambo hili tuliache tusilirudie tena, si jambo zuri, sisi tutakuja kuibana Serikali hapa, tunaweza tukafanya kama mafuta ya kupikia kwamba nendeni mkawadai hao mliowasamehe wasilipe kodi. Hakuna *justification* ya kuwasamehe hao kulipa kodi, *they made money*, nani anaweza ku-*justify* kwamba, bei ya mchele kwa mlaji ilishuka baada ya kusamehe kodi, nani anaweza kueleza hapa, hebu tuelezeni kama yapo maelezo hayo. Hakuna maelezo hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nilitaka niseme hayo. La mwisho nataka nirudie tena kwamba, sisi viongozi tuna wajibu mkubwa na utoaji wa takwimu lazima tuuangalie. Juzi hapa Mheshimiwa Waziri mmoja alisema kilimo kimekua kwa asilimia 5, Benki Kuu wanasema asilimia 4. Kwa hiyo, takwimu zinazoelezwa hapa zinangongana pia.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. NAZIR M. KARAMAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja mbili zilizoko mbele yetu. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, waliowasilisha hoja hizi pamoja na wasaidizi wao wote. Lakini kwanza, kama ilivyokwishakuwa desturi, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bariadi katika ushindani uliokuwa mkali, lakini ameonekana kwamba ni mkali zaidi. (*Makofi*)

Baada ya hizo pongezi napenda kuchangia hoja kwa kuipongeza Serikali kutoa unafuu wa kodi kwa wakulima wa Tanzania, nikisema wakulima ina maana kwa ujumla wake wakiwemo wavuvi na wafugaji. (*Makofi*)

Vilevile napongeza juhudhi ya kuhamasisha kutoka katika kilimo cha asili kuingia katika kilimo cha kisasa, nikiwa na maana kwamba, hizi kodi zote zilizosamehewa kama mkulima hatunzi mahesabu vizuri atashindwa kunufaika na misamaha hiyo. Kwa hali hii ningependekeza kwamba, kwa wote wahusika katika sekta mbalimbali, kuanza kuwaelimisha wananchi kwa ujumla hasa wakulima wadogo wadogo, namna ya kutunza mahesabu yao. Kwa sababu sera zinaweza kuwa nzuri lakini kama hujawaandaa wale ambao sera zimeelekezwa kwao wanaweza kushindwa kutumia fursa hii. Kwa hiyo, natoa rai kwamba, katika sekta mbalimbali tuanze kuwaelimisha wakulima na wafugaji wadogo wadogo na wavuvi namna gani wanaweza kutumia fursa hii ya msamaha wa kodi ili wanufaike nayo.

Vilevile napenda kuipongeza Serikali kwa kuondoa rasimu katika upatikanaji wa leseni hasa wafanyabiashara wadogo wadogo, ingawa sana sana watu wa mjini watasema kwamba, inawanufaisha wamachinga, nina hakika watakaonufaika sana ni wananchi wa vijijini kwa sababu maduka mengi ambayo yapo vijijini ni maduka madogo madogo na nafikiri kwamba, watanufaika na hilo kwa hiyo, naipongeza Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili ni la ujumla kwa wawekezaji wakubwa wakubwa katika sekta ambazo ni maalum, naipongeza Serikali kwamba, wameondoa utaratibu wa *Multiple* leseni, mtu anatafuta leseni kama 10 na huku anafanya biashara moja. Hiki ni kitu ambacho kilikuwa kinalalamikiwa sana na wawekezaji na nafikiri Serikali imekiona na kuondoa leseni kuwa kama chanzo cha mapato ili iwe tu ni namna ya kuorodhesha watu na kuwa katika utaratibu mzuri wa kujulikana Serikalini ilimradi anafanya shughuli halali.

Sasa baada ya hizo pongezi nina maoni ama mapendekezo kwa sehemu zifuatazo: Pamekuwepo hoja ya wawekezaji mbalimbali kutokutumia mabenki yetu ama masoko yetu ya mitaji nchini. Inabidi tuangalie sababu gani zimesababisha hali hii ili kuweza kuzirekebisha. Kwenye mabenki tunajua kuna fedha nyingi ambazo badala ya kuziweka kwenye vitega uchumi kuwakopesha ambao wanazalisha wanaziweka kwenye amana na tunajua kwamba, tofauti kati ya riba ya kukopa na kuweka bado ni kubwa, lakini inatokana na nini? Inatokana labda na sheria zetu ambazo tunazo wakati mwingine zinamlinda sana mkopaji na kuweza kuzitumia kukwepa kwepa na kufanya nchi yetu iwe na *risk rating* kubwa katika kukopesha. Hali hii ikiendelea bila kurekebisha sheria hizo, itafanya mabenki yawe yanatuwekea riba zilizo kubwa ama yawe yanasisita kuwakopesha watu mahali ambapo miradi ipo.

Halafu pili, inabidi kuangalia hata sheria yetu katika soko la mitaji, kuna miradi mizuri mizuri tu ambayo ina uhakika wa mapato, ambayo siyo lazima ingojee utekelezaji na kungoja miaka mitatu ya faida. Kwa mfano, Mradi wa Songo Songo Gesi hakukuwa na sababu ya kwenda kutafuta fedha nje kama wangeweza kwenda kwenye soko la mitaji wakapata hizo fedha, kwa sababu huo mradi ulikuwa unajulikana kuwa mapato yake mengi sana yatakuwa ya uhakika na yanatoka humu nchini. Lakini kwa sababu ya sheria zetu ambazo haziruhusu hivyo, inabidi waende kutafuta fedha nje ambapo wangeweza kuzitoa hapa nchini na kwa wananchi wa kawaida wakafaidika na miradi hiyo.

La pili, nzungumzie juu ya wakulima wadogo wadogo kwa ujumla wake kama nilivyokwishaeleza. Katika ukurasa wa 30 kipengele cha 33 kinasema kuwa: "Serikali itadhamini wakulima wadogo wadogo kukopa kutoka Mabenki ya Kibiashara". Nafikiri kwa wakulima wadogo wadogo haitawasaidia hii. Serikali afadhali iendelee na dhamira yake ya kuunda haraka haraka Benki ya Kilimo ama kuwekeza kwa Mabenki ya Kilimo ambayo yapo tayari kwa sababu mkulima wetu huyu ambaye tunataka kumtoa katika kilimo cha asilia kumwingiza katika kilimo cha kisasa hataweza kumudu hiyo riba ambayo inatozwa na Mabenki ya Kibiashara. (*Makofii*)

La tatu, kwa haraka haraka nachangia katika mgao wa fedha ukurasa 37 kipengele cha 5 ambacho kinaendeleza kilimo katika Wilaya kwa utaratibu wa zao moja la chakula na moja la biashara. Mpango huu ultangazwa katika Bajeti ya mwaka jana na tuliupokea na kumshangilia. Lakini sijui katika Wilaya yangu sikuona mkakati wowote wa Wizara husika katika kutekeleza azma hii. Kama hiyo fedha kweli ililetwa Wilaya ya Bukoba Vijiji basi ningependa kujuu ilitumikaje. Kwa kweli kuwekeza kwenye mpango wa

zao la chakula na zao la biashara lilikuwa zuri sana na tulilipongeza sana. Lakini inaonekana kwamba labda lilitangazwa bila sekta husika zote kuwa na mkakati maalum namna ya kulitekeleza. Mwaka huu limetangazwa tena kwa hiyo tungependa kujua haswa mkakati uliowekwa ili litekelezwe lisiwe kama mwaka jana.

La nne, ningependa kuchangia juu ya sekta ya mafuta. Naipongeza Serikali kwa mbinu walizoziweka kwa kubana ukwepaji wa kodi ya mafuta na kweli inaonyesha kwamba sekta hii imeweza kuchangia maradufu katika pato la Taifa. Lakini kama ilivyoonekana ili umkamue ng'ombe maziwa lazima umlishe vizuri, ukimkamua sana bila ya kumlisha vizuri hutapata maziwa uliyokuwa unatarajwa.

Kwa hiyo, matatizo ya sekta hii vile vile Serikali inabidi kuyaangalia ili baadaye hii faida iliyopatikana tusije tukaipoteza. Tumewahi kukutana na Makampuni ya Mafuta yanasema kwamba ili kuagiza shehena na mafuta inachukua siku 45. Lakini wamepewa siku 30 kulipa kiasi kwamba inawawia vigumu sio vigumu tu inabidi kutumia fedha nyingi na kukopa fedha nyingi ili kumudu sera hii iliyowekwa. Sasa kama tunaweza kuwaongezea siku toka 30 kufika 60 na kama haitachangia katika ukwepaji wa kodi labda itasaidia kuwaongezea unafuu na pengine hata kuleta unafuu wa bei. Kwa hili sioni sababu gani ya kuendelea kuwaumiza kutowapa unafuu. Kama ilivyoeleza kwenye kitabu kwamba kuna sekta iliyopewa unafuu na badala yake ikazalisha maradufu na tukapata faida yake.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tano na wa mwisho labda ni kupongeza Serikali kwa kuwarudisha wastaifu waliopokea mafao yao kwa mkupuo katika daftari la pensheni. Kwa niaba ya wastaifu wa Bukoba Vijijini, napenda kumpongeza Waziri pamoja na Serikali nzima kwa ujumla kwa kuweza kusikia kilio cha hawa wastaifu ambao wengi ni wazee kuwarudisha katika pensheni hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na ningeomba awali kabisa kutoa rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba walioupatu naomba Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho ya baba yao. (*Amin*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kumpongeza Ndugu Danhi Makanga, kwa kurejea Bungeni kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Mramba kwa hotuba zao. Nampongeza sana Mheshimiwa Mramba na Watendaji wake wote Wizara ya Fedha kwa kuandaa Bajeti yenye kuendeleza mafanikio ya mageuzi ya uchumi ambayo tumeishaanza kuendelea nayo hadi hivi sasa. (*Makofî*)

Nashukuru sana kwa Waziri kuelekeza haya mageuzi kwenye sekta ya kilimo pamoja na viwanda na biashara. Ni kweli kabisa siku za huko nyuma hizi sehemu mbili zilikuwa hazijapewa msukumo unaostahili tukitambua kabisa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa nchi na kuwa Viwanda na Biashara ni sekta kiongozi. Nikikumbuka tu na

kuangalia kwenye kitabu cha 4 mwaka jana Wizara ya Kilimo kwenye sekta ya kuendeleza kilimo ilipangiwa na Serikali Shs. 50 milioni ni kipato kidogo sana. Lakini mwaka huu fedha hizo amevishwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwenye kuongeza tija kwenye Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini inaelekea kabisa Mheshimiwa Waziri kwa makini ameelekeza mabadiliko haya kwenye kuangalia *micro economics policies objectives* za Serikali pamoja na *monetary policy statement* ya Benki Kuu na hivyo kuhakikisha kuwa tunaelekeza kuwa maendeleo yetu kwenye sehemu ambazo zitaweza kutukwamua kiuchumi. Kuna mapungufu ambayo yametokea kwenye taratibu hizo zote za kukuza uchumi wetu. Kama utakumbuka nilivyosema awali kwenye sekta ya kilimo mwaka jana ilipewa Shs. 50 milioni tu. Mwaka huu kwenye mpango mzima wa maendeleo kuna Shs. bilioni 29.1 zilizotengwa lakini ni kiasi kidogo sana kimetoka kwenye mapato ya ndani. Tumetenga bilioni 8.7 kwa hiyo ni kuelekeza tena utegemezi wa Bajeti yetu kwa huko nje. Lakini naamini kwa kuwa Serikali sasa imetambua kuendeleza kilimo itachukua mikakati inayofanana kabisa na ile tuliyoiendeleza kwenye upande wa barabara kuchangia kila mwezi kipato cha mapato yetu ya ndani ili kuinua sekta hiyo.

Kwenye 29 bilioni kuchangia bilioni 8.7 ni kuendelea kuwa tegemezi. Isipokuwa kinachofurahisha tu kwenye Bajeti hiyo inaonyesha kwa mwaka huu angalau misaada kutoka nje imepungua chini ya asilimia 45 kwenye msaada kutoka kwenye *High Indented Poor Countries* misaada kutoka nje ambayo tulichangia asilimia 45 ya matumizi yetu yote mwaka jana lakini mwaka huu inaelekea kuwa tumefanya kazi nzuri na kiwango hicho kimepungua kufika 40.84 hiyo ni hali nzuri na naamini kabisa kwa mikakati ya kuweza kuwekeza ndani basi tungeweza tukapunguza tegemezi hizo ili itakapofika mwaka 2025 kama tulivyojipangia katika mkakati wa Taifa tuweze kuwa na uchumi wa kuijendeleza wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tuna uchumi sasa hivi nikichukua mfano ni kama baisedeli. Tuna gurudumu, mnyororo, sahani na *pedal*. Wizara ya Fedha kama *pedal*, mnyonyoro ikiwa kama Benki na Wizara ya Mipango kama sahani ni uchumi ambao sasa umeshajishika, lakini naona tuna kila sababu ya kuhakikisha kuwa ifike muda hayo maendeleo yatakuja yenyewe bila kutaka msukumo zaidi wa ubinadamu. Tuna nyonga lakini ifike muda tupate *auto pilot* iwe kama ndege uchumi ujiendeshe wenyewe. Ndiyo sababu naona kwenye upande wa Wizara ya Viwanda pato tuliloingiza mwaka huu karibuni Shilingi 998,300,000/=.

Lakini kujitengea Shilingi 50,000,000/= ni kutowezesha sekta hiyo kuendelea. Kama sekta kiongozi ninaamini kabisa tunaweza kuiendeleza hasa kabisa tukiangalia suala la uchumi umechangiwa zaidi ya asilimia 8.6 na Wizara hiyo. Kama nilivyosema tufanye mikakati ya makusudi kabisa kama tulivyofanya upande wa kilimo mwaka huu kwa kuipa bilioni 4 basi na Wizara hii ya Viwanda na Biashara iongezewe pato ili tuweze kusukuma mauzo yetu nje na hivyo kuweza kuwa na Bajeti ambayo itawenza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hayo naomba nirudi tena kwenye taratibu za ukusanyaji wa kodi. Kwenye ukurasa wa 49 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameonyesha taratibu za ukusanyaji wa kodi kwa kuwaingiza watu ambao hawako kwenye sekta rasmi walipaji kodi wadogo wadogo. Taratibu inaonyesha kuwa kwa mtindo ule ulioonyeshwa hawa walipa kodi ambao hawatakuwa na kumbukumbu watalipa kodi zaidi kuliko waliokuwa na kumbukumbu. Hiyo kidogo nadhani inakiuka taratibu za kuweka hesabu sahihi, taratibu na kanuni za fedha. Itatusaidia kwa mpito kuweza kuwapata walipa kodi wengi zaidi ambao watatuongezea pato lakini tutakuwa na walipa kodi ambao hawathamini taratibu za kuweka kumbukumbu na kuweza kuheshimu taratibu za kifedha. Kama nilivyosema kwa mpito ni sahihi lakini ni lazima hapo baadaye tuweke taratibu ambayo itampa moyo pia yule ambaye anaweka kumbukumbu sahihi aweze kuchangia pato bila kuwa na manung'unico. Tutakuwa na uitiri wa walipa kodi ambao pia inaweza ikasababisha mianya ya ubadhirifu sio kwa mlipa kodi tu bali hata mtoza kodi kwa sababu ni kitu ambacho kitategemea uamuzi ambao sio wa kisayansi

Mheshimiwa Spika, kwenye taratibu za kilimo imefurahisha kuwa Waziri ameamua pia kuwapunguzia wale wenzetu ambao wataingia kwenye sekta ya kilimo gharama ya asilimia mia moja kwa ajili ya kusafisha shamba. Taratibu iliyokuwa kwenye sheria ya zamani ya mwaka 1973 sheria na. 33 ya *Income Tax* ilitoa unafuu wa asilimia moja ya tano ya gharama za uendeshaji kusafisha shamba na uwekezaji wa miundombinu kwa maana hiyo ni kuwa taratibu ilitambua kabisa kilimo sio kama biashara nyingine ambayo inaweza ikatoa tu tija baada ya muda mfupi, inahitaji tu angalau miaka mitano. Kwa hivyo zaidi ya yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Waziri kwenye kuleta nafuu kwenye sekta hiyo ningeshauri pia iangalie muda wa kupewa sekta ya kilimo kitu kama *Tax holiday* iweze kuwasaidia wawekezaji kujiandaa kwenye uzalishaji na hatimaye waweze kuwa wanalipa kodi zao stahiki. Kama nilivyosema mwanzoni kwenye hiyo *preventive assessment* inaonyesha kwenye viwango vya Shilingi 3 milioni yule mwenye kuweka kumbukumbu atalipwa Sh. 36,000 asiyekuwa na kumbukumbu atalipwa shilingi 35,000. Yule ambaye atakuwa ana mauzo yanayofikia shilingi 7 milioni yeye atalipa Sh. 95,000 na asiyeweka pia atalipa Sh. 95,000. Yule ambaye atakayekuwa na *turn over* ya Shilingi 20 milioni mwenye kumbukumbu atalipa Sh. 591,000. Asiyekuwa na kumbukumbu atalipa Sh. 589,000. Kwa maana hiyo kutakuwa tunakaribisha watu ambao hawataweka hesabu na hii ni hatari kwa Serikali kupoteza mapato sawa kabisa na usemi usemao kuwa mali bila daftari hupotea bila habari. (*Makofi*)

Naafiki hatua hii ya mpito kwa kuwawezesha hawa wenzetu ambao hawako kwenye sekta rasmi waingie ili waweze katuongezea kipato hili ni sawa lakini kiwe kipato chenye mfumo uliokamilika na usiwe mfumo wa kubahatisha. Kwenye *Monetary Policy Statement* iliyotolewa na Benki Kuu imezungumzia waziwazi kuwa uwezekano wa mafanikio kwenye Bajeti yetu itategemea sana uzalishaji au uvunaji wa mazao na hatimaye hali nzuri ya hewa. Sasa hapo inanikumbusha balaa la njaa tulilolipata mwaka huu. Miezi mitano toka mwezi wa Novemba, 2003 mpaka mwezi Machi, 2004, hali yetu ya chakula imekuwa ni mbaya. Sababu kubwa ni kwa sababu tulikuwa hatuna chakula kwenye ghalaa zetu. Ni muhimu kwa sababu sasa tunaamua

kutambaa umuhimu wa kuingia kwenye sekta ya kilimo kuipa kipaumbele basi Serikali ijenge tabia ya kuweka akiba ya chakula angalau kwa wakati huo wa msimu na kuuza hiyo akiba hapo baadaye. Bila ya kuwa na chakula hii ni hatari kubwa kwa nchi hasa wakati wa majanga.

Naamini kabisa kwa taratibu zilizotolewa na Waziri wa Mipango na malengo yaliyotolewa ya kifedha na Benki Kuu pamoja na kazi iliyofanyika ya kutekeleza azma hiyo na Wizara ya Fedha malengo yote tuliojipangia ya kukuza uchumi wetu wa kupunguza mfumko wa bei pia kuchangia pato la ndani utafanikiwa. Isipokuwa kuna kitu kimoja tu lazima niseme kabla sijamalizia ni kuwa pamoja na mafanikio ya mwelekeo wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 inaelekea Bajeti yetu imetoa mapato kidogo sana kwenye huduma za jamii na ulinzi.

Lakini sababu hilo kidogo linalelewaka kwa kuzingatia sekta ya kiuchumi na uzalishaji, Matumizi ya pato la Taifa kwenye sekta hizi mbili limeongezeka. Naamini kabisa hapo baadaye tukishaweza kuchangia vya kutosha basi huduma hizi za jamii na ulinzi na sehemu zile nyeti zote zitapewa mafungu mwafaka.

Baada ya kusema hayo naomba niunge mkono mipango yote ya Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Ofisi ya Rais na mwelekeo wa Benki Kuu, kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. EDWARD N. NDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha. Kabla ya kufanya hivyo naomba nitoe pole zangu kwa msiba uliompata Mheshimiwa Waziri huyo pamoja na Mheshimiwa Aisha Kigoda kwa kufiwa na mpenzi baba yake. Nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kuchaguliwa kwake kujiunga katika Bunge hili. Nampongeza sana. Baada ya pongezi hizo nirejee kwenye hotuba na kwa kuwa nimezipitia hotuba zote mbili, hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Waziri wa Nchi, Mipango na Ubinafsishaji napenda kabisa kwa dhati niwapongeze Mawaziri hao pamoja na wataalamu wao kwa kuandaa hotuba ambazo kwa kina na upeo nilioupitia baada ya kuzisoma napenda kabisa niseme naziunga mkono asilimia mia. Mchango wangu nitauselekeza katika hotuba ya Waziri wa Nchi. Katika kufanya hivyo nitajielekeza katika kifungu au sehemu ya hotuba hiyo inayozungumzia ukuaji na maendeleo ya sekta muhimu sekta za uzalishaji. Hapa nitajielekeza kwenye sekta ya kilimo. Katika kifungu namba 36 tumefahamishwa katika hotuba hiyo kwamba sekta ya kilimo ilishuka kutoka asilimia 5 mwaka 2002 hadi asilimia 4. Sekta ndogo ya mazao nayo pia ukuaji wake ukashuka kutoka asilimia 5.3 hadi asilimia 3.6.

Mwelekeo huu sio mzuri na sababu ambayo imedhihirika katika hotuba hii ni kukosekana kwa mvua. Hotuba pia imetuonyesha kwamba katika kifungu namba 37 kwamba Serikali ilichukua hatua za haraka ili kunusuru hali ya uchumi wa Taifa letu katika kipindi cha mwaka unaokuja. Sasa hapa nina tatizo kidogo. Zipo hatua sita zilizoonyeshwa kuchukuliwa kwa ajili ya kunusuri Taifa dhidi ya ukosefu wa mvua. Hatua zote sita ni moja tu ambayo naona ni ya haraka ambayo inaweza kukabiliana na

ukosefu wa mvua nayo ile ya kukamilisha maandalizi ya sehemu ya kwanza ya mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji. Kwa sababu nyingine ambazo zimeorodheshwa pale kwa mfano kutoa Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kufidia gharama ya usafirishaji wa mbolea, kufanya ukarabati mkubwa wa vituo 17 vya utafiti, kuongeza uwezo wa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na kununua na kusafirisha matreketa 170, hizo zote tano jinsi zinavyoweza kuleta utatuvi wa tatizo la ukosefu wa maji. Kwa hiyo, hatua pekee ambayo ninaiona ni ile ya kuelekeza katika maeneo yale ambayo yana uwezekano wa kumwagilia maji mashamba. Hata katika hiyo ukiangalia kiasi cha hekta ambazo nchi hii inaweza kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji hekta milioni 29.4 na hata ukiacha hiyo ukachukua hekta zile milioni 2.3 ambazo zina uwezekano mkubwa kwa maana ya kwamba ina mito ya uhakika basi kiasi hicho ambacho ndicho kilichotekeliza mpaka sasa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2001 mpaka leo hekta 280,095 ni kiasi kidogo sana hasa kwa nchi yetu ambayo kila mara tumekuwa tukitegemea mvua wakati mabadiliko yale yanapotokea tunapata misukosuko. Kwa hiyo, kiasi hicho cha hekta za umwagiliaji 200,000 kati ya hekta 2,300,000 ni kidogo sana ni asilimia 8 ambayo ni kiasi kidogo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, Waziri alipokuwa anajibu swali wakati wa kipindi cha maswali na majibu asubuhi alikuwa anazungumzia mkakati kabambe kwa kweli kwa uelekeo huu ukabambe hauonekani. Ningedhani kuna haja kabisa ya Wizara ya Mipango kama Mheshimiwa Mzindakaya alivyoelezea kwamba ielekeze Wizara hizi nyingine katika kutatua matatizo kulingana na mipango ambayo ni bayana na inayoelekeza kule ambako utatuvi unaweza kupatikana. Nitatoa mfano. Katika Tanzania tuna maeneo makubwa mawili ambapo utegemezi wa mvua unaweza kupunguka kama tukijielekeza huko. Bonde la kwanza ni bonde la Mto Rufiji. Bonde hili la Mto Rufiji linagusa mikoa minane kwa kiasi kikubwa ni Mkoa wa Mbeya, Iringa, Morogoro na Pwani. Hiyo inaguswa kiasi kikubwa na bonde hili. Pia mikoa mingine ambayo inaguswa kwa kiasi kidogo ni Mkoa wa Singida, Dodoma, Ruvuma na Lindi. Sasa kama unahusisha mikoa minane katika umwagiliaji ambao una mito ya uhakika, mito hiyo inayotengeneza bonde la Mto Rufiji ni mito mikubwa yenyе uhakika upo Mto Ruaha, Kilombero, Ruhuji na Rufiji yenyewe. Sasa eneo kama hili linahitaji tuelekeze huko ili kuweza kupambana na tatizo la kutegemea mvua. Tafiti nyingi zimefanyika katika bonde hili la Mto Rufiji. Zimefanyika na Makampuni yenyе uwezo wa kutoa majibu sahihi. Kuna Kampuni moja ya Kijerumani. *JICA* imeshughulika pia, *NORCONSULT* wamefanya utafiti na *RUBADA* ambayo ndiyo ilipewa jukumu la kusimamia uendelezaji wa bonde hili imekuwa ikisimamia tafiti mbalimbali.

Matokeo ya tafiti hizi yamedhihirisha kwamba mbolea ya asili ya bonde hili inawezesha bonde hili kuzalisha hadi tani 7 kwa hekta za mpunga. Sasa hata ungetumia nusu ya eneo hili ambalo lina mabonde madogo madogo Usangu, Kilombero na Rufiji Chini kiasi cha hekta 617,000 zina uwezo kabisa wa kuzalisha kiasi kikubwa sana cha hiyo nafasi. Hiyo basi ni dhahiri kule ambako utafiti ulikwishafanyika na ikadhihirika na kule ambako kuna raslimali hiyo ya uhakika ya maji ndiko ambako nadhani Wizara hii ingestahili ielekeze kiasi kikubwa cha fedha kwenda katika uzalishaji ili tuweze kupata mavuno.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Bonde la Mto Malagarasi. Bonde hili ni sehemu ya Aldowevu ya Lamsa na ukubwa wa eneo hili ni hekta mia tatu na laki mbili na hamsini. Lakini kati ya hizi ambazo ukiondoa misitu ambazo zimedhihirika kwamba zina uwezo wa kuzalisha kwa njia ya umwagiliaji ni hekta laki sita sawa karibu na lile bonde la Mto Rufiji. Ardhi pia ile inafanana kwa uwezo wa kuzalisha kwa hekta kiasi cha tani hadi saba. Kama tungeelekeza mipango yetu katika bonde hili na bonde lile linagusa mikoa minne Mkoa wa Kigoma wenyewe kwa Wilaya zake zote tatu na Mkoa wa Shinyanga Wilaya Bukombe, Mkoa wa Tabora Wilaya ya Urambo na Sikonge na Mkoa wa Rukwa Wilaya ya Mpanda. Kwa hiyo, ungekuwa umehusisha mikoa mingi katika utekelezaji kwa kutumia raslimali ya maji yenye uhakika. Kwa sababu ardhi au mbolea ya asili katika eneo lile lina uwezekano wa kuzalisha hadi tani 7. Kwa hiyo, tatizo la upungufu wa chakula lingekwisha kama tungejielekeza katika utekelezaji wa mabonde haya. Kwa hiyo, ndipo tungezungumzia mpango kabambe kama tungejielekeza huko wa umwagiliaji sio hii ya kudonoa donoa ambao unakuta kuna hekta 7,000 au hekta 200,000 tu. Baada ya kusisitiza hilo ningeiomba kabisa nimalizie kwa kusema kwamba katika kulitekeleza hilo ni lazima mpango mkubwa uandaliwe utakaojumuisha maeneo hayo makubwa mawili. Hata hayo mengine yataendelea lakini kipaumbele kiwekwe katika maeneo hayo. Pia inavyodhihirika kilimo hakivutii wawekezaji kutoka nje, lakini sekta ya madini inawavutia. Sasa mapato yote yanayopatikana kutoka sekta ya madini tuyaelekeze katika maeneo hayo ya uzalishaji kwa njia ya kilimo.

Mwisho kuna suala la mbolea. Mimi ni mjambe katika Kamati ya Kilimo na Ardhi ilioneckana kwamba mbolea ya *Minjingu Phosphate* haijahamasishwa vya kutosha. Mimi nilitembelea mkoaa ule wa Arusha nikakuta kule *Minjingu Phosphate* raslimali ya *phosphate* iliyoko pale kwa maelezo ya Meneja wa Kiwanda kile ni tani 15 milioni. Mbolea hii haina madhara kwa ardhi, mbolea hii inaweza kupatikana kwa bei nafuu. Lakini inaoneckana wakulima hawajaipendelea ni kwa sababu haijahamasishwa kwa hiyo Wizara ya Kilimo ingehamasisha wananchi kutumia mbolea hii kwa sababu ni raslimali ya asili ya kwetu tunayo katika Tanzania. Tani zote hizi bado hazijavunwa zingewenza kusaidia katika kuimarisha kilimo chetu katika nchi hii na ktuondoa katika adha ya kulazimika kuomba chakula au kununua chakula kwa dharura kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naziunga mkono hotuba zote mbili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. ELISA D. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2004/2005. Kabla ya mchango wangu, naomba nitoe pongezi kwa Mawaziri wote wawili, Manaibu Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu na Watendaji wao kwa utekelezaji mzuri wa bajeti ya mwaka 2003/2004 na maandalizi mazuri ya Bajeti ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, aidha niipongeze Serikali hususan Kamishna Mkuu wa *TRA* kwa ukusanyaji mzuri wa mapato ya Serikali katika mwaka wa 2003/2004 ambapo walivuka malengo yaliyokuwa yamewekwa. Baada ya pongezi hizo tunawapa shime ya kufanya vizuri katika mwaka ujao wa fedha wa 2004/2005. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 imetoa kipaumbele kwa Sekta muhimu za uzalishaji na kuondoa umaskini ambazo ni maji, elimu, afya, barabara, kilimo (ambayo inajumuisha uvuvi na ufugaji), pamoja na wawekezaji katika Sekta hizi muhimu za uzalishaji. Aidha, wastaafu, walimu na wafanyakazi wamekumbukwa katika Bajeti hii. Kwa sura ya bajeti hii na kwa mwelekeo wa Bajeti hii, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo machache kwa nia ya kuomba kupata ufanuzi kwa Waheshimiwa Mawaziri wahusika. Kwanza kabisa nianze na kodi za kilimo. Inaridhisha kuona kwamba Serikali imetambua umuhimu wa hii Sekta ya Kilimo na imeondoa baadhi ya ushuru na kodi mbalimbali ambazo zilikuwa zimelimbikizana kwenye hii Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, katika mwaka wa fedha uliopita 2003/2004 pia Serikali ilifuta kodi zote za usumbufu katika uchumi wetu na katika jamii yetu. Kutokana na hayo mawili, ningeomba niikumbushe Serikali kwamba wameacha kodi moja ambayo inawagusa Wananchi moja kwa moja na inawagusa wakulima moja kwa moja, nayo ni kodi ya mashamba ya Shilingi 200 kwa eka. Nakumbuka kabisa kwamba Serikali ilisema kodi ambazo ni za usumbufu zote zimeondolewa na zitaendelea kuondolewa. Sasa, hii kodi ya namna hii ambayo haina madhara yoyote kwenye mapato ya Serikali lakini inamsumbuwa sana mkulima ni kwa nini imebakizwa na Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kodi hii naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba, kodi hii ingawa inaonekana ni kidogo, lakini katika hali ya kilimo chetu cha uhaba wa mvua mwaka hadi mwaka ni kubwa. Inaweza kutokea miaka mitatu, minne mfululizo mkulima hapati mavuno yoyote na kodi hii inalimbikizana mpaka inakuwa kubwa kabisa kiasi ambacho inakuwa ni kero kwa mkulima. Kwa sababu Serikali imekubali kwamba inaondoa kodi hizi za usumbufu na ambazo ni kero kwa Wananchi tunaomba itazame upya ili kuondoa kodi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Utabiri wa Hali ya Hewa. Katika hatua mbalimbali ambazo Serikali itachukua kuboresha kilimo, kuboresha uzalishaji ni pamoja na kurekebisha ama kuwekeza katika Utabiri wa Hali ya Hewa katika nchi yetu. Wakati tunaelekeza nguvu zetu kwa muda wa kati na muda mrefu kwenye kilimo cha umwagiliaji ni vema pia tutazame hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa katika muda huu wa sasa, nazo ni pamoja na kutambua kwamba sehemu kubwa ya kilimo cha nchi yetu bado kinategemea mvua. Ni muhimu basi katika hili Utabiri wa Hali ya Hewa uzingatiwe ili wakulima wawe na uhakika wa nyakati za mvua, wawe na uhakika wa mbegu ambazo zitaendana na mvua ambayo inatarajiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tukisikiliza na ninaamini wote tunasikiliza Taarifa za Hali ya Hewa katika nchi yetu. Katika *channels* zote za TV, Watabiri wa Hali ya Hewa wana sentensi moja tu ya kwamba: "Kutakuwa na mvua za hapa na pale na manyunu ya hapa na pale na vipindi virefu vyaya juu." (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba kwa kweli wakati umefika kwa kitengo hiki cha Utabiri wa Hali ya Hewa na kwa sababu naamini tuna wataalam katika taaluma hii naona ni vema Serikali sasa ijizatiti iwape hawa wataalam wetu vitendea kazi tusiwe tena tunapata taarifa za mvua za hapa na pale, manyunu ya hapa na pale na hawasemi mvua kiasi gani na hawasemi hapa na pale ni wapi. Naomba hilo lizingatiwe wakati tukijiandaa kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji kama alivyosema Mheshimiwa Ndeka ambaye amenitangulia kuzungumza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kuzungumzia juu ya Mifuko ya Uwezeshwaji. Tunaipongeza Serikali kwa kutenga Mifuko hii ya Uwezeshwaji wa Wananchi kushiriki katika ukuaji wa uchumi wetu kwa njia ya kupata *credit facility* kutoka Serikalini na kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya fedha. Mifuko hiyo ni dhamana ya mikopo kwa wauzaji wa bidhaa nje (*Export Credit Guarantee Scheme*) na dhamana kwa wafanyabiashara wadogo wadogo (*Semi Credit Guarantee*).

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba Mifuko hii ilikuwepo tangu mwaka huu wa fedha tunaomalizia sasa wa 2003/2004, lakini tulipokuwa tunatazama taarifa mbalimbali za Serikali na Mashirika mbalimbali tulikuta kwamba bado fedha hizi hazijatumika kikamilifu kama ilivyopangwa. Wadau wa Mifuko hii hawakuelewa Mifuko hii inaendeshwaje na hawakuelewa hata kwamba wafuate fedha hizi katika sehemu gani kwenye vyombo hivi. Maelezo yaliyotolewa na katika taarifa hizi ni kwamba miongozo, taratibu, kanuni za utumiaji wa fedha hizi zilikuwa bado hazijakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, naona katika mwaka ujao wa fedha wa 2004/2005 Serikali imeweka tena fedha, imetunisha tena Mifuko hii kikamilifu, ni hatua nzuri. Lakini kama Wananchi husika hawatapata elimu, hawatapata ufanuzi mzuri, hawatakuwa na taratibu na kanuni ya jinsi gani ya kupata mikopo hii, tutamaliza tena mwaka ujao wa fedha bila fedha hizi kutumika na itakuwa siyo jambo zuri na haki. Ukuaji wa uchumi uliokusudiwa hautakuwepo. Kwa hiyo, naomba basi Serikali iandae utaratibu mzuri na kanuni na itoe elimu ya kutosha kwa Wananchi ili tuweze kutumia Mifuko hii kikamilifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba nizungumzie juu ya Taasisi za Fedha. Inaridhisha kuona kwamba Serikali imekubali kufungua ama kuanzisha Benki ya Maendeleo na Kilimo kwa kuigeuza *TIB* kuwa Benki ya aina hiyo. Serikali pia imetueleza kwamba wataangalia, watachunguza vizuri tena vyombo vingine vya fedha kama Benki ya Posta na Benki ya *National Bureau de Change* kutazama kwamba watafanya nini nazo.

Mheshimiwa Spika, katika hili ningombia niishauri Serikali kwamba Benki hii ya Maendeleo na Kilimo, basi ifunguliwe mapema ili Wananchi na wakulima hawa wanaotaka kuingia kwenye miradi ya maendeleo waweze kupata huduma hii kwa hakika kutoka kwenye chombo hicho kitakachoundwa. Aidha, Benki hizi mbili za *Posta na*

National Bureau de Change Serikali iamuwe iwape *license wa-operate* kama Mabenki kamili.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie juu ya Taasisi za Taaluma mbalimbali katika nchi yetu. Kuna Taasisi mbalimbali za taaluma mbalimbali katika nchi yetu na ningependa kujielekeza katika Taasisi za Uhasibu na Takwimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi imepata nafasi ya kutembelea baadhi ya Taasisi hizi na tulikuta kwamba wana upungufu mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo na mahali pengine kama *Tanzania Institute of Accountancy (TIA)* wana upungufu zaidi wa fedha za miradi, wana upungufu wa walimu kwani kuna karibu nafasi 10 ambazo hazijajazwa kwa miaka karibu miwili. Hii inatokana na mishahara kuwa midogo na kukosa pia hata mishahara hiyo midogo ambayo wangepaswa kuwalipa hao walimu watakaoajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika hili tungeomba kuishauri Serikali kwamba, pale ambapo wameji-*commit* kutoa ruzuku, kutoa fedha za miradi ya maendeleo, kutoa fedha za kusaidia Vyuo na Taasisi hizi, wajaribu kuwa waungwana na kutoa fedha hizo zinazotakiwa na kwa muda unaotakiwa. Katika Chuo kile cha Takwimu wana shida ya maji. Hutaamini kwamba hapo chuoni wenyewe chuo hicho wanawantuua maji ya kunywa na hawana barabara nzuri ya kufika kwenye Chuo chenyewe. Tunaomba haya yatiliwe maanani.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kuwakumbuka wastaafu ambao sasa wataendelea kupata mafao yao kutoka Serikalini. Kwa niaba ya wastaafu wa Jimbo langu la Arumeru, naishukuru sana Serikali kwa suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nizungumzie suala hili muhimu sana la kuipongeza Serikali kwa kukabiliana na tatizo kubwa la njaa lililotokea mwaka wa 2003/2004 ambapo iliweza kutenga fedha zake katika Bajeti ya Serikali na kusaidia kupunguza makali ya upungufu wa hali ya chakula nichini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache narudia kusema naunga mkono hoja hii ya Bajeti. (*Makofii*)

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi katika kipindi hiki na ukatuheshimu wanawake kwamba na sisi tuna mchangano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Basil Mramba pamoja na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Wataalam wote katika Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuleta hoja hii. Lakini pia nampa pole Mheshimiwa Kigoda kwa kumpoteza baba yetu. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, na mimi kama wenzangu nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga kwa ushindi mkubwa alioupata kwa tiketi ya CCM. Mheshimiwa Makanga ni mwenzetu na ninaamini ataendeleza Sera za CCM kama alivyowaahidi Wananchi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Getrude Mongella kwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Wanawake wa Tanzania tumefurahia sana suala hilo, tumelipokea na tunajivuna kuona kumbe wanawake wana uwezo mkubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bajeti, pia kama wenzangu nimeona kwamba Bajeti hii ni nzuri na ya kufurahisha na kutia moyo na pia inatupa imani kwamba ikisimamiwa vizuri italeta maendeleo. Bajeti hii ina mwelekeo wa kumtetea mkulima, mfugaji, mvuvi na mfanyakishara mdogo mdogo kama Mheshimiwa Waziri alivyotueleza. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha waziwazi kwamba sasa katika nchi yetu kiwango cha uchumi kinainuka. Pia, katika hoja yake ameonyesha wazi kwamba mwaka 2004 uchumi umeinuka kwa asilimia 6.3, mwaka 2005 asilimia 6.5, mwaka 2006 asilimia 6.9 na mwaka 2007 asilimia 7.4. Kwa hiyo, hii yote inaonyesha kwamba kazi inafanyika na uchumi umeinuka kwa sababu takwimu zimetuonyesha. Tunashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, tunaishukuru Serikali yetu kwa kutueleza kwamba mapato yetu yamefikia Sh.1,739,288,000,000/= na pia tumeleweshwa kwamba upandaji wa bei utapungua itakapofikia Juni 2005 kwa kufikia asilimia 4. Hizi zote ni pongezi kwa Serikali yetu kwa sababu Rais wetu alituambia kwamba kama sehemu imefanya vizuri tusione haya kujisifu, tujisifu na pale panapohitaji kukosolewa, tutakosoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ya mwaka 2004/2005 tumelezwa imekusudia kuongeza mapato, kupunguza utegemezi, kuondoa umaskini na kutobeba madeni. Sasa labda nianze kuangalia suala moja moja. Suala la kwanza ni kuongeza mapato. Tunaishukuru Serikali kwa kuongeza mapato na kama ilivyolezwa katika hoja hii ukurasa wa 11 kwamba: "Kwa sababu ya sera nzuri, utawala bora na usimamizi imara wameweza kukusanya mapato makubwa." Kwa hiyo, tunaipongeza *TRA* kwa kazi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya pongezi kwa *TRA*, ningependa kuwaambia kwamba bado hawajachukua hatua ya kuweza katuondolea kero kwa wafanyakishara wadogo wadogo kule Mlandege Zanzibar. Ningemba *TRA* iangalie tena hizi kero kwa sababu tuliamiwa hapa inaundwa Kamati, sasa imefikia wapi maana bado kero za wafanyakishara ndogo ndogo zipo kwa upande wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika kuongeza mapato Serikali imetuambia kwamba gesi yetu ya Songo Songo tutaweza kutumia ifikapo mwezi wa Julai, 2004. Nilikuwa natazama katika kitabu chetu cha mipango ya 2004 na tunajua kwamba tukiiza gesi hii mapato yake ni ya Muungano, lakini katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa

Mipango na Ubinafsishaji hajaonyesha mgao utakuwaje kwenye mapato, basi hata kukisia tu mbona hamna lolote? Ningependa nifahamu kwamba inakuwaje kwa sababu tunaelewa kwamba gesi ikiuzwa tutakuwa pamoja katika mapato. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pia, ninashukuru wameelezea katika hoja yetu hapa kwamba sheria mbalimbali zinafanyiwa marekebisho mfano Sheria za Madini na pia Sheria za Kodi, tunashukuru sana.

Lakini tunaposema tunaongeza mapato halafu tukiangalia katika Mashirika yale ya Wizara ya Viwanda na Biashara mfano *CAMATEC*, *SIDO* na *TIRDO* Bajeti hii wamepangiwa mshahara tu. Kwa mwaka mzima watafanya kazi gani?

Hawa *CAMATEC* wanafanya utafiti na *SIDO* wanashughulika na viwanda vidogo vidogo. Wananchi wanyonge wa nchi hii ndiyo tunawategemea, mbona wamepangiwa mishahara tu, hawatazalisha hawa, hamna lolote litakalofanyika! Nafikiri Mheshimiwa Waziri angenisaidia kwa sababu ni moja ya njia za kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza utegemezi, tumeona sote hapa kwamba bajeti hii bado ni tegemezi, misaada na mikopo ya masharti nafuu bado Serikali itaitumia. Tumeona hapa katika jedwali la mwaka 2003 utegemezi ulikuwa asilimia 47, mwaka 2004 asilimia 45, 2004/2005 asilimia 41, sasa bado ingawa tunapata mafanikio, lakini hili linatutia dosari. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba tuangalie ni namna gani tutaweza kupunguza utegemezi huu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika nchi yetu tumpatanya nafasi ya *AGOA*, hili soko la kwenda kupeleka bidhaa zetu ambazo zitaleta fedha za kigeni. Nchi kama Kenya na Lesotho wametumia kama Dola milioni 200, lakini wameongeza Dola bilioni 1 mpaka 2, sasa Tanzania je? Ningewomba Mheshimiwa Waziri tuangalie tena ni vipi Serikali itatusaidia Watanzania ili tuweze kutumia hili soko la *AGOA* kwa sababu litaongeza fedha za kigeni kuliko huu utegemezi mkubwa ambao tunauouona hapa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu kuondoa umaskini katika Bajeti yetu na ninashukuru kabisa katika hoja ya Waziri hapa ametilia mkazo kuboresha mazingira kwa ajili ya kukuza Sekta ya biashara ndogo ndogo na za kati ili kuondoa umaskini na (ninanukuu katika ukurasa wa 48).

Mheshimiwa Spika, katika kuondoa umaskini Serikali yetu imeweza kuhamasisha Vyama vya Ushirika na hasa katika Chama hiki cha kuweka na kukopa, *SACCOS*. Katika Tanzania sasa Wilaya nyingi wameanzisha *SACCOS* na hiki Chama cha Ushirika ambacho ni cha kuweka na kukopa ndiyo Chama cha wanyonge na ndiyo kitawasaidia hawa wakulima wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo, wavuvi na wafugaji.

Sasa ningeomba basi kwamba katika Sekta husika tuongeze mitaji ili *SACCOS* ziimarike kwa sababu hizi ndizo Benki za wanyonge katika Vijiji. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tunazungumzia katika kuondoa umaskini, hapa imeelezwa katika ukurasa wa 39 kwamba Tume yetu ya Pamoja ya Fedha imetenga fedha katika Bajeti hii, ile asilimia 4.5 % kutokana na misaada.

Mwaka jana tulipangiwa asilimia 4.5 na mwaka huu asilimia 4.5. Sasa wanyonge na maskini wa kule Zanzibar ambao na sisi tunasubiri hii kila mwaka mbona haiongezeki wakati kwingine kote tunaona kunaongezwa? Halafu tunashukuru kwamba Mwenyekiti wa Tume hii ya Pamoja ya Fedha, Mheshimiwa William Shellukindo, yumo humu ndani ya Bunge, yeche atatuelewesha kwa sababu hata pesa alizoomba kapewa milioni 700 badala ya kupewa bilioni 1 na laki 8. Kweli watafanya kazi au bado mnataka Zanzibar tubakie kusikitika na hii 4.5%? Naomba Mheshimiwa Waziri aiangalie sana hii 4.5%. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa nina swalî moja. Sisi wanawake wa Tanzania tumeshirikishwaje katika Bajeti hii? Ningombâ Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, wakati wa ku-*windup* watueleze au walieleze Bunge hili kama Bajeti hii imizingatia masuala ya kijinsia kisekta. Mbona katika mipango sijaona?

Bajeti imekuwa ikituambia kwamba inanufaisha wakulima, wavuvi, wafanyabiashara wadogo wadogo na wafugaji; je, wanawake wavuvi ni wangapi? Tunajua kwenye maeneo ya maziwa wapo wavuvi, lakini ni wangapi? Wafugaji wakubwa wanawake wapo wangapi?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itusaidie sana katika suala hii wakati wa kutuelimisha. Je, utaratibu wa masuala ya jinsia umezingatiwa? Kuna mwongozo wowote kwa Wizara zingine walopewa ili waingize masuala ya jinsia? Kama maagizo hayo yapo basi yalizingatiwa na Wizara nyininge au kisekta?

Ningeomba tuelezwe haya kwa sababu sisi wanawake wa Tanzania tutajitahidi kubuni njia zozote za kuweza kuinua kiwango cha uchumi wetu kwa kuongeza juhudi zetu katika kutekeleza sera katika Sekta binafsi, lakini tuone na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji inatuangalia katika kutupangia haya masuala. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba tunashukuru kwa sababu tumeambiwa kuwa vimeondolewa vikwazo katika kuendeleza kilimo na biashara ndogo ndogo na mikakati mahsusî ya kuwapatia wanawake elimu ya juu. Tumeona leo kuna gazeti la Majira hapa wamesema: "Vichwa 20 ambavyo vimepata *point* saba katika mtihani wa *form four* mwaka, 2003."

Katika hao tumeangalia 10 ni wasichana. Inaonyesha kwamba wasichana au akina mama tunahitaji sana mkakati wa kupatiwa elimu ya juu kwa sababu tunakwenda sambamba mpaka *form four*, lakini ukienda *form six* na Chuo Kikuu takwimu zinashuka.

Kwa hiyo, hapa ninaomba kabisa Wizara inayohusika inapokuja itupangie mkakati wa kusaidia akina mama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninaipongeza Bajeti hii kwa kuwa na mkakati wa kujenga ukumbi mpya wa Bunge ili Wabunge wanawake tukiingia tusiwe na matatizo. Pia, ile asilimia 30 na isiwe katika Viongozi wa Bunge tu, lakini tutakwenda ngazi hadi ngazi mpaka tufikie asilimia 30. Tunaanza na wale ambao wanatunga sera, lakini tutaendelea kwenye ngazi zote za maamuzi, asilimia 30 inakwenda. Naomba wenzangu walielewe hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaipongeza Bajeti kwa kuweka pesa za uwanja wa michezo ambao Watanzania kwa muda mrefu tunauhitaji na Mungu akijaalia na sisi tutakuwa tunashinda kama wengine kwa sababu tatizo kubwa likuwa ni kwamba hatuna uwanja wa kisasa. Kwa hiyo, hii Bajeti ni nzuri kwa sababu inatugusa wazee na vijana na Wananchi wote kwa jumla kwa sababu michezo ni lazima kwa afya zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja lakini nijibiwe masuala yangu kuhusu mtazamo wa Bajeti na ushirikishwaji wa wanawake katika mwaka 2004/2005. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika siku ya kwanza ya kuchangia Bajeti hii.

Pili, ningependa nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kwenye Bunge la Afrika na nimpongeze Mheshimiwa Mongella, Mheshimiwa Ntagazwa, Mheshimiwa Ng'wandu kwa kuchaguliwa kuwa viongozi katika ngazi ya Afrika. Tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile napenda nimpongeze Mheshimiwa Danhi B. Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge kuitia Chama cha Mapinduzi. Mimi nina uhakika Mheshimiwa Danhi Makanga, alipogombea kuitia Chama cha *UDP* wananchi hawakufurahi. Sasa alipogombea kuitia Chama cha Mapinduzi, nadhani hapo ndipo walipokuwa wanataka. Kwa hiyo, nawapongeza sana wananchi wa Bariadi kwa kuchagua mgombea kutoka Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niwape pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na mzazi wao mpendwa. Mungu aiweke mahali pema peponi roho ya Marehemu. Vile vile niwape pole Mheshimiwa Anne Malecela pamoja na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa matatizo waliyoyapata wakati wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Vile vile niombe Serikali ilione hilo na iangalie maeneo kama haya yenye matatizo ijaribu kufanya msako wa mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri walioifanya ya kuandaa Bajeti hii. Ni kweli kabisa kwamba Bajeti hii

itakuwa ni nafuu kwa wananchi wa Tanzania. Lakini vile vile pamoja na unafuu huu ni vizuri basi tukachangia kwa yale maeneo ambayo tunaona pengine yana mapungufu fulani fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie suala la kilimo. Kilimo naamini Watanzania wote tunajua kwamba ili umaskini uondoke ni lazima watu walime. Vile vile ili tuweze tuishi ni lazima tulime. Vile vile ili uchumi wa nchi uongezeke ni kilimo. Suala la kilimo ni la muhimu wote tunajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile niipongeze Serikali kwa mipango mizuri iliyoweka kwa ajili ya kusimamia suala zima la kilimo. Lakini mimi niombe basi kwamba kilimo hiki kiboreshwe. Najua wananchi najua kwamba tunalima na kila siku wananchi tunalima. Sasa bila kuangalia utofauti wa kilimo cha wananchi na yale yanayosimamiwa na Serikali ni kweli wananchi hawataelewa. Wataona kama hakuna watalaan wanaowasaidia, wanaoelekeza kama hakuna msaada wowote unaotoka Serikalini, kama hakuna lolote linaloonekana kutoka Serikalini kuhusu kilimo, wananchi hawataelewa kwa sababu wanajua kwamba wao ni wakulima wa kila siku. Sasa kwa sababu Serikali tayari imeshasema kuhusu kuanzisha benki za kilimo, naomba niipongeze Serikali. Kama ni kweli Serikali itasimamia suala hili basi ni vizuri tukaelewa benki hizi zinaanzishwa na nani? Zinaanzishwa na wakulima wenyewe, zinaanzishwa na watu mbalimbali kutoka nje, au zinaanzishwa na nani. Maana isije ikafika mahali tena benki imeanzishwa mara tena inauzwa, mara ina binafsishwa, na kadhalika. (*Makofi*)

Sasa ni vizuri basi maadam suala hili limeonekana mapema basi lielezwe kwa uwazi zaidi ili lieleweke kama kuna wananchi na kama kuna watu ambao wako tayari kuanzisha benki kama hii, basi ieeweke na vile vile ieeweke kwamba mabenki yote yanayoanzishwa yaanzie mijini. Wakulima wengi wako vijijini. Sasa mkulima kutoka kijijini aje mijini kukopa kidogo inamwia vigumu.

Sasa basi tunaiomba Serikali kama benki hizi zinaanzishwa basi zianzishwe katika maeneo ya wakulima, ili wananchi waelewe, wajue na waelimishwe vyta kutosha waweze kukopa kwa sababu ni kweli kama wananchi wetu wataendelea kutumia jembe la mkono, kilimo kama hiki hakitawakwamua katika suala zima la kuondoa umaskini na wala hakitawaongeza kipato cha aina yeoyote.

Tunaiomba Serikali katika mikakati iliyojiwekea, basi wananchi waelimishwe zaidi, wahusika waende vijijini wakawaelimishe wananchi wetu, wakulima wetu. La msingi vile vile wote tunaamini na tunajua na tunaelewa kwamba kilimo ni akina mama. Wakulima wakubwa wa nchi hii ni akina mama. Tunachowaomba ebu hii nafasi ya akina mama iangaliwe. Akina mama wapewe nafasi, ni kweli ni wakulima wazuri, sasa waangaliwe ni vipi wasaidiwe ili kilimo hiki wanapokilima basi wapate matunda mazuri. Kama Serikali ya nchi hii ikitaka kilimo kifanikiwe basi tuwaelimishe akina mama zaidi vinginevyo kilimo hakitaenda sawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nizungumzie suala la utafiti. Katika miaka iliyopita tulikuwa na vituo vingi vyta kufanya utafiti katika masuala ya kilimo, masuala ya

mbegu, masuala ya madawa, masuala ya aina mbalimbali. Lakini sasa hivi unakuta vituo kama hivyo kwa kweli bado havijapewa umuhimu. Nikichukulia kituo kingine ambacho kiko Hombolo pale na kingine ambacho kiko Mpwapwa kwa kweli havifanyi kazi kama vilivyokuwa vikifanya kazi huko nyuma. Tunaiomba Serikali kama ni kuvióngezea fedha basi hivi vituo viongezewe fedha na viweze kufanya kazi yake vizuri. (*Makofî*)

Vile vile taarifa za utafiti zinazofanywa na watalaam wetu sijui zinafungiwa masandukuni, sijui zinafungiwa kwenye makabati hata hatuelewi. Tafiti kama hizi ndizo ambazo zinatakiwa wananchi wazione, wazijue, waelewe matatizo ya kilimo ni nini, vinginevyo hizo tafiti hazina maana yoyote. Haziwasaidii wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba hilo Serikali ilijue na ilione na naamini inalijua. Lakini jambo la kushangaza hajjalitoa wazi. Kama mtu amefanya utafiti basi arudi kule alikofanya utafiti akawaeleze wananchi, akawaeleze wakulima, akawaeleze wafanyabiashara kwamba utafiti niliyofanya katika eneo hili, ulikuwa unahusu hili, hili na matokeo yake ni haya. Sasa hakuna sababu ya kufanya utafiti kama tafiti haziwezi kufanyiwa kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nizungumzie suala la zana za kilimo. Zamani katika vituo nilivyoeleza vilikuwa na matrekta, yalikuwa yanaletwa na Serikali. Sasa wananchi walikuwa wanapata urahisi wa kwenda kukodisha matrekta pale na kwenda kulimia mashamba yao na kukuza kilimo chao.

Lakini sasa hivi huo utaratibu haupo pamoja na kwamba sasa hivi biashara ni huria, lakini sasa ni kweli ni huria, lakini kuna maeneo ya kuangaliwa, kwa mfano suala la kilimo, bado tunahitaji Serikali itusaidie zaidi. Lakini ukimwacha mwananchi asilione trekta mahali lilipo ni shida. (*Makofî*)

Kwa mfano kuna maeneo fulani nilisikia jana mwenzangu alikuwa anasema kwamba kuna sehemu nyingine watoto wakiona trekta wanakimbia. Sasa namna hiyo kwa kweli haiwezekani hata kidogo. Kwa hiyo, tunaomba zana hiz i zifikishwe vijijini. Vile vile ningeomba niishukuru Serikali kwa suala la kupunguza kodi au kuwaondolea kodi wafanyabiashara ndogo ndogo, ambao ndiyo hao hao wanauzza biashara kutoka mashambani, akina mama wanauzza mboga mboga, wanauzza vitu mbalimbali. Kwa hiyo, kuwaondolea kodi hizi ni kweli itawasaidia angalau kipato wanachokuwa wakikitoa kwenye kodi kinaongezeka katika mapato yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile naomba nizungumzie suala la kilimo cha umwagiliaji. Suala la kilimo cha umwagiliaji sisi Mkoa wa Dodoma, tunayo mabonde. Kule Mpwapwa tuna Bonde la Matomondo, Dodoma Vijijini tuna bonde la Bahi, Kondoa tuna bombe la Bubu. Maeneo haya kama yangweza kufanyiwa kazi ndiyo Wizara itaonekana inafanya kazi. Lakini Wizara ikiendelea kuongea ongea tu hivi hivi kweli bado Wizara haitaonekana inafanya kazi. Mimi naomba Serikali ijizatiti katika maeneo ambayo itaonekana ni muhimu kusaidia, vinginevyo kwa kweli ndugu yangu Charles Keenja itakuwa ni tabu kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la elimu. Serikali inapata kigugumizi juu ya suala la elimu. Tunasema hivi hata elimu ya msingi ni baada ya Serikali kuamua elimu iwe kwa wote, ndiyo maana mashule mengi ya msingi yamejengwa, ndiyo maana vijana wengi wameongezeka kwenda shule. Lakini sasa ebu tufike mahali tuzungumze suala la sekondari. Kwa nini tusiamue tu kwamba sasa shule za msingi ziende mpaka sekondari tunangoja nini? Ni kweli kuna gharama zipo za kuendesha shule za sekondari, kuna gharama za walimu na vitu mbalimbali. Lakini tufike mahali tuseme, tugawane majukumu Serikali ifanye nini, wananchi wafanye nini, tukiendelea kuwa na kiguguzi namna hii miaka mingi itachukua. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu naomba niishukuru Serikali kwa wastaa fu kuwarejesha katika *computer*. Vile vile niwaombe basi Serikali katika wale wastaa fu waliostaafishwa bila ya utaratibu bila ya umri basi na wenyewe warudishwe huko maana yake hawakutegemea. Maana yake katika watu maskini wanaongezeka tumewaongeza kwa utaratibu huo. Tunaomba Serikali iwarudishe kwenye *computer*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la mishahara ya watumishi. Ni kweli Bajeti imepunguza maeneo mbalimbali ya kodi kuwanufaisha wananchi. Lakini vile vile basi tuwaone na wafanyakazi. Ebu Serikali iweke hata kitu kidogo katika mishahara yao, ni motisha ambayo inaweza ikawasaidia katika kufanya kazi vizuri zaidi.

Mimi naomba niishawishi Serikali angalau iongeze mishahara ya watumishi wote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la rushwa. Rushwa ni kweli ipo lakini sasa iko wapi ebu tunaulizana hii rushwa iko wapi? Kwa nini watu tunapenda kusemasema rushwa ukiambiwa mtaje basi aliyepokea rushwa unashindwa kumtaja. Sasa tutaendelea kusema hivi mpaka lini? Mimi naomba kabisa viongozi wa nchi hii wako wengi hata Mheshimiwa Rais, yuko tayari kumsikiliza mtu ambaye anaweza kwenda kumwambia na amesema mwenyewe, anayekwenda kumwambia kwamba fulani anakula rushwa atamsikiliza.

MBUNGE FULANI: Haitaisha kwa maneno.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mwenzangu mmoja anasema haitaisha kwa maneno ni kweli haitaisha kwa maneno. Lakini tukitamka tukasema kwamba fulani anakula rushwa hata kama una ushahidi mdogo mdogo, peleka huo huo Serikali itafanya kazi itamshughulikia. Lakini suala la rushwa, rushwa, haitaisha. Mimi nasema kwa kweli Serikali imejitahidi kudhibiti rushwa, ni lazima tujisifu. Kama hatujajisifu nani atatusifu jamani! Kwa hiyo, kwa kweli mimi niwaombe sana wenzangu au niombe sana Serikali katika suala zima la kuangalia maeneo yale ambayo Waheshimiwa Wabunge, wanayasemea basi wakati wa ku-*wind up* tujaribu kuyasemea na sisi tujue kwamba kweli sasa Serikali inatusikiliza na inatujibu maneno yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja hizi mbili za Wizara mbili kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa kuwa siyo mara yangu ya kwanza kusimama Bungeni katika kipindi hiki naomba pongezi zangu nizifupishe tu. Lakini nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda ,pamoja na kwamba nilikwishakutoa lakini hawakuwepo, naomba niwape rambirambi za dhati kabisa kwa kuondokewa na Baba yetu mpenzi. Mwenyezi Mungu awafariji na awape nguvu waweze kuvumilia katika kipindi hiki kigumu. Mwenyezi Mungu amweke marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba sikutaka kuzungumzia suala la rushwa, naomba nianzie hilo hilo kwa sababu sasa naona kuna u-turn ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge. Kwa kuanzia tu nataka niweke rekodi sahihi. Yako majina yalikwisha kutajwa na naomba hapa niseme kabisa kwamba Mheshimiwa Mtikila, alitaja hadharani majina hatujamwona akipelekwa mahakamani. Kama majina yaliyotajwa na Mheshimiwa Mtikila ni ya uongo ninaomba ku-*challenge* kwamba Serikali ina njia zote za kumpeleka Mtikila Mahakamani na tunaomba afikishwe mahakamani, ili hili suala la rushwa na wingu liliko liweze kuondoka katika wale walijotajwa. Vinginevyo tutakuwa tunafanya mchezo wa maneno hapa na Wabunge tunaanza kuzunguka kana kwamba huko tunakoishi hatuoni hiyo rushwa. Itakuwa ni ajabu kabisa kama Wabunge tunaanza kufanya u-*turn* leo eti kwa sababu hatuwezi kutaja majina. Rushwa hakuna asiyejua ilivyo ngumu kwa mtu wa kawaida kutaja, lakini Serikali ndiyo yenye vyombo na haitaki kufanya kazi yake. Mimi naomba hiyo, tuiweke vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme machache katika Bajeti. Lakini kabla ya kusema hayo, naomba niwapongezi Waheshimiwa Mawaziri, wote wawili na timu yao kwa kazi nzuri. Kwa kweli wamejithahidi kutoa Bajeti ambayo inaunganisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na kutoa unafuu wa maisha kwa watu wetu kwa sehemu kubwa. Lakini nina mambo machache ya kusema.

Jambo la kwanza katika Bajeti hii kwa wale walioangalia vitabu vya Bajeti kuna mambo ambayo mimi nafikiri tusipoyazingatia na kuyaangalia yataanza kuleta hatari katika nchi yetu. Mwaka jana tulianza na kutoa upendeleo kwa kanda na sina tatizo na upendeleo kwa kanda kwa maana ya kupunguza gharama ya mbolea katika ukanda wa Kusini. Tatizo langu ni kwamba haikupelekwa kwa jinsi tulivyoahidiwa. Lakini vile vile naomba niseme kwamba sina shida na kupeleka mahali kwa sababu lazima tuchukue *comparative advantage* pale panapozalisha kitu tuweze kusaidia tuka-*boost* uchumi vizuri zaidi ili uchumi wetu unufaikie kwa kile kinachowenza kuzalishwa na upande mmoja.

Lakini tatizo langu ni kwamba tusipoangalia tukafanya *comparative advantage* kwa sehemu zote za nchi hii tutaanza kutengeneza matabaka. Ukipeleka kwenye ukanda mmoja kesho ukapeleka kwenye Wilaya 47 Bajeti bila kuwa na mkazo kwamba hizi Wilaya zingine 160 na kitu zitafanya nini tunadhani tunaanza kutengeneza matabaka

katika nchi yetu kwa jinsi ile ambavyo tumeanza kuona matabaka katika mishahara. Nchi hii imejengwa katika misingi ambayo siyo lazima kila mmoja awe sawa kwa maana ya kuwa sawa kabisa. Lakini lazima kuwe na uwiano ambao unaondoa tofauti kubwa kubwa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Nataka kutoa mfano. Katika mwongozo uliotolewa na Serikali kuna vigezo vilivyotolewa ambavyo vimefanya nchi yetu sasa Wilaya 47 tu na sina hakika kama Waheshimiwa Wabunge wanajua hili, zinapata misaada kutoka Serikali Kuu. Sasa zingine hazina uhakika zinakwenda wapi. Lakini kinachonishtua mimi ni vigezo vinavyotumika kutoa hiyo, misaada ambayo inakuja kwa sura mbili. Sura ya kwanza ni kinachoitwa: *General Government Development Grants* na sura ya pili ni *Local Government Support Program*". Kwenye kitabu hiki cha hazina wanassema kwamba ni *pilot program*. Lakini sina hakika *pilot program* nchi hii ikianza inaisha lini. Tumeanza na maboresho leo bado tuko bado kwenye maboresho zaidi ya miaka 7 tangu tumeanza, ni wilaya zile zile na leo naambiwa kwamba kuna Wilaya 52 zinataka kuingia, lakini tuko pale pale na wilaya zile zilizoanza zinaendelea hivyo zile nyininge hazina kitu.

Sasa vigezo vilivyopangwa na Serikali mimi ndivyo vinavyotia wasiwasi mkubwa. Vigezo hivyo ni kwamba kwanza yule ambaye ataingia ni lazima *a- submit accounts for audit within three months after the end of the financial year*. Wote tunafahamu *submission* ya *account* inategemea wataalam. Serikali ndiyo inayopeleka watalaam kule kwenye Halmashauri, lakini inakuwepo kama kigezo kwamba huwezi kupata kama *accounts* zake hazijapelekwa. Inasema vile vile kwamba huwezi kupata hizo fedha kwa njia hizo mbili *GGD* na *LGSP* kama vile vile ulipata *adverse opinion* katika akaunti zake mwaka uliotangulia. Anayesababisha *adverse opinion* ni watalaam wale wale ulioletewa na Serikali. Lakini anayeadhibiwa leo ni wananchi wa wilaya husika, hawana uwezo wa kujiajilia watu wao hawana uwezo wa kumwajili mhasibu anayefaa, wala afisa mipango mahesabu yataandaliwa, hesabu zile zikakataliwa zikapewa *adverse opinion* wilaya inaadhibiwa wananchi wote wanaadhibiwa kwa sababu watalaam walioletwa na Serikali eti wamesababisha kusiwe na certificate ambayo ni clean. Kigezo hicho mimi nakisikitikia kidogo. (*Makofi*)

Lakini wanatuambia vile vile kwamba "*the council should prepare and submit quarterly implementation report*". Nani anatayarisha *implementation report*? Wabunge hapa sijui kama wanajua inakwenda kwenye council lakini zote zinapelekwa na wataalam wa Halmashauri wote ni waajiriwa wa Serikali. Wabunge hapa wanakwenda wanaangalia kilichopelekwa pale. Tuna tunakosa kwa sababu hiyo tena. (*Makofi*)

Kwa upande mwingine wanaongeza vigezo vingine kwa ajili ya *LGSP*. Navyo vinasema: "*The bank conciliation should be under taken monthly*". Sasa *reconciliation* Diwani au Mbunge atajuaje? Kwanza utujuaje kwamba wanafanya au hawafanya? Ukienda kule kwenye council ukisema wanafanya wanakumbia wanafanya. Lakini hakuna sheria inayolazimisha, wala siku hizi tena hakuna Diwani anayeweza kuamuru kwamba Mkurugenzi lete taarifa hizi wanafanya wao wanaleta wanachotaka. Mimi nina hakika Wabunge wote ni ndiyo hali halisi ilivyo.

Tatu, tunafanya nini Halmashauri inakwenda kukosa kwa sababu hiyo. Kigezo kingine kinazungumza: “*The council should have an internal auditor and reports issued by him/her should be acted upon*”.

Nani anaajiri *internal auditor* kama si Serikali? Mheshimiwa Waziri, naomba uniletee internal auditor kama sina ili niweze kutimiza sharti hili kama umeninyima hela kwa ajili hii. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wote wangependa kupata hiso fedha lakini hatuna kwa sababu hukutuletea hawa watu ambao unataka wafanye hiyo kazi.

Sasa hivi pia inatia utata na nitaomba Waziri anisaidie tunafanyaje. “*The council should contribute 5% of the cost of the project to be financed*”. Sasa tumefuta vile vianzio vyote vyta Halmashauri na tumesema Serikali inaleta ruzuku. Nitaomba Waziri anisaidie ninafanyaje ili hiyo 5% kutoka kwenye *local sources* tuzipate ili tuweze ku-access ile misaada ambayo tunaambiwa hapa tu-*contribute 5%*. (*Makofit*)

Sasa naacha hiyo kwa sababu viko vingi na Wabunge wakipenda nitawasaidia baadaye wapate hiyo. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba tunaweka vigezo kabla ya kutengeneza uwanja unaofanana kwa sisi sote kuchenza. Mimi nilifikiri kwanza Serikali ingetengeneza uwanja unaofanana, Halmashauri zote zikasaidiwa, zikifiki *level* fulani tuanje kuweka *bench marks*, lakini *bench marks* tunaziweka kabla hatujategeneza *fair level ground*, halafu tunaanza kugawa. Niliuliza kwenye kamati na naomba niulize tena leo Serikalini, nani anayetupa hizi *bench marks*, kuna msukumo gani? Mimi nimehudhuria semina moja na wenye semina ile walisema hatuwezi kutoa hela tu kwa sababu hela zetu zinatumbukia mpaka tuone kwamba zitatumika vizuri. Sasa je, zinatoka kweli hayo masharti yanatoka nje au ya kwetu ndani? Kama ni ya kwetu kwa nini hatukuandaa mazingira ya kwetu kabla hatujaanza kusema tutoe? Sasa Halmashauri 47 naomba kila Mbunge aangalie, lakini namwomba Waziri atusaidie Halmashauri hizi 47 atutajie hapa ni zipi ili nikitoka nijue kama ya kwangu ipo au haipo. Nina hakika Wabunge wote watataka kujua Halmashauri ziko au haziko pia kwenye mpango huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nigosia kidogo tu zao la biashara na la chakula. Mheshimiwa Waziri atusaidie kabisa kama tutaisifu Bajeti yake tunataka kujua utekelezaji wa mwaka jana wa zao la kilimo na chakula ambao aliahidi itapelekwa Wilayani tunataka kujua ilifika wapi? Mimi kwangu sijaona, nimeuliza kwenye mikutano wanasema hawana taarifa, walichoambiwa ni kwamba wapeleke takwimu, hatuna kitu zaidi ya pale. Sasa tulifiki kwamba zao lile lingeanza kufanyiwa kazi la chakula na biashara. Lakini hatuna kitu. Lakini kwenye vitabu vingine nimejaribu kuona inawezekana kuna wilaya wamepelekewa tena kuna Wilaya zimepelekewa zaidi ya milioni 100, milioni 200, milioni 300, lakini kuna wilaya zingine zina 15, zingine hazina. Ningetaka kujua kama hivyo ndivyo kama kuna waliopelekewa, Waziri atusaidie ni vigezo gani anatumia wakati hapa alitutangazia ni Halmashauri zote zitapelekewa kwa nchi nzima? Je, tumeanza kuwa na ubaguzi pia kwenye utaratibu huo au vipi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nilifikiri vile vile ni vema sasa tumwulize Mheshimiwa Waziri, katika Bajeti hii Serikali najua ni moja, huko nyuma tulikwisha liza fedha za *STABEX* Wizara ya Kilimo na Chakula, imetufanya semina hapa kwamba fedha nyingi sana za *STABEX* zitakwenda kwenye kilimo, kwenye *irrigation programme*. Kwenye Bajeti hii nimechunguza pote sioni tena popote, Waziri wa Kilimo tumeuliza hapa maswali mara kadhaa amesema ziko Hazina. Waziri wa Hazina wanasesma ziko ujenzi. Tungependa Serikali sasa iliambie Bunge hili, hizi fedha ziko au haziko? Kama ziko, ziko wapi? Na kwenye Bajeti zinaonekana wapi na zinakwenda kufanya kazi mahali gani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nigosie suala ambalo kidogo mimi limeniumiza. Katika taarifa ambayo imetolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nina hakika ni taarifa iliyofanyiwa kazi na ni utafiti ambao ni wa kweli kwa sababu ameeleza hata vitu vilivyo fanyika, inaniuma kabisa kuona kwamba sasa hata hela ya Ukimwi tumeanza kuzitumia vibaya au kuzi-*miss appropriate* au kuzila sijui lugha gani tutumie ipi. Kwenye kamati yetu tumeulizwa tulichengwa, majibu haya yanayotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, hayafanani na majibu tuliyopata kwenye Kamati. Sasa mimi ningombaa Serikali itupe jibu la kweli ni nini kimetokea, vitabu elfu tano na laki sita vinachapishwa, havikidhi mahitaji ya Wizara ya Elimu kwa sababu havikufuata utaratibu halafu ni sawa na vitu tulivyo tupa huko nje. Kwa hiyo, ni sawa na bilioni tumetupa wakati watu wetu wanaendelea kuangamia na Ukimwi. Ukimwi tumelesema ni janga la taifa haungojei, hauhitaji urasimu, hautaki utaratibu ambao ni wa kawaida lakini tunafanya vitu ambavyo vimeonyeshwa katika taarifa hii. Tungependa Serikali itupe taarifa ya wazi kabisa na sahihi kuhusu nini kimetokea kuhusu mradi huu wa ukimwi na fedha za watu zimetumika kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niseme kwamba Serikali imefanya vizuri tu katika kuondoa leseni za biashara ambavyo ni vianzio muhimu kwa Halmashauri. Tatizo langu ni jinsi maamuzi yanavyofanyika, Serikali tumekwisha kuoanisha mwaka wa fedha kwa Halmashauri na kwa Serikali Kuu, wote tunafanana sasa tunaanzia Julai, tunaishia Juni. Miongozo ya kutengeneza Bajeti, inatengenezwa na Serikali Kuu, Halmashauri zimekaa zimetengeneza tumekaa huko tumevutana tumetumia hela ya wananchi, tunatengeneza Bajeti, hatuna maelekezo yoyote leo ghafla unaondoa kile kianzio. Mimi nilifikiri kuna haja kubwa kabisa Serikali kujaribu kuwasiliana na vyombo vinavyohusika navyo ili waweze kuwa na mipango inayofanana ili leo tusirudi tena kwenda kutengeneza Bajeti ya Halmashauri. Anatuambia hapa kwamba tutapata *compensation*, lakini *compensation* tuliyopata kwa *Development Levy* haioani na fedha ambazo tulikuwa tunapata. Sijui kama Halmashauri zingine zinapata mimi ya kwangu haipati fedha tulizozipoteza kwenye *Development Levy* tunapata kweli ruzuku lakini haifiki kile kiwango na kwa sababu hiyo maendeleo yetu yanaanza kuathirika. (*Makofî*)

Sasa ameisema vile vile Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwenye taarifa ya Kamati na mimi nairudia hivyo kwamba ni kweli tukifuta kitu ni lazima tuanze kuitoa. Waheshimiwa Wabunge, sijui kama wameuona huu mwongozo. Serikali sasa imegawa utaratibu wa kupeleka fedha kwenye Halmashauri kwamba asilimia 70 itatumika kwa ajili ya *population* kwamba wataangalia *population* utapata mgao kufuatana na asilimia

70 ya *population* yako. Asilimia 20 ni *poverty count* sina hakika hii *poverty count* kama tuna *data* za kutosha kwa kila wilaya, asilimia 10 ni kwa *council area*, nadhani ukubwa wa eneo. Sasa ni vema kama tumeanza kuondoa kodi zetu basi ni vema tukaoanisha. Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tumefikia mwisho wa Kikao cha asubuhi kwa mujibu wa Kanuni, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi nilimtaja lakini ndiyo atakuwa msemaji wa kwanza kipindi cha mchana. Baada ya hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.49 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kuniruhusu nitoe mchango wangu wa mawazo. Umesema tunachangia hoja mbili na namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema kwamba atatekeleza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na nina imani hakusema atasikiliza pongezi, lakini atasikiliza na yale mengine ambayo pengine hayafanani na ya kwake.

Nilichotaka kuchangia cha kwanza ni hii theluthi ya Bajeti mzima kuwa ndiyo zimetengwa fedha kwa ajili ya fedha za maendeleo trillion 1 na bilioni 100. Sijui kuna Kanuni gani za kiuchumi ambazo zinasema lazima unapopanga mipango yako ya maendeleo moja ya tatu ndiyo iwe ya zile fedha zingine za uendeshaji. Kanakwamba haitoshi kati ya hizo theluthi moja ya Bajeti mzima asilimia 20 tu ndiyo mchango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zingine ni kusubiri wafadhili na hii inatukwamisha kwa sababu miaka ya fedha ya wafadhili pengine haifanani na mwaka wa fedha wa kwetu na matokeo yake ni wao kuleta fedha zimechelewa na miradi iliyokuwa imepangwa katika mwaka ule wa fedha kutotekelezwa.

Kwa hiyo, tunawaomba wanakuwa wanapanga mipango na wanaandaa Bajeti na Serikali ione kwamba kwa kweli tunakoendelea hatukumwondoa Mwingereza arudi kwa mwaka 61 ili hivi sasa tuwe tunamwomba fedha za maendeleo. Halafu sisi tuwe tunaweka asilimia 20. Kwa hiyo, tunaomba hilo waliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nilikuwa naangalia kwenye vyombo vyahabari watu wanachekelea na kushangilia kwamba Bajeti hii ya ukombozi ya kuondoa umaskini. Pengine mimi natofautiana nao. Wamezungumza, unajua wamefikia leseni hata kila mwaka, wamachinga watafaulu, watafaulu. Mimi sijawahi kuona machinga ana leseni. Na siyo tu kwamba machinga hana leseni na sijui hii timu ya machinga tunashangilia na kusherehekea machinga, machinga.

Sijui kuna utafiti gani Mheshimiwa Naibu Spika ambao umeonyesha kwamba baada ya miaka mitano ya kuwa na wamachinga, kila mwaka asilimia 50 ya machinga, basi wanahama kutoka kwenye umachinga, wanakwenda kwenye wafanya biashara wa

kati kuelekea wafanyabiashara wakubwa, *otherwise* tu machinga kila mwaka machinga tu, wanabeba maduka kwenye migongo yao. Kwa hiyo, hii ya kucheklea tu kwamba kwa kufuta hii imewasaidia wamachinga, haiwasaidii chochote na sisi ni kuwadanganya wamachinga ili waendelee kuwa wamachinga pale badala ya kutafuta suluhisho.

Bajeti hii Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu haiwasaidii. Mimi sijui nikiuliza inamsaidia nini Mwenyekiti wa Kitongoji, Bajeti hii inamsaidia nini Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji. Bajeti hii inamsaidia nini Mheshimiwa Diwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa Waheshimiwa Madiwani tunawadhulumu, wape na wao hamna. Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji anasimamia MMEM, anasomba matofali, mpe na yeze posho, mpe mshahara hamna! Mbona Katekista analipwa kwa kufanya kazi ya Mungu.

Sasa tufike mahala, inavyoelekeea watu wa kuchaguliwa wana matatizo, wanagombana na *Executive*, Afisa Mtendaji wa Kata huyo mpe, tena mpe na pikipiki. Diwani haa! Huyu usimpe. Sasa tufike mahali, hawa wengine wa Serikali za Mitaa, Serikali za Kijiji wanafanyakazi kubwa sana, pale Dar es Salaam Rais yuko pale, Mkuu wa Majeshi yupo pale, vyombo vyote vya usalama viro pale. Wizara ya Ulinzi na Usalama pale, kamkoa kadogo, majambazi kila siku wapo. Lakini ukienda kule kwetu vijijini jambazi akiguswa tu Mwenyekiti wa Kitongoji amekwishakumkamata Mwenyekiti na wanamshughulikia. Lakini wao kuwapa hata katuzo kamshahara hamna. Sasa tuanje kufikiria kwamba unapomwajiri Mwenyekiti wa Kitongoji halafu unamwambia mliviyotekeleza mlipokaa kwenye kikao hebu lete hapa Muhtasari, anauleta kwa hela zipi? Hiso karatasi atazinunua na nini? Kwa hiyo tunawaomba ninyi mnaopanga mhakikishe kwamba mnatafuta namna ya kuhakikisha kwamba na watu wengine hao mnawajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema Wenyeviti wa Vitongoji, kwa sababu walizowezwa hivyo kwamba wewe fanya tu kama punda, basi inaonekana ni kitu ambacho hakina neno.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko moja siwezi kuacha kulisema la mipango ya Serikali kuitia kilimo ili kuondoa umaskini. Nadhani hapa tunatofautiana katika msimamo. Mkulima mkubwa kama alivyosema Mheshimiwa Mzindakaya, mimi simsemei, nitawasemea wale wengine, kwa sababu yeze hajawahi kulima kwa jembe. Nadhani kwa sababu ya *exposure*, kwenye Serikali na uzoefu wake na kadhalika anapata mikopo. Kwa hiyo, wako watu wanatumika pale wanalima. Sasa mimi nawasemea wale wenzangu tunaolima kwa kajembe hivi. Imeelezwa kwamba mchango wa Sekta ya Kilimo katika uchumi kwa mwaka unaokwisha imeporomoka kutoka kati ya bilioni 440 kuja bilioni mia mbili na ishirini na kitu.

Sasa tafsiri yake ni nini. Tumekitekeleza kilimo ambacho tunasema sasa kwenye takwimu zote zilizopo hapa kwamba hiki kinaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania. Sasa *indication* ya kwamba watu hawa ni maskini kuliko walivyokuwa mwaka 80 na mwaka 90 mjue kwamba *export* yao imeonyesha nini, kwa sababu zile hela zinavyokuja

ndivyo zinavyo-speed over kwa watu hao wote kule vijijini. Halafu mtu anacheka anasema dhahabu unajua tumechukua ya bilioni 500. Sasa dhahabu mwenye kampuni kwanza hawazidi watu 50. Watumishi kwenye kampuni wala hawazidi watu 10,000. Lakini kilimo hiki ambacho umekwisha kuonyesha hapa kwamba zile hela zilizopatikana ndizo zimekwenda kule ni robo kabisa. Sasa huwezi kuondoa umaskini wakati ambao kila mmoja, kama ni wakulima kule Moshi kule wa kahawa, kama imeingia bilioni 1 kwenye mfuko wa watu wa kahawa kwa maana ya kuuza yao, ndizo hizo watakazogawana vinyumba vyote vile vyenye kutegemea kilimo. Lakini zingeingia bilioni 10 ndivyo hivyo wangeendelea kuwa na nyingi. Sasa kwa sababu walioko Serikalini wakiangalia utalii, mapato ya leo wakaangalia samaki wamechokonoa wakaangalia dhahabu, wanachekelea wanadhani kwa sababu wanaojilipa mshahara basi kilimo hata kikitupwa.

Na katika hili Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakuwa na mtizamo kama wa bundi. Unajua bundi ana macho makubwa sana. Sasa tatizo ni kwamba bundi wakati wa mchana hawezi kumwona tembo wala hawezi kumwona hata twiga pamoja na urefu wake. Lakini yeze wakati wa usiku kufuatana na mazingira anaona hata sisimizi, hata vyura, hata mijusi. (*Kicheko*)

Sasa kwa sababu tunakuwa kwenye *position*. Tumekaa kaa hapa Dar es Salaam, tunatunga Sera. Unatoa hela kwamba zitawasaidia wakulima. Tumefanya utafiti. Nakubaliana kuna utafiti wa aina na madhumuni mbalimbali. Nilikuwa Chuo Kikuu cha Sokoine, wanafanya utafiti wa mapanya yaweze kutegua mabomu, japokuwa hapa Tanzania hatuna mabomu. Lakini wanafanya pengine tutauza hayo mapanya na mtu mwingine anaweza kuchukua hela akafanya utafiti wa kutafiti jinsi ya kupandikiza mbegu za kiume za tembo kwa mbegu za kike za panya, yeze aone huyu mnyama atalinganaje. Kwa hiyo, haya ni malengo ya kila mmoja anapotoa hela za utafiti anataka nini. (*Kicheko*)

Ninachotaka kusema, tumepewa hela hapa kila siku tunafanya utafiti wa maharage, tunafanya utafiti wa kila aina. Sasa nikiwaliza hapa tufanyie tathmini, kuna tafiti ngapi zimefanyika katika vyuo vyote vya Kilimo na hayo mazao mmeyapeleka kule kila Mkoa kila Wilaya. Tathmini yake imesaidia kuongeza pato namna gani na kwa kiasi gani.

Lakini kuna vitu vingine ambavyo vinahitaji kufanyiwa utafiti kule kwamba utafiti tunaoutaka, tunataka kufanya utafiti wa soko na wenyewe ni utafiti. Ninyi kama mna ndizi pale Kilimanjaro, mnauza wapi, ni ndizi gani zinapatikana kwenda Dar es Salaam, wengine mnachoma nyama choma na ndizi za kuchoma. Soko lipo, ninyi mnazilishaje, ukizalisha hizo unaweza kupata soko hapa, unaweza ku-export China, huo nao ni utafiti. Huo nao hamuoni ya kwamba tunafanya utafiti, unapeleka huko hela sijui zimefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo huo pale Uganda, wanalima ndizi halafu wanatengeneza pombe ya rubisi kama kule kwetu. Sasa Rais Museveni akawaambia ahaa! Mnajua gongo tunasema ni haramu, lakini nina uhakika kabla ya Museveni

hajazaliwa, watu walikuwa wanakunywa gongo, kati ya 500 wanaokunywa gongo, 10 wanakuwa na ndiyo maana tunapiga marufuku. Lakini wanaendelea kunywa na wengine wanasomesha watoto kwa gongo hiyo hiyo.

Sasa akasema huwezi kwenda kufanya kwenye gongo hii, ili tuihalalishe tuache kuiharamisha lazima tufanye majaribio ya kisayansi, tutoe vile vijiini ambavyo ni *content* ambavyo vinaweza kuua watu, halafu baadaye tukishafanya hilo tukaona kwamba haiwezi kuua wanywaji, tunai-legalize watu wauze gongo yao halafu wanapata hela wanasomesha watoto, na wamefanya.

Sasa na sisi tufanye hivyo, haa! Tumefanya utafiti wa kuongeza mazao, sijui miche sijui ni vitu gani na vyote tumekwishafanya sasa tatizo lililopo ni kwamba kwa Watanzania hakuna linkage kati ya utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu sehemu fulani au Chuo cha Utafiti kuupeleka kwa wahusika *wa-manufacture* kile kitu kwa nguvu na wapeleke kwa Wazalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Mheshimiwa Waziri wa Kilimo sijui yupo, naona anaingia. Tumemfukuza Mwingereza, kwamba hakuleta maendeleo atoke ili tujitegemee. Sasa katika kilimo, mwaka uliopita na mwaka huu, njaa imetukaba, mimi siamini kama tumemfukuza Mwingereza ili twende kuomba chakula kule jangwani. Tumesomewa hapa asubuhi tulikwenda hata Ethiopia. Tanzania kwenda Ethiopia wamepigana miaka hii wanadundana, kwenda kuomba chakula. Tanzania, halafu wengine wanasema wakati wa njaa, tusali kwa Mungu. Yaani Mungu kwanza anabidi atuadhibu. (*Kicheko*)

Mungu ametupa akili, akatupa mito na maziwa, akatupa ardhi kubwa ambayo hatujailima. Sasa kama siyo kumchokoza, eti uende kwa Mungu unamwomba nini? Alikupa akili, akakupa na maji na mito yote. Kama siyo kumchokoza halafu unakwenda Jangwani, Misri kuomba chakula. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahali tukubaliane, tunayafanya haya kwa sababu hakuna tunayemwogopa. Tunayafanya haya kwa sababu hakuna tunayeshindana naye. Wamarekani ukiwaliza wakashindana na Wachina, sasa sisi tunashindana na Taifa gani? Hivi hatufanyi hilo kwa sababu hakuna mtu wa kutuadhibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya hivyo kwa sababu hakuna mtu wa kutuadhibu. Tumeletewa hela, wapeni wakulima hela za *STABEX*. Mheshimiwa Waziri akalidanganya Bunge kwamba ahaa! Tukiwapa watakwenda kunywa kitochi, ipo kwenye *Hansard*. Hata watu wa Kilimanjaro kwa kweli na wao wamesomesha watu mpaka wakubwa wote mnaoa huko mnawapa hela wanakunywa vitochi hawa? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakasema hela hizo tutakwenda kutengeneza barabara. Karagwe inazalisha nusu ya kahawa yote ya *Robuster* na kama kuna mtu ana takwimu tofauti, akuambie Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitakaa chini yeche aendeleee.

Sasa barabara mliotupa ni ipi? Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Karagwe hatukuomba chakula kutoka Serikalini na kwa miaka 30 hatujawahi kuomba. Na imenyesha mvua mwezi wa nane mwaka jana, imeharibu barabara zote na Serikali ikakaa pale ikasema tutawapa hela hizi ambazo mtakwenda kunywa pombe. Mimi sielewi kama unakunywa pombe, mfike hapa mtengeneze barabara hata moja hamna. Na wengine wamesema huko wanaotoka maeneo yanayolima kahawa, wanasema tutaendeleza kila Wilaya zao moja la chakula na biashara. Zao moja lipi?

Mimi nimekwenda kwa Mheshimiwa Profesa Mwандосya, wanalima chai, wanalima ndizi, wanalima mahindi, wanalima kahawa. Hivi kama hutaki kuwadhulumu, unataka walime zao moja lipi? (*Kicheko/Makofi*)

Mimi nadhani Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya kudhulumu ni kudhulumu na kudhulumu ni kutokumpa mtu anachostahili. Pale Karagwe tuna kiwanda cha kukoboa kahawa, kimenunuliwa na *KCU* tangu mwaka 66. Mheshimiwa Waziri akaeleza kwamba hatuwapi hela tutapeleka kwenye viwanda. Sasa tuna kiwanda, nataka Mheshimiwa Waziri wakati mna-*wind up* mniambie hapa. Sisi tunajenga kiwanda pale cha kukoboa kahawa cha Chama cha Ushirika, mmewapa shilingi ngapi?

Sasa hii tabia ya kuwanyonya watu eti kwa kuwa wao ni wa kuliwa. Sasa hawa wa kuliwa sijui wakulima siyo wakulima, wao ndiyo hao hao miaka yote arobaini mkulima huwezi kumkuta amenunua shangingi, labda akinunua mjue anayelima kwa matrekta ambaye labda pengine alikuwa Waziri au ana cheo hivi amekaa karibu na mabenki. Mkulima na kajembe kake anunue shangingi tuone. Halafu tumekaa hapo ndiyo hao wanaotupa kura kila siku sasa sijui inakuwaje.

Lakini mimi tufike mahala Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema humu Bungeni, hizo takwimu mimi naomba, Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unajibu, tunaomba na hela za utafiti mzielekeze kule, mwende inkafanye utafiti wa masoko, mnafanyaje, muwaulize watu kwamba ninyi Kyela hapa mna matatizo gani. Ninyi hapa Bunda mna matatizo gani? Ninyi hapa Rombo mna matatizo gani? Ninyi Kagera hapa mna matatizo gani mnazalisha nini? Waulize halafu *then* wakupe *framework* ya utafiti wanaotaka kufanya, uwasakiidie ufuatane na matashi yao.

Lakini hii ya kupeleka hela huko eti sijui mmepeleka kwenye *Institute* wanatafiti nini? Sijui Lyamungu, sijui ngano, sijui maharage, sijui pamba, yote yamerundikana kule na ule utafiti haufikishwi kule. Na ukitaka kupima utafiti na thamani yake haiko.

Baada ya kuyasema hayo, nadhani sasa Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba hao wanaonilazimisha kuunga mkono sijui kuna Kanuni inanilazimisha hivyo mimi sielewi. Lakini nadhani nikipata majibu baadaye nitaambua cha kufanya. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema jioni hii ya leo. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumwomba Mwenyezi Mungu amsaidie Mheshimiwa

Rais ambaye yupo kwenye matibabu na wote tunafahamu kwamba mara nyingi tunapokuwa kwenye *Budget Session* huwa tunamwona kwenye maeneo ya Dodoma. Lakini tunaomba basi afikishiwe salaam zetu na Mwenyezi Mungu amsaidie ili apone haraka. (*Makofit*)

La pili naomba vile vile nitumie nafasi kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba na kwa kweli tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake pema Peponi.

Mwisho kabla sijachangia Bajeti, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wake kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki na niseme tu kwamba hiyo inatokana na imani ya wananchi kutokana na kazi yake aliyokuwa anafanya lakini vile vile ni kwa sababu ya sera nzuri. Sasa uko mahali ambapo ndiko kwenye sera zenyewe. Kwa hiyo, karibu sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie vile vile nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Waziri wa Fedha kwa Bajeti zao. Kwa kweli Bajeti ni nzuri imeendelea kuonyesha kwamba tunapunguza utegemezi hilo ni jambo zuri na vile vile uchumi unakua licha ya matatizo ya ukame. Kwa hiyo, kwa kweli tunawapongeza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatumia muda wangu karibu wote kuzungumzia juu ya eneo moja ambalo nadhani mimi naona halijagusiwa sana. Eneo la huduma za jamii. Katika eneo hilo tumeona mengi tumeona sasa kwenye eneo la elimu kuna ongezeko kubwa la maendeleo katika Sekta hii. Idadi ya wanafunzi inaongezeka, madarasa yanajengwa, nyumba za walimu zinajengwa. Idadi ya walimu inaongezeka. Viwango vya kufauli vile vile vinaongezeka.

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tukubaliane kwamba mafanikio haya hayawezi kabisa kulindwa kama hatutaondoa kero kubwa ya walimu na hasa madai yao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo, ningependa kusema kwamba tangu mwaka 1995 mpaka karibu 1998 walimu wamekuwa wakidai sana malimbikizo ya mishahara yao ya posho za uhamisho, ya likizo, ya matibabu, ya usafiri na posho ya kujikimu. Tangu 1995 mpaka 1998. Ilipofika 1998, madai kulingana na takwimu ya Chama ya Walimu yalifikia milioni 8. Lakini Serikali katika mwaka 1999 Serikali ilichukua jukumu la kuhakiki hayo madeni na baadaye iliweza kulipa karibu bilioni 4 kwa mwaka 1999 mpaka 2001.

Sasa baada ya hapo tulitazamia kwamba walimu hawatakuwa tena na madai yao. Lakini hivi ninavyozungumza takwimu ya chama cha Walimu inaonyesha kwamba walimu wanadai karibu bilioni 18 na wakati ule Serikali iliunda Timu ya kuhakiki haya madeni na bado ikatumia miaka karibu mitatu kuyalipa. Sasa tumerudi kule kule. Sasa ongezeko la shule la nyumba haitasaidia hata kidogo kama hatutaondoa madai ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya mishahara, si jambo linalohitaji kuhakikiwa kwa muda mrefu sana. Kwa sababu mishahara ya walimu inajulikana. Una sababu gani ya kulimbikiza, kama wamepanda madaraja au mapunjo yao, ni wewe ndiye unayejua Serikali. Sasa unataka tena uhakiki kwa kupitia wapi? Haya yanatakiwa yalipwe tu. Na takwimu zinaonyesha zaidi ya karibu bilioni 4 ndiyo wanayodai kwenye eneo hilo.

Takwimu zinaweza zikatofautiana kutokana na maeneo yanayohakikiwa lakini ninachosema hoja kubwa hapo ni malimbikizo ya mshahara. Halafu ajira mpya ya walimu. Serikali ndiyo mnatoa ajira mpya ya walimu. Halafu tunasikiaje kwamba walimu wanateseka sana hawapati mshahara, wanaajiriwa wanakaa muda mrefu mpaka mishahara walipwe inachukua zaidi ya miezi mingi kidogo. Halafu bado wakipata ule mshahara wa kwanza yale malimbikizo ya nyuma yanawekwa kama deni. Hii maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya kazi ya aina gani? Utendaji wa aina gani huu. Sasa lazima turekebishe hili. Uhamisho wa walimu. Taarifa za uhamisho ndiyo anayo mwajiri na ndiyo Serikali. Sasa kwenye uhamisho kama huna fedha za kumlipa hivi kwa nini unamhamisha? Eneo hili linaonekana kwamba kulingana na taarifa za Chama cha Walimu karibu bilioni 6.4 mpaka sasa.

Kwa jumla maeneo haya ya malimbikizo ya mshahara, ajira ya walimu na uhamisho yanahitaji karibu bilioni 2.2 hayahitaji kukaa muda mrefu, Serikali kumaliza madeni haya. Na hakuna sababu hata kidogo. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha umetamka kwenye kauli yako ukurasa wa 39 nikianza kwenye ukurasa 37 pale uliposema mgao wa fedha kwa mwaka 2004/2005 izingatie mambo yafuatayo:-

Katika jambo la saba ukurasa wa 38 umeeleza kwamba Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha mishahara ya watumishi wake, lakini ukasema Serikali inaandaa utaratibu maalum wa kushughulikia kwa haraka malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Serikali wakiwemo walimu. Na ulisema kwamba malimbikizo yalisimamishwa kutokana na wizi uliofanywa na wizi wa kalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo la wizi wa kalamu sasa ni kubwa. Na kwa sababu ni kubwa hasa kwenye eneo hili la walimu, mimi ninashukuru Kamati ya Huduma za Jamii imeunda Kamati Ndogo ya kushughulikia jambo hili lakini vile vile nataka kuomba Kamati ya *LAAC* ambayo ndiyo inakagua mahesabu ya Halmashauri za Wilaya nayo ichukie jambo hili na bahati nzuri Mwenyekiti wake yupo hapa, Mheshimiwa Msindai.

Ningependa na yeze aseme juu ya eneo hili tunataka jambo hili liishe. Hakuna sababu ya kutesa walimu. Walimu wanapata mishahara nayo yenyewe siyo mikubwa. Ni midogo na huku tunataka kulinda haya mafanikio yanayopatikana ya MMEM na MES tutalinda vipi? Madai tu tunashindwa kulipa haya malimbikizo, sababu zake ni nini.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa kabisa. Waziri wa Fedha inawezekana akawa ametoa fedha kwenye Halmashauri za Wilaya.

Lakini kule fedha zinaweza zikatumbukizwa kwenye mfuko unaitwa Mfuko Mkoo ambao kwa vyo vyote vile umetoboka kila mahali. Maana cheki yoyote itakayoingia kule itasomba fedha yoyote ambayo itakuwa kule. Na kama kweli fedha za walimu zinatumbukizwa kwenye Mfuko Mkoo ni kosa kubwa sana linalofanywa. Kwa sababu kuna *account* maalum ya kuweka fedha hizi za walimu.

Sasa tunashangaa kwamba Serikali inashindwaje kufuatilia jambo hili. Hatukupata mafunzo kutoka ile mwaka 1995 mpaka 1998 ambapo madeni haya yalikuwa yalisafikia kiwango kikubwa mpaka leo tena baada ya hapo tena tumelimbikiza hii. Hivi utendaji wa Serikali unakwama katikati au unapaswa kuendelea vizuri.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la kutumia vibaya fedha zinazokwenda kwenye Sekta ya Walimu sasa ni kubwa na hasa hili la eneo la mishahara ya walimu na malimbikizo yao. Katika eneo moja unaweza ukakuta kwamba *OC* inayopelekwa Wilayani kwenye Halmashauri ya Wilaya, Ofisi ya *DO* inaweza kuwa na watumishi wachache sana lakini inaweza kutumia mpaka zaidi ya milioni mia moja na ambazo zinapelekwa pale lakini walimu pale wakapewa milioni 2 na ambao ndiyo wengi zaidi.

Jambo hili kwa nini Serikali haitaki kuliangalia. Kwa nini tunapeleka tu fedha lakini hatujui fedha hizi zinakwenda kufanya nini kule. Naomba niishie hapo hili ni jambo ambalo kwa kweli wote na mimi naomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu bado Wizara zenye ndio zinakuja, kila mtu alizungumzie tatizo hili la malimbikizo ya walimu mpaka tumalize jambo hili. Tusiendelee kuliachia hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilitaka kusema katika eneo la huduma za jamii ni Mfuko wa Elimu. Tulianzisha hapa mfuko wa elimu kwa Sheria Na. 8 ya mwaka 2001 na ikaundwa mamlaka ya kusimamia mfuko wa elimu. Tuliunda Mamlaka, Mamlaka ya Elimu Tanzania. Kwa kifungu cha 13 (a) cha Sheria hiyo Na. 8 kama nina kumbukumbu vizuri.

Katika eneo hilo ilipangwa kabisa kisheria pale kwamba fungu la Bajeti ya Serikali kwenda kwenye mfuko huu itengwe kiasi kisichozidi asilimia 2 ya pato la Taifa baada ya kuondoa kinachohitajika kulipia madeni ya Taifa. Sasa hali ikoje kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2001/2002 ambapo 2002 ndipo mfuko ulipoanzishwa, Serikali ilitoa bilioni 5.2. Hii ni sawa na asilimia 0.5. Tulikubaliana walau isizidi asilimia 2 ya pato la Taifa baada ya kuondoa madeni. Lakini Serikali ikatoa asilimia 0.5 mwaka 2002/2003 Serikali ilitoa karibu bilioni 4.9 ambayo ilikuwa sawa na asilimia 0.4 inazidi kwenda chini, 2003/2004 kiasi ambacho kilitolewa kilizidi kuteremka na kufikia asilimia 0.36.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda wapi? Tumekubaliana tufikishe pale. Hili nimeona kuna tatizo linalojionyesha kwamba kuna tatizo hapa la upungufu wa kisheria labda kwamba Serikali hailazimiki kutamka kiwango cha chini kwa kuwa kwenye Sheria tulishasema kiwango cha juu. Kwa hiyo, inaweza kufika mahali huu mfuko ukapewa hata sefuri.

Kwa hiyo, Serikali inaweza ikaamua kuufikisha hapo mfuko ukawa sifuri. Maana unatoka 1.05 hata moja msifike? Mnakuja 0.4, 0.36, maana yake nini.

Tunaomba kabisa kama eneo hili linahitaji marekebisho ya Sheria, Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria iletwe ya kurekebisha ili Serikali iweze kutamka kiwango cha chini na tuweke kabisa kwenye Sheria, tujue kabisa inalazimika kuweka kiwango hicho. Na ninasema hivyo kwa sababu mfuko huu ndiyo unaosaidia mambo mengi sana kutoka elimu ya chini mpaka elimu ya juu kwa mwaka jana tu ilitoa karibu bilioni 4.8 kwa ajili ya vyuo vikuu na taasisi mbali mbali na ndiyo uliodhamini hata Madaktari na ndiyo unaodhamini hata wale vijana 603 amba Wizara za Serikali hazikuweza kudhamini.

Huu mfuko ndiyo unaosaidia na huu mfuko ndiyo unaosaidia watoto wasio na uwezo. Sasa tunaomba Serikali itumie nafasi hii vile vile kuhakikisha kwamba kiwango cha chini kinajulikana na Serikali iendelee kuhamasisha mashirika kama *TBL*, *CELTEL*, *VODACOM*, *TTCL*, mabenki na mengine. Tunajua haya yanadhamini michezo na mambo mengine. (*Makofi*)

Sasa kama tunaweza tukadhamini mambo ya michezo na unenguaji na mambo haya kwenye michezo kwa kiwango hiki kwa nini tusidhamini elimu? Tudhamini elimu. Hapa naipongeza *VODACOM* kwamba imedhamini karibu wanafunzi watano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walau. (*Makofi*)

Na *City Bank* walau imeshiriki katika ujenzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Bugando. Tuelekeze haya mashirika yetu na makampuni yetu huko. Kwa hiyo, nilitaka kusema hilo.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema kwamba kwenye Sera ya Sayansi na Teknolojia tumekubaliana mwaka wa 1996 wazo la kutenga asilimia moja ya pato la Taifa, kwa taasisi mbalimbali kwa ajili ya utafiti. Lakini hali bado haionyeshi kwamba jambo hili lipo. Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu iko kwenye shilingi milioni mia tatu sijui sasa Wizara zingine hali ikoje? Tungependa kujua jambo hililifanyiwe utafiti kwenye Wizara zingine, eneo la utafiti linapewa fedha kiasi gani kwa sababu kama tunataka kwenda kwenye sayansi na teknolojia, lazima tuzungumze habari ya maarifa ya sayansi na teknolojia. Tufikie hapo kwenye hilo pato iwe asilimia moja ambayo tulikubaliana huko nyuma kwenye sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme la mwisho kwenye Wizara ya Afya. Liko tatizo Wizara ya Afya inadaiwa karibu shilingi bilioni 11 na Bohari ya Madawa(*MSD*). Jambo hili linasababisha upungufu wa madawa kwenye hospitali zetu, nina hakika Wizara ya Fedha ndiyo inapaswa kuhakikisha kwamba Wizara ya Afya ina fedha hizi.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha utuambie kama fedha hizi uliwapa wakatumia vibaya Wizara ya Afya au bado ziko kwako na kama ziko kwako utuambie unakaa nazo za nini. Na huku dawa hakuna. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ninayo mengi lakini nadhani haya yanatosha isipokuwa niseme moja, Serikali inapotaka kupunguza matumizi kutokana na ukame isiguse zile sehemu ambazo ni nyeti. Punguzeni sehemu hizi za matumizi ya *OC*, kwenye Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, mmeondoa shilingi mia 770 kwa nini msiondoe huku kwenye makasma haya ya Semina, Starehe, *Hospitality*. Ndiyo mngeondoa huko. Lakini unakwenda kupunguza eneo ambalo ndiyo eneo muhimu kabisa kwa ajili ya maendeleo.

Ndio vile vile imepunguzwa kwenye Sayansi karibu bilioni 1.8 lakini kwanza fedha yenyewe ya Maendeleo ilikuwa bilioni 2.1 tu ukiondoa 700,000 umebakiza nini na hii ndio ilikuwa fedha muhimu kwenye maendeleo kwa ajili ya Vyuo vyetu Vikuu lakini mkaziondoa. Kwa hiyo, nashauri ikitokea dhararu na nini ondoeni yale maeneo ambayo si lazima sana Wizara zinaweza kukaa bila *OC* kwa muda fulani kama tatizo kweli ni kubwa sana lakini wakati wa upungufu wa chakula wote tuliona semina zilikuwa zinaendelea kila kitu kilikuwa kinaendelea, *business as usual*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nami napenda kumpa pole sana Mheshimiwa Dr. Kigoda na dada yetu Asha Kigoda kwa kumpoteza mzazi wao, baba yao, bila shaka Mungu atawafariji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze sana wote tuliowachagua kwenye Bunge la Afrika na napenda sana nimpongeze Mama Mongella kwa sababu ametuletea heshima kubwa sana kwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana sana kummpongeza rafiki yangu Danhi Makanga kwa kurudi tena Bungeni na hivyo kudhihirisha wazi kwamba wananchi wakimpenda mtu hata akiwa Chama chochote watamchagua sasa amerudi CCM na amechaguliwa. Kwangu ni faraja kwa sababu Danhi Makanga tulikuwa naye kwenye Tume ya Bunge bahati mbaya sasa uko Chama chetu Tawala ilibidi nafasi yako ichukuliwe na upande wa Upinzani lakini karibu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Kigoda na Mheshimiwa Waziri Mramba pamoja na Wasaidizi wao kwa Bajeti nzuri ambayo wameileta hapa Bungeni. Ni Bajeti nzuri kwa sababu imemtazama sana mkulima mdogo, mfanyabiashara mdogo na hao ndio wadau wetu na sisi ni wadau wao. Kama Wabunge, ukimtzama mkulima mdogo na mfanyabiashara mdogo kwa kumpunguzia vikwazo vingi, tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachojuwa ni kwamba Bajeti ni nzuri, aliyeleta Bajeti ameleta Bajeti nzuri, tatizo ni jinsi itakavyosimamiwa na kutekelezwa ukilaumu tu kwa kweli utakuwa unakosea suala ni jinsi gani fedha hizi zitakavyokusanywa na zitakavyotumika. Kama zisiposimamiwa vizuri katika mapato na matumizi Bajeti yote itaonekana ni kazi bure tu. Kwa hiyo, ni vema sasa watu wajipange na siku zote mimi nasema *sense of seriousness*, watu kuwajibika sana ni kazi ngumu sana, watu kujali shughuli waliyopewa ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika nchi yetu tunapata mapato kutokana na kilimo lakini kila mmoja anayeongea juu ya kilimo anaonyesha wazi bado kilimo ni duni. Bado hatujaffika popote na tunajua kwamba kilimo ndio haswa uti wa mgongo na hatuna njia nyiningine ya kukusanya mapato yetu isipokuwa kwenye kilimo lakini bado kilimo kiko chini sana hatujafanya mapinduzi. Tumeimba wimbo huu wa milele na milele kilimo bado, kilimo bado, kilimo bado sasa tunatakiwa tukae tuweke mikakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesikia sijui ni mtu alikuwa anajibu swali hapa akasema katika vyakula tulivyoletewa na Ethiopia walituletea, sikusikia sawasawa sijui kama ni sawasawa? (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Sawa.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Sasa Ethiopia wanatuletea chakula sisi? Kweli kabisa watu wote mnaifahamu Ethiopia, hakuna mtu asiyeifahamu Ethiopia katika nchi hii leo wewe unaletewa chakula kutoka Ethiopia! Watu wale ni wanyonge kabisa ukiangalia kwenye *TV*, maisha yao ni ya ajabu sana mpaka utawaonea huruma leo wanakuja kutulisha sisi Watanzania! Mimi nilishangaa sana lakini nikasema labda masikio yangu hayasikii sawasawa ila mnavyoniambia ni kweli basi ni balaa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo hiki cha kutumia jembe la mkono hakiwezi kuinua uchumi. Mheshimiwa Mzindikaya leo asubuhi amesema sana na wengine wamesema sana juu ya kilimo lakini kwa nini siku moja tusikae tuamue kabisa tunayatumiaje mabonde hata Ndugu Ndeka alisema sana, haya mabonde tunayatumiaje? Tunacheza tu ngoma ya zeze kwa sababu hatujaamua tunataka iwe hivi na isimamiwe hivi lakini tunaongea lugha nzuri tu. Mtu mmoja alisema kama ni sera, mipango mizuri, kama ni papers nzuri nenda Tanzania, ukienda kwenye makabati yetu sera, mipango, aah kwa kweli *we are leading* katika Afrika lakini bado nchi hii tunategemea watu watulishe na Ethiopia iwe ni mojawapo katika kutulisha, inatisha sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaweza kupata mapato mambo mengi kutoka kwenye utalii lakini sasa tunafanya nini na utalii huu? Tunatunzaje mazingira yetu, misitu na wanyama tunawalinda namna gani mambo yanayoendelea huko ni ya ajabu. Mimi nashangaa sana siku nyiningine nikitembea hapo Dar es Salaam sehemu za Kizuiani kule nakuta malori makubwa sana yamebeba magogo makubwa sana yanatoka Kusini. Hivi haya magogo yanatoka wapi, kwanza magogo yenyewe yanakwenda wapi, nani ameruhusu magogo yale yakatwe kwa kiasi kile, halafu huko kweli miti itabakia,

inatosha. Lakini hakuna mtu anayejali tunatazama hivi kwamba eeh ndio wanakata hivyo, ndio wanakata hivyo, yale magogo ni misitu na ni makubwa, kutoka Kusini Mikoa ya Lindi, Mtwara nafikiri na Ruvuma, hakuna mtu anayewasimamisha, *sense of seriousness*. Sasa sijui hiyo ni biashara lakini kama ndio biashara yenewe basi tungetafuta biashara nyingine kwa kweli suala la miti tungeliweka kando kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilisema pamoja na kuvuna msitu ule wa Mufindi lakini wenyewe ulikuwa ni kivutio watu kupita mle lakini ukavurugwa katwa katwa mpaka barabarani, tukapiga kelele hapa wakasema lakini wanapanda ukienda kuangalia vingine vimejiotea vyenyewe hakuna utunzaji wowote na ule ni utalii tu wa kutumia mandhari. Mwalimu wangu Makwetta alishasema hata kutumia *Geography* ni utalii wa ajabu sana, nchi nyingine hazina kitu kingine ni *Geography* tu unakwenda kuangalia maajabu, wanyama, misitu lakini speed ya ukataji wa miti ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishasema ukataji wa mkaa sasa umekuwa ndio ushirika kuna Vyama vya Ushirika watu wana vikundi wana magunia kadhaa kama 50, 60 na wamechora picha za watu wamefunga vitambaa wanaonyesha mkaa uko kule halafu basi tunapita, hii ni hatari. Ukienda mahali pengine unakuta magunia 200, 300 mpaka 500 sasa hiki si Chama sio cha Msingi tena ni *Union* ya mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulipiga hesabu na jamaa mmoja gunia moja Sh.6000, 7000 watu wamehamia kufanya biashara hiyo. Ukienda kuchukua magunia 100 ukununua kwa Sh.2000 kule wanakochukua ukauza Sh.7000 mara magunia hayo upige *trip* ya 1,2,3,4 kwa nini ufanye kazi nyingine? Sasa imeshakuwa ni *business* sio tena matumizi ya kawaida yote haya tunasema tunaonekana tuna mdomo, ni watu wabaya tunalaumu sana, basi hiyo ni nchi yetu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatuwezi kukusanya kwenye kilimo tutakusanya kwenye madini lakini sasa madini yenewe ndio haya yana mgogoro usiokuwa na mwisho. Nilishasema hapa na nikaleta *terminology* inayoitwa ‘Mupetee’. Mupetee kwetu ni kango ambako watoto ambao hawana nguo, watupu kabisa wanapewa katika maeneo maskini. Kwa hiyo, anakafunga kwenye kamba hasa kuficha eneo maalum, nyeti, kananing’inia hakawezi kuwa zaidi ya upana huu kanafungwa hapa, kuficha huku na inakuwa na sikuu maalum kwa watoto waliopata Mupetee kuruka kusema sikontela, nsimayapya, sikondela, simayapya na ugali uko tayari vijana wanaruka. Siku ile nilisema kwa sababu hakajakaza sawasawa kwa hiyo hakana hata formula kana kaa wapi inawezakuwa ile furaha ya kuruka kupata kale kango unakuta kako huku kwa hiyo huku kumebaki wazi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema ile 3% ni Mupetee tu.

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Kweli kabisa kama tunategemea kupata mapato yetu kutoka kwenye madini huwezi kuwa na huruma ya watu wachukue 97% sisi tuchukue Mupetee kabisa kale kadogo 3%. Hiyo ndio rasilimali uliyonayo wewe ambapo

lazima uzalishe kutoka hapo lakini tumekakamata hako tumecheza nako tumepata barabara na shule wamejenga hako ni Kamupetee tu wao wanapeleka nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ndicho kitu tulichonacho, ndicho Mungu ametujalia. Mungu ni wa ajabu sana kule jangwani amewecka mafuta, kule jangwani amevusha mto Nile hawanyimi waja wake sisi huku amewecka madini lakini ndio hiyo tena Kamupetee tunapata hako.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali sasa hivi nadhani kuna Tume au kuna kitu fulani kinapita kuchunguza madini yetu tuyatumie namna gani au tufanye mikataba namna gani. Kama hilo linafanyika, naipongeza Serikali kwamba lazima ifike mahali tufanye kitu cha maana haya madini hayawezi kwenda hivi hivi. Hawezi mtu kuwa anahamisha *Tanzanite* anapeleka huko, anahamisha anapeleka huko sisi hata kama ni huruma Mungu atakuja kusema lakini ninyi ni watu wa ajabu sana niliwapa hiki hamkutumia, niliwapa hiki hamkutumia mljidai ni watu wema. Nilishaongea juu ya habari ya kwamba wachimbe bure au sijui wafanye biashara bure mnaita *Tax Holiday* halafu mtu akifanya kazi ikibaki mmoja, miwili aingie kwenye malipo anabadilisha biashara anaingia kwenye biashara nyingine, halafu tena anabadilisha, haiwezekani kwa watu wasomi kama Tanzania tufanye mchezo kama huu, haiwezekani kabisa. Madini yetu ndio haya tunapata nini ni hiyo Mupetee tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu vingine ukiangalia unasema sijui nitaonekana namna gani lakini tukizungumza wengine tunachukiwa au unaambiwa wewe unakosoa sana. Hii ni nchi yetu inawezekana wewe hujaona lakini wenzako wanaona ndio maana vichwa viko vingi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kweli bahati mbaya hujaona sawasawa lakini mwingine hata mtoto mdogo akasema. Kuna hadithi ambayo mtoto ndio alisema lakini yule wanayembeba yule ingawa wanamshangilia sana yule wanasema kwamba amevaa lakini mimi naona yuko uchi tu. Mtoto mdogo ndio aliyesema wengine wote walisema amevaa tu maana imesemwa kwamba kama humuoni una dhambi sasa kila mmoja anataka asionekane ana dhambi. Kwa hiyo, akisema amevaa anasema amevaa vizuri sana lakini moyoni anasema lakini nadhani yuko uchi tu mtoto mdogo anasema yule amekaa utupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi wengine kwa sababu tuko wengi hapa tunashauriana tunafanya nini na kilimo chetu ili tusipate chakula kutoka Ethiopia, tunafanya nini na utalii wetu ili kusudi mazingira yetu yaweze kutusaidia, tunafanya nini na madini yetu ili kusudi mtu asiwe anachukua tu jamani. Sisi tumekusanyika hapa kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri vichwa vyote visaidiane na Serikali yetu pasiwe na kusema huyu anajua zaidi, huyu hajui huyu ni mbishi tu huyu hafai hapana vichwa vyote ni mali ya wananchi hapa tusaidiane. Tunafanya nini magogo yanayokwenda tu hivi hakuna mtu anayezungumza, tunafanya nini na biashara mbovu inayofanywa na watu mbalimbali?

Siku moja tumekwenda mahali kuna kiwanda kinaitwa *Sisal* Kamba palikuwa na jengo kubwa sana tumemuuzia mfanyabiashara mmoja pale tumekwenda kukagua tumekuta ni uwanja wa *netball* kwa sababu amekusanya vitu vyote *machinery* yote, niliwaambia tu wale wenzangu hapa undeni timu ya *netball*. Tukauliza kwa nini amekusanya na kulipa hajalipa wanasema ooh, Simpasa unataka kuishi wewe, usimguse huyu *Jesus Christ, in the name of Jesus*, watu wananiambia acha kama unataka kuishi usimguse huyo. Ameuziwa na Serikali kupitia *LART* ameamua kung'oa *machinery* yote na hajalipa na hakuna kusema ukisema wanasema wewe wameshatangulia wangapi, chunga sana usimseme huyo wote kimya, kwa jina la Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami pia napenda niwape pole Ndugu zetu Mheshimiwa Dr. Kigoda na dada yake kwa kufiwa na mzee wetu na tunaomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

WABUNGE FULANI: *Amin.*

MHE. EDSON M. HALINGA: Pia tunampongeza Danhi Makanga, Danhi Makanga alikuwa mtoto mpotevu sasa amerudi zizini lazima tusherehekee. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tunalo tatizo wenzangu wanalisema lakini nadhani tunalo tatizo ama la kuzaliwa nalo au ni balaa iliyotuangukia. Waziri wa Fedha amesema tumepata *inflation* kwa sababu uagizaji wa bidhaa kutoka nje umezidi. Kuagiza mchele, mahindi, madodoki haya ya kuogea, hivi tuna matatizo gani? Hata tungechana magunia haya tunapooga tungejisugulia leo mpaka tuagize madodoki ya Uchina na Korea? Hivi sisi watu tunafikiri juu ya uchumi wetu kweli au tuna matatizo gani? Tutumie fedha yetu ya nje badala ya kuleta vitu vya kutusaidia tuagize viatu, kandambili na nguo za ndani, hivi tuna matatizo gani? Kwa kweli tunalo tatizo tusipoliangalia ndugu zangu nchi hii *tuta-perish* kama tunavyoona hivi hivi na ni vema tufe tunaangalia kama samaki. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili matumizi yetu ni ya ovyo, nitatoa mfano. Wizara ya Mipango ya Mheshimiwa Kigoda ina Kitengo kile cha Tija. Kile Kitengo sisi tumeitisha hata hesabu za mwaka jana hakuna lakini mwaka huu kimepangiwa kipate fedha, hivi kweli hawaoni? Wapewe fedha wafanyie nini za mwaka jana hazieleweki tunawapa nyingine tena hivi kweli tuna mawazo sawasawa ya kujali uchumi wetu? Hivi tunadhani mambo haya ya maendeleo yatakuja kiajabu ajabu tu hata mto hautiririki hovyo hovyo. Ukitiririka hovyo maji yatakwisha unakauka kwa hiyo kukauka huku matumizi yetu ni mabaya. Naomba Kitengo hicho cha Tija kiondolewe katika mgao wa fedha ya mwaka huu maana hakina faida yoyote au iwekeni iwe ndio Tume ya Mipango. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 18 wa kitabu cha Waziri anaeleza kwamba hali imekuwa mbaya kwa sababu wale Wakurugenzi hawakuwasilisha malipo ya watumishi ya *PPF* kwa hiyo Serikali ifidie, iwalipe wale watumishi ambao fedha zao hazikuwakilishwa kule *PPF*. Wale watu wamelipwa haki zao zote na Serikali hii tena tuwalipie kwa wale wengine ambao hela zao hazikwenda kule hivi kweli tuna mawazo sawasawa na Hazina yetu halafu tunasema hela haziko, hela ziko ila tunashindwa kudhibiti matumizi yake. Hata ningekuwa mimi kama ninaweza kula hela halafu wengine mkalipa kwa nini niziache? Yaani nchi hii tumejenga tabia ambayo haiko katika dunia hii ila ni dunia ya mashetani tu ya kudhulumu tu basi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane wale wanaotumia hela ovyo za nchi hii wafilisiwe. Wako watu wamejenga majumba hapa, wako watu wamenunua magari hapa kwa fedha za nchi hii lakini wanatazamwa tu, wanaachiwa wanakwenda wanatamba hii ni dhuluma mbaya katika nchi yetu na haiwezi kutusaidia kwenda popote. Watu wanasema tuzalishe zaidi nani azalishe zaidi? Tulikuwa na Sheria ya Nguvu Kazi imefutwa hivi utambanaje mtu azalishe katika nini? Watu wamejinyamazia sasa wanabaki kulala barabarani kuwa wapiga debe, utawafanya nini, huna sheria, hakuna anayefanya kazi. Tunabaki maneno tu tuzalishe, tuongeze, tuwajibike tutawajibika katika nini wakati sheria hakuna? Utamwadhibu mtu asiyefanya kazi kwa njia ipi? Machinga watazidi sasa sio Machinga wa kule Kusini ni kampuni nzima ya Tanzania ndio Wamachinga wa nchi hii, wote tuko mle. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wahasibu wapo lakini hela zinatumika hovyo. Gazeti la Rai la tarehe 2/6/2004 limeeleza kwamba Redio Tanzania ilipewa fedha inunue vifaa. Vifaa vilivyopatikana na ambavyo vilitosheleza ni vya Sh.79 milioni lakini zimechukuliwa kwa *ku-over invoice* shilingi milioni 266, hapa hapa Dar es Salaam na Kamishna wa *Central Tender Board* yuko hapa hapa Wizara ya Fedha, hakuona? Hivi huyu anafanya nini kama si kumfukuza akafilie mbali huko? Tunaweka watu wa kudhulumu tu waondoke hawa. Hatujengi tabia na taratibu za asili yetu hata kidogo ila tunaweza matabaka ya watu wenye kudhulumu tu hivi kuna maana gani ya kuwa na *Tender Board* hapa Dar es Salaam hapa hapa *Radio Tanzania* tu hela zinaliwa wanatazama hivi hivi, tunafanya nini? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka watu wa kukagua sijui almasi huko Uingereza watu wanakula hakuna anayeshughulika. Leo tunasema hatuna hizi hela nani awaletee? Hata fisi hangoji aletewe anatafuta hata mifupa ya kale anaitafuta sisi tunaachia watu wanakula tu halafu tunasema nchi hii maskini, maskini wapi? Hela zilizopangwa kwenye Bajeti zinatosha kabisa kuleta mabadiliko na maendeleo tunayoyatazamia lakini sasa hakuna anayeshughulika na mnayemuweka anataka yeze anufaike ale ashibe watu wengine wabaki katika matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza juu ya *EPZ*, kuna Kiwanda cha Kubangua Korosho kule Vingunguti walikuwa wanafanya kazi nzuri tu na walijiriki akina mama 2000 leo *EPZ* wamenyimwa wale watu waliokuwa wanashughulika na kitu hicho. Tumesema hapa, tulimweleza hata Waziri wa Viwanda hakuna, kimekufa wanapewa watu wa *NIDA* nenda mkaone vifaa viko *NIDA* pale nje ni magofu matupu wala

hakitakaa sana nendeni mkatembee muone pale. Lakini maelezo yanayotolewa utafikiri kuna maajabu ya uzalishaji hakuna kitu pale tumebeba bomu litatupasukia mkononi. Kama Serikali haioni haya tunayowaambia basi hili ni balaa lingine tulilonalo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda *MUTEX* pale mtu aliyeuziwa kiwanda hicho ameweka ukoo mke wake ndio Mhasibu yeye Meneja na mdogo wake Mwangalizi wa Ofisi. Sasa juzi tena yametokea malalamiko watu wananyanyaswa hivi kweli hatuoni hayo mambo nani akaone kama hatuoni au Bunge zima twende tukalione jambo hilo ndio lieleweke limeonwa, macho yetu ni Serikali yetu muwe tayari kwenda kuona. (*Kicheko/Makofi*)

Tunazungumzia kilimo tutalimaje? Tumekubaliana tupate mbolea, mbolea haikuja kwa utaratibu ulioko watu wamefanya kienyeji wamepewa mabepari wale wale wamenyonya mbolea hatukuiipata. Hata ukisema leo mmeagiza mbolea hakuna anayeeleza bado tunasema tutalima vizuri, tutalima vizuri wapi, mbolea umeagiza? Tusikalie maneno tu tuachane na maneno tubanane kabisa. Wizara ya Fedha imbane kila Waziri aonyeshe utekelezaji wa hela alizopewa kama hakuna utekelezaji huyu Waziri aletwe hapa tumkalishe, 'Kiti Moto'. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna namna nyingine ya kufanya, vinginevyo nchi hii itakuwa ni kama mzaha mzaha tu. Hatuwezi kuendelea, wenzetu kama Urusi mtu aliyechezea uchumi wa nchi yao alipigwa risasi maana huyu ni muuaji au mhujumu. Kwa nini sisi tuwachekelee watu wanaoharibu uchumi wetu na kutuvuruga, eti ndugu, ndugu ndiyo sifa ya kutudhulumu! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuachane na masuala haya ya ndugu ambaye hawesi kutekeleza lengo la Taifa hili, tuwe na tujenge uzalendo. Wale wenye uzalendo wakabidhiwe mamlaka ya kuendesha na kuleta mafanikio na wale ndiyo twende nao kwa pamoa na ndipo tutakapofanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda umefika basi naomba haya tuyaone katika msingi huu. Siku hizi kila ofisi, hata ya kila mtu ni chai asubuhi, watu wameacha kunywa chai nyumbani, wanakunywa ofisini, hela za umma zinateketea. Mimi nilikuwa DC, nilikuwa sinywi chai ofisini. Leo dunia hii imegeuka ndiyo ya kunywea chai ofisini. Hela za umma zinakwenda, sasa maana yake ni nini? Tunakwenda wapi? Turudi, Serikali ibadilike, igeuke na ilione hili na isimamie kwa nia njema ya kuleta mabadiliko na usalama wa fedha zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha kulipa hela ambazo kuna hili jitu limeiba huko Mwanza za walimu, leo mnasema tumepeleleza, kwa hiyo, tutawalipa wale walimu, lakini lile bado lipo linatembea tu, maana yake nini? Acheni, mkamateni yule, mfilisini kila kitu, hata na wajomba zake ili turudishe mali yetu. Nchi hii hatuwezi kwenda maana midomo imekuwa balaa na sumu ya mali yetu ya nchi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hotuba hizi mbili za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na ya Waziri wa Fedha. Kwanza nichukue nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Katibu Mkuu na Makamishna wote kwa kazi nzuri sana ambayo wamejitahidi katika kuandaa hotuba hii ambayo nafikiri ina mwelekeo wa kutuonyesha sisi wapi twende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake wawili ndugu yangu Abdisalaam Issa Khatibu pamoja na Dr. Festus Limbu na Katibu Mkuu ndugu yangu Gray Mgonja na ndugu Lyimo na wasaidizi wote kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya hasa katika kipindi hiki cha Bajeti ya kuhakikisha kwamba hotuba hii kweli ni hotuba ambayo tulitegemea tuipate. Nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hizi mbili ndizo Wizara zinazotupa au kutuonyesha dira na zote mbili zimetamka kabisa kwamba tatizo letu kubwa ni kupambana na umaskini, tuondoe umaskini hiyo ndiyo *agenda* kubwa.

Mimi nianzie pale ambapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amejitahidi sana kutuelekeza jitihada zake za kuona tatizo hilo kubwa la ukuzi wa uchumi hasa kwa upande wa kilimo kwa kuwasaidia wakulima wadogo wadogo, wawekezaji pamoja na wafanyabiashara ndogo ndogo. Kutokana na mabadiliko yale ambayo ameyaleta kwa kweli tungeweza kusema moja kwa moja kwamba hii hotuba amejitahidi kwa nguvu zake zote kusaidia eneo hili au sekta hii ya kilimo. Sekta ambayo Watanzania wengi ndiyo wanaoshiriki na tukitaka kuikomboa nchi hii ni lazima tuhangaike na sekta hii tu basi, tunaweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa ninukuu maneno ya Waziri wa Fedha ndiyo kama mchango wangu alipotamka tarehe 10 Juni, 2004 akisoma Bajeti yake akasema: "Sasa umefika wakati kwamba tupange mikakati, tupange mbinu zetu za maendeleo kwa mbinu za kukusanya nguvu, huu ni mpango wakilishi." Kwa kweli mipango ya kukusanya nguvu ndiyo inayotakiwa hapa. Sasa ukija kwenye mipango ya kukusanya nguvu maana yake nini, *logic* yake ni nini au mikakati yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kumpiga adui mahali dhaifu, ndiyo kilimo na maendeleo Vijiijini. Mapambano Kaskazini mwelekeo Kusini na ndiyo stahili yenye na tatu fyeka adui mmoja baada ya mwengine. Sasa tukielewana hapa mimi nafikiri mambo yatanyooka. Adui yetu mkubwa ni kilimo, sasa tupeleke nguvu zetu zote kwa kilimo na siyo lazima tupeleke kila mahali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nafikiri umeshachagua tangu mwaka jana maeneo yale yaliyo dhaifu, maeneo ambayo yanaweza kufanya yale ambayo tunategemea kufanya, kama vile Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Huo ni uchaguzi sahihi, tunaanza hapo halafu tunaendelea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukitazama katika miaka ya nyuma tulikuwa tunazungumzia juu ya *big four, big four, big four?* Kitu gani kilicholeta *big four*. Kitu

kilicholeta *big four* ni Serikali ilipoamua kupeleka mbolea zote zinazohitajika kufika mpaka kule kwenye Vijiji kwa bei ya nusu ya bei ya mbolea na kutoa mbolea kwa mkopo. Hiyo ndiyo *strategy* iliyotumika, hakuna njia nyingine. Kufikisha mbolea kwenye Vijiji kwa nusu ya bei yake na kwa kutoa mkopo, basi watu walilima, walizalisha hata mahali pa kuweka hapakuwepo, tuliweka katika makanisa, katika ma-*godown* ya shule na katika Kiwanja cha Majimaji, kote kulijaa mahindi. Ndipo tukajifunza, kumbe tulihitajika kujenga maghala na tukapewa fedha ya kujenga mahala na tulijenga. Bahati mbaya sasa hivi hayo maghala hayatumiki na mengine yamegeuzwa kuwa *Secondary Schools*. Sasa hiyo ndiyo ilikuwa mikakati yenewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika tatizo hili la kilimo ambalo tunalizungumzia sasa hivi, mbolea ndiyo msingi wenyewe. Lazima tujue ni kiasi gani cha mbolea kinatumika na inafikaje fikaje mbolea huko Vijijini. Labda ningetoa mfano kidogo wa matumizi ya mbolea. Ndugu yangu Eliachim Simpasa alikuwa anasema hivi hawa Waethiopia wanaweza kutupa sisi chakula, sasa nikimpa *figures* hapa atajua. Ethiopia matumizi yake ya mbolea ni kilo kumi na sita kwa hekta moja, Tanzania ni kilo sita kwa hekta moja.

Sasa unaweza kujua kwamba sisi hatufanyi kazi wakati wenzetu Ethiopia wanafanya kazi, hii ina maana gani? Ina maana kwamba kilimo ni mbolea, kama hakuna mbolea hakuna kilimo. Matumizi ya mbolea kwa Watanzania sasa hivi tunatumia tani 120,000 tumewahi kufika mara moja mpaka tani 180,000 lakini hatujavuka tani laki mbili wakati wenzetu wanatumia tani milioni mbili au milioni tatu za mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni mbolea, bila mbolea hakuna kilimo, huu ndiyo ukweli na hii ndiyo siri yenewe. Sasa katika hili mimi nilifikiri kama tunataka kuleta mapinduzi ambayo Mheshimiwa Basil Mramba ameshaonyesha hapa, basi tuzungumzie suala la mbolea. Mbolea zifike kwanza Vijijini siyo Mkoani, hilo moja. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ifike kule vijijini kwa nusu ya bei. Sasa kama mikakati aliyopanga Mheshimiwa Basil Mramba na itatifikishia mbolea kwa nusu ya bei ya mbolea itakuwa hatujafanya kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanavijiji wapewe mbolea kwa mkopo. Tujaribu hivi tuone matokeo. Matokeo yake yataonekana wazi wazi. Halafu kupeleka mbolea kule vijijini kunataka barabara, lazima uwe na barabara na zipo *standard* hapa. “Kwa wananchi milioni moja basi kama barabara hazijatengenezwa zaidi ya kilomita 1,000 basi hujafanya kitu na mbolea haziwezi kufika vijijini.”

Sasa tunapotengeneza barabara tutazame masuala kama haya na mipango yake kwa kuoanisha suala hili la mbolea na barabara. Mimi nachukulia haya mambo muhimu zaidi. Yako mambo mengi ambayo tungeweza kuzungumzia kama vile mambo ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikikusomea *figures* nyingine kuhusiana na mbolea unaweza kucheka. Sisi Tanzania kwa barabara katika watu milioni moja tumeweza

kutengeneza barabara kwa wastani wa kilomita 114, kwa hiyo, hakuna kitu hapa na mbolea zinaweza kufika kwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbolea katika kilimo ndiyo siri yenewe. Mheshimiwa Waziri labda atajaribu kunielezea kwamba tunapochagua Mikoa michache kama hii ya Nyanda za Juu Kusini, tukapeleka mbolea kwa nusu ya bei, tukazifikisha mbolea Vijijini, hivyo ina gharama kubwa kiasi gani mpaka sisi tushindwe kutekeleza jambo hili. Kwa nini tusijaribu tukaona matokeo yake kwa sababu mimi nasema hii ndiyo siri yenewe ya mafanikio!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la kuwahamasisha maaskari wapiganaji, ndio wakulima hawa. Wakulima Serikali imefanya mambo makubwa sana, imeondoa kodi ya kichwa sasa, wanafanya nini hawa wananchi, unawaondolea kodi basi, halafu hawafanyi kazi, lazima wafanye kazi. Tumeondoa kodi za kila aina, kodi ya kichwa, kodi zenyenye kero za Halmashauri na kodi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi nafurahi kwamba wazee wale wa *Songea Pensioners* mwezi Januari watapata pensheni zao. Sasa hii ni morali kubwa sana. Lakini hii morali italeta nini, tunataka watu wafanye kazi. Tuchukue nafasi hii kuwafanya watu wafanye kazi. Suala la kumfanya kila mtu afanye kazi linakuja hapo. Je, Watanzania wote tutafanya kazi? Ndiyo Mheshimiwa Edson Halinga amelizungumzia. Suala lile la kufanya kazi halina nguvu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Halmashauri kuna kitengo cha kila mtu afanye kazi au wanasema nguvukazi. Ukimwuliza yule ofisa anayekaa pale haelewi maana ya nguvukazi ni nini? Hakuna ratiba ya kazi, baada ya kulima watu wanafanya nini. Wakati wa kiangazi wanafanya nini, Mkuu wa Mkoo unapokwenda kukagua Vijiji anakwenda kukagua kitu gani. Hakuna ratiba ya shughuli za kazi. Hatuwezi kujenga uchumi katika mwelekeo wa namna hii. Kwa hiyo, lazima tubadilishe *attitude* zetu na lazima tufanye kazi kwa bidii zaidi kama tunataka kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kitendo alichofanya cha kuongeza Bajeti ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na amefanya hivyo siyo kwa mwaka huu tu nafikiri katika miaka miwili au mitatu iliyopita. Mimi nampa hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wengine wanakuwa na wasiwasi wanasema ohoo, haya mambo yanahuishwa na uchaguzi wa mwakani na ujambazi. Haya mambo ni ya ulinzi na usalama, ukitaka kuzuia vurugu, jiandae kuzuia kivurugu na ukijiandaa kivurugu, vurugu haiji na ikija haitafanikiwa.

Kwa hiyo, mimi nafikiri kuandaa Bajeti hii ya vyombo vya ulinzi na kuvipa uwezo, sidhani kwamba lengo ni kwa Serikali ya CCM kuwakandamiza wapinzani. Hapana. Watu wenye akili nzuri tu wanapanga vizuri mambo kama haya ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwapa pole sana tena sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata misiba, siyo misiba tu peke yake lakini na kuvamiwa na majambazi barabarani na kupinduka na magari kwa kweli imekuwa ni mikasa ya kusikitisha sana.

Mimi kwa niaba ya wapiga kura wa Songea Mjini natoa pole sana, kwa walioumia Mwenyezi Mungu awasaidie waweze kupona haraka haraka na watu-*join* hapa twende pamoja ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja na wale ambao bado wapo hospitalini tungependa watoke haraka sana ili tuungane wote katika kuijadili Bajeti hii kwa sababu juzi Kamishna wa kuondoa umaskini alitusema sana, alisema ninyi Waheshimiwa Wabunge tunataka mzungumze juu ya Bajeti hii na tunazungumza, hatusubiri kuambiwa sisi tunazungumza. Huu ni wajibu wetu wa kuzungumzia hii Bajeti, kuiweka sawa, kuirekebisha na kuiboresha ili iwe nzuri zaidi na tutaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja zote mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumzia Bajeti ya Wizara hizi mbili. Kwanza kabisa napenda nitoe rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na dada yetu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mzee wetu. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilikuwa napenda tu kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kupata ushindi mkubwa. Mimi naona kana kwamba ameokoka kwa sababu alikuwa amepotea, sasa hivi ameokoka amemrudia bwana nampa hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia katika kuchangia hii hoja iliyo mbele yetu kwa kuanzia kabisa kwa upande wa elimu. Nitazungumzia elimu hasa katika Wilaya yetu ya Geita. Wilaya yetu ya Geita tumeamua kwa moyo mmoja kuendeleza elimu katika Wilaya yetu. Hatuna matatizo mengi mengi makubwa, tumekuja kugundua kwamba katika Wilaya yetu tuna tatizo kubwa la elimu na ndiyo maana kwa siku ya leo nitalizungumzia kwa undani zaidi ili Waziri wa Fedha aweze kunisaidia ni jinsi gani tunaweza kupata fedha ili kuendeleza elimu katika Wilaya yetu. Bahati nzuri katika kitabu chake cha Bajeti ukurasa wa 63, katika upande wa matumizi kuna fedha ya dharura ambayo haikutengewa kitu chochote, mimi nilikuwa naomba tu aipeleke Wilaya ya Geita kama bilioni 4.4 ili ziweze kusaidia katika ujenzi wa shule za msingi, nyumba za walimu na shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo nikiwa na maana tumeamua kwa pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba lazima tuboreshe shule katika Wilaya ya Geita. Mpaka sasa ninavyozungumza tuna maboma 826 ambayo yapo tayari kwa wananchi, kuna maboma 250 nyumba za walimu, tuna shule 21 za sekondari ambazo zipo tayari tunasubiri nguvu ya Serikali. Sasa nilivyokuwa naangalia nikaona kwamba Wizara ya

Elimu haitaweza kumudu kuleta Bajeti yake katika majengo haya. Majengo haya tumeyapigia Bajeti sisi wenyewe katika Wilaya tukakuta kwamba tunahitaji kiasi cha shilingi bilioni 4.4 ambayo tukiitupia Wizara ya Elimu haitaweza kutupatia hizo pesa.

Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akijumuisha katika hii bilioni kumi na sita basi atoe shilingi bilioni 4.4 aipelekee Wilaya ya Geita ili tuweze kupata elimu kama maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Nasema hivyo baada ya kuja hawa wawekezaji katika Wilaya yetu tumeona kuna mapungufu hayo. Hakuna hata kijana mmoja kutoka Geita ambaye ameingia mgodini kufanya kazi, tatizo ni elimu.

Sasa ili kuwakomboa wananchi wa Geita basi namwomba Mheshimiwa Waziri Basil Mramba atoe bilioni 4.4 kuwapelekea wananchi wa Geita ili na wao waonekane katika ulimwengu huu wa Tanzania kuwa na wenyewe wamo, isionekane kwamba Geita wamerudi nyuma na wengine wametangulia na wao kubakia kama wasindikizaji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naingia katika sehemu moja ambayo Mheshimiwa Waziri amejaribu kuelezea, nayo ni kuhusu wastaafu. Tumekubaliana kwamba wastaafu wataanza kulipwa mwezi Januari, 2005. Mimi hilo kwa kweli naliona kama tunazidi kuwatesa hawa watu.

Kwanza kabisa hawa wastaafu hawajui ni akina nani ambao watalipwa. Katika sheria ambayo tulipitisha hapa tulisema kwamba ambao walichukua mkupuo na wamemaliza miaka kumi wakati wameshachukua, lakini wapo ambao mpaka sasa hivi wamechoka tu hata kama alichukua mwaka jana lakini mpaka sasa hivi hana uwezo, pesa zile ameshazimaliza, kwa nini wale watu na wenyewe wasiwekwe katika ule mpango wa mwaka 2005?

Nimesikia hapa Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba afadhali wangeanza mwezi Julai, 2004 kulipwa, hapo ingeweza kuwasaidia bila kuleta matatizo. Lakini tunavyoangalia hapa hao wastaafu wengi mpaka sasa hivi wanatukera katika maeneo yetu, wanasema kwamba itakuwaje watu tumeshastaafu muda mrefu, waje walipwe watu wengine na waliomaliza miaka kumi wengi wameshafariki kwa sababu sera haikuwa hivyo na malengo na maono ya Watanzania au wasomi wa zamani walikuwa wanaona kwamba mtu ukishastaafu basi umeshakufa. Wengi wameshakufa waliobaki ni wachache, kwa nini wale waliochukua mkupuo wasianze kulipwa wote kwa ujumla mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naliomba kabisa hilo Waziri wakati anajumuisha hapa tusiweke kwamba wastaafu walipwe mpaka mwaka 2005, ila waanze kulipwa Julai, 2004. Hilo nilikuwa naliomba tu liweze kutiliwa mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naingia katika *point* ambayo nimeamua nichangie haya mengine yalikuwa ni madondoo tu. Sisi tunaotoka katika maeneo ya madini Mwenyezi Mungu ametuonyesha katika Bajeti hii kwa sababu siku

zote tulikuwa tunaomba mrahaba wanasema kwamba tunataka kuigawa nchi hii na kwamba kuna maeneo ambayo wengine watakuwa matajiri na wengine watakuwa maskini.

Lakini katika Bajeti hii ukurasa wa 57, sehemu ya nne hapo juu sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa inasema, nanukuu: "Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kuzipa uwezo Halmashauri kukusanya mrabaha kwenye madini ya Jasi, *Gypsum*, *Hozorana* na *Chokaa*."

Enheee, jamani, mbona sijaona dhahabu hapa! Kwa nini sijaona Almasi au *Tanzanite*? Ina maana haya siyo madini? Hapo ndiyo nilikuwa naangalia, nilikuwa nasikia kwamba kuna Tume nilikuwa najiuliza hii Tume imeshatoa majibu yake kwamba kuna maeneo fulani madini yake yapewe mrabaha na mengine yasipewe mrabaha. Kwa kweli hii imenisikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kabisa wakati wa kujumuisha hiki kipengele kisifutwe kibaki vile vile, lakini yaongezwe na madini mengine kama Dhahabu, Almasi na *Tanzanite*. Nje ya hapo tutaona kwamba kumbe kuna maeneo mengine yanapogundulika madini yanakuwa ni ya watu, sehemu nyingine basi waishie hivyo hivyo na ndiyo maana ukiangalia kwa undani zaidi sehemu inapopatikana dhahabu hata kwako Mheshimiwa Naibu Spika, almasi, ni watu wapole ambao hawapendi kuzungumza na ndiyo maana mnasema *sleeping gents* na hasa ukiwaona watu wenyewe wanaotoka kule ukimwangalia Mheshimiwa Leonard Derefa, ukimwangalia Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, ukimwangalia Mheshimiwa Ernest Mabina, wote unaawaona kweli hawa wamelala tu hawastahili kuzungumza lolote. Lakini sasa hivi lazima tuseme kwa nini sehemu hivi msiruhusu na sisi Halmashauri zetu zikusanye mrahaba katika madini haya? Kwani sisi tumekosa nini kwa Mwenyezi Mungu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nilikuwa naliomba kabisa wananchi wetu waweze kufaidika na madini haya. Haya madini ni ya Mwenyezi Mungu, tutakuja, Mheshimiwa Anatory Choya huwa anasema kila siku hapa, kwamba tutakuja kuadhibiwa na wajukuu zetu hata kama tumekufa, lakini watakuja kuchapa hata mifupa yetu kwa ajili ya kuachia achia tu vitu kama hivi vikaenda kama wengine wanavyopenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sikupenda kabisa afadhali wasingeweka kipengele kama hiki, watu wengine tusingeona wangetuziba tu kwamba vitu kama hivi haviwezekani, lakini kuna kipengele kimeshaonekana kwa nini maeneo ya Geita Halmashauri zake wasipate mrahaba? Kwa nini Halmashauri ya Kahama isipate mrahaba? Kwa nini Halmashauri ya Tarime, Serengeti na maeneo mengine kama Simanjiro yasipate mrahaba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwa kweli limeshakuwa ni kero na tunamwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa makini. Kama kuna hii Tume tayari imeshatoa majibu basi tuambiwe kwa nini imetoa katika baadhi ya madini tu au katika maeneo tu na haya madini ukiyaangalia yanatoka maeneo ambayo wenzetu wanasema kwamba wameshaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya madini ukiangalia yametoka wapi, utajua kabisa ni sehemu ambazo zilizoendelea, sehemu ambazo hazijaendelea au kuna ule usemi wanaosema kwamba mwenye nacho anazidi kuongezewa, asiyekuwa nacho basi ananyang'anywa hata kile kidogo alichokuwa nacho.

Mimi naona hili suala la madini lazima litiliwe mkazo, sikupenda kulizungumza, nilipenda nilizungumzie katika Wizara yake maalum lakini nimeamua kwa makusudi kabisa kulizungumzia hapa kwa sababu Waziri wa Fedha ameliweka hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba Waheshimiwa wenzangu nafikiri hili kama mlikuwa hamjaliona, nafikiri kuna tatizo katika Serikali yetu kwa nini maeneo mengine yanakuwa na umuhimu na sehemu nyingine hakuna umuhimu. Lazima tuangalie umuhimu ni wa sehemu zote na tunaomba kabisa na ndiyo maana unakuta hata Geita sasa hivi watu wake wanakuwa na maisha ya chini, hawana uwezo wowote. Unakuta kwamba wameshaingiziwa tabia mbaya, lakini hakuna chochote unachoona kwamba madini yametunufaisha, lakini haya madini ambayo yana thamani ndogo ndiyo unakuta kwamba wanachukua mrabaha. Sisi wenye madini yenye thamani kubwa ndiyo tunanyang'anywa yote maana yake nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana kitendo hiki nafikiri kisirudiwe tena, lakini hiki kipengele kisiondoke na wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha aongeze haya madini kwamba na yenyewe yakusanyiwe mrahaba katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi nichangie hoja mbili zilizo mbele yetu.

Kwanza, napenda nimpongeze sana ndugu yangu, mdogo wangu Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kushinda uchaguzi katika Jimbo letu la Bariadi Mashariki. Huyu ni kijana wetu na ni mwana mpotevu na ninaamini kabisa kwamba Mheshimiwa Benjamin William Mkapa atampokea mwana huyu mpotevu na atampongeza kwa kuchinja ng'ombe mnono na mavazi na mambo mengine zaidi. Kwa hiyo, mimi kwa kweli nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niwape pole sana ndugu zangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao impenzi. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Vile vile napenda nimpe pole sana mama yetu Mheshimiwa Anna Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi, kwa kweli nampa pole sana na faraja iliyopo ni kwamba watu waliofanya hicho kitendo juzi nimeona kwenye gazeti wamekamatwa na ningependa niipongeze Serikali kwa kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makofi*)

Vile vile napenda nimpe pole sana ndugu yangu mtoto wa Baba wa Taifa, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa ajali aliyopata wakati anakuja hapa Dodoma. Nampa pole sana na ninaamini kabisa kwamba atapona mapema ili tujumuike naye katika kutatua matatizo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua tunapoongea hapa Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine unawenza ukafikiri kwamba hakuna Serikali hapa, lakini Serikali ya Tanzania ni Serikali mahiri sana, ninaamini kabisa kwamba viongozi wake Mawaziri, Mheshimiwa Rais wetu na hata Chama chetu napenda vile vile nikipongeze ni chama mahiri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Mapinduzi ni Chama na kina masikio mazuri na kinasikiliza. Napenda niipongeze Serikali katika Jimbo langu la Shinyanga Mjini nilikuwa na matatizo makubwa ya maji, mwaka 1994 Bwawa lilikauka, mwaka 1996 lilikauka, mwaka 2000 lilikauka, lakini Serikali ilichukua hatua thabiti. Kusema kweli pamoja na kwamba hatujapata maji ya *Lake Victoria*, lakini tatizo la maji limeshughulikiwa kikamilifu na ninyi ni mashahidi hata hapa Dodoma wakati tunaanza Bunge hapa hatukuwa namna hii. Kwa hiyo, mimi ningependa niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuwe na subira, Serikali inasikiliza. (*Makofii*)

Vile vile napenda niipongeze Wizara ya Ujenzi katika ahadi za Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, mojawapo ilikuwa ni barabara itapita katika Mkoa wa Shinyanga, kazi hizi zote zimefanyika na maji sasa hivi tunayo ya kutosha kwa kiasi kikubwa ingawa hatujapata maji ya Mradi wa *Lake Victoria* ambaeo na wenyewe sasa hivi unashughulikiwa.

Vile vile ningependa niipongeze sana Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana na Wizara nyingi zimefanya kazi nzuri sana kuhakikisha kabisa kwamba nchi ya Tanzania inatawaliwa na watu mahiri, inatawaliwa na viongozi mahiri, inatawaliwa na chama mahiri, naamini kabisa kwamba mapungufu tuliyokuwa nayo tangu tumejitawala ni mengi na wengi tungelipenda mambo yabadilike kesho lakini maendeleo siyo rahisi ni kama kupanda mwembe, huwezi kuupanda leo kesho yake ukala maembe. (*Makofii*)

Vile vile ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, sasa hivi huyu *brother* ni Pesanyingi. *Actually* kwa kutumia neno la Kiingereza *is a Financial Wizard* ni mchawi wa fedha. Kwa sababu ukitazama tulikotoka na mimi niliwahi kusema hapa mkachecha, lakini nikasema kwamba fedha ndiyo kitu ambacho kinaweza kikatuondolea matatizo, ukiwa huna hela hata kama ni Profesa, *brother you are useless present*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Basil Mramba ameifanya nchi hii angalau ikawa na hela na matatizo yetu tunayoyaongelea hapa yatakelezwa *because there is money now*. Tunaelewa kabisa kwamba *in past* nikiongea hapa watu wengine wanawenza wakanihukumu lakini *let us be very frankly* kwamba Serikali ya Awamu ya

Kwanza haikuacha hela kwenye *Treasury*. Halafu Serikali ya Awamu ya Pili, haikuacha fedha kwenye *Treasury*, mimi nilimwuliza Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, kwamba, *how much money is there, now we are Members of Parliament? He said there was zero money.*

Lakini Mheshimiwa Benjamin William Mkapa pamoja na huyu *brother he has created money in this country* na ndiyo maana tunaona sasa hivi miradi inafanyika. Kwa hiyo, pamoja na mapungufu yaliyopo kwa kweli mimi nasema kwamba lazima tuwapongeze sana ndugu zetu hawa wamefanya kazi vizuri, tunaelewa kabisa kwamba hata sisi hapa tulipo hapa hata mimi *I am not NGO*, siyo lakini kazi inafanyika na ninaamini kabisa kwamba mapungufu yaliyopo Serikali inayashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti tunayoongelea hapa sasa hivi ni Bajeti nzuri, kusema ukweli bila kuficha *is an excellent budget*. Yapo mapungufu ambayo mimi baada ya kuisoma hii Bajeti, mapungufu yapo katika viwango vingi siyo vidogo *per se* hasa ni kwenye madini. Suala la madini lina mapungufu makubwa sana mimi nimejifunza mambo ya Benki na uchumi kidogo *I am not a Professor*, lakini nafikiri unaweza kusema kwamba ni *traditional economist* kwa kutazama vitu vinavyokuwepo. (*Kicheko*)

Lakini nataka niseme hivi, kwa mfano, katika nchi ya Tanzania *factors of production, land* ndiyo namba moja, huwezi ukafanya *investment* juu ya hewa, halafu inafuatiwa na mtaji (*capital*), walio na mtaji, halafu inafuatiwa na *Entrepreneurial function* lakini huwezi uka-invest hewani bwana. Sasa hawa watu wanaoleta fedha hapa kwenye ardhi yetu je, kama kwa kweli nchi hii tumesema kwamba waje watu wavune hapa *we could see, can I say a bad word* lakini *we could be stupid*, sababu haiwezekani kabisa mtu aje na hela zake tu na ardhi yetu halafu achukue madini yetu hapa, Dhahabu zetu, Almasi zetu, *Tanzanite zetu this stupidity*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ila nimefaidika kwenye Bajeti kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema kwamba lazima zile sheria *we have to review them*, lazima ziwe *reviewed* na hii kazi lazima ifanyike haraka *because otherwise we are loosing so much money*, inawezekanaje mtu anakuja na fedha zake tu hapa, halafu anachukua dhahabu zote hapa, halafu anakwenda huko, halafu hao watu waliofanya *investment* hapa wanakuja na fedha zao, siyo, halafu matumizi yao ni ya kipuuzi puuzi, unakuta wanakaa Dar es Saalam, *they fly with an aircraft* kutoka Dar es Salaam mpaka *Kahama Gold Mine* mara nne, halafu tunakubali matumizi yao, *are we crazy?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo maneno machache nafikiri yamenitosha. Dhahabu sasa hivi imepanda bei hawa watu hawalipi *wind fall tax*, wakati tunakubaliana nao dhahabu ilikuwa dola 250, leo dola ni 450, halafu *they are taking everything, are we crazy! No this is bad.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niongelee kuhusu benki ya kilimo. Hili suala tunatakiwa tulifanye haraka kama inawezekana kubadilisha baadhi ya benki

zilizopo zibadilishwe. Ningependa nisema hapa *experience* ya India. Ni kwamba India ilisema hivi *five percent* ya *Commercial Bank Deposits* lazima zipelekwe kwenye *Agricultural Bank*, halafu zichanjiwe *at very low*, Tanzania ukitazama kwenye *interest Bank Bulletin we have about one point four trillion* na hizi *trillion* uki-calculate about *seventy billion* zingeweza zikaenda kwenye benki ya kilimo na kwa hapa ndiyo tungeweza tukabdalisha mambo.

Napenda niongelee vile vile suala la njaa. *Actually* njaa unajua ukichukua zile *farming seasons*. Sasa hivi tunamaliza 2003/2004 lakini tunakwenda kwenye 2004/2005 *this is an introduction* ya njaa, njaa *actually* iko kwenye 2004/2005. Ningependa nisema kwamba uchaguzi mara nyingi tunaufanya wakati wa njaa na lazima tukubaliane nimepita njiani kuna mahindi mengi sana sasa hivi *the price of maize is very cheap*, hivi Serikali kwa nini isiwapo watu *SGR* wakaanza kununua mahindi pale. *I know* hivi kwa nini tunapenda ku-import at high price wakati tukiwa fedha hapa tungeliweza tukapata mahindi kwa bei nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme suala la hospitali ya Shinyanga. Hospitali yetu ya Shinyanga ni hospitali ya Mkoa na kwa bahati mbaya tuko watu milioni 2.9 *almost three million*, lakini kwa bahati mbaya hatuna wataalam wa kutosha nilikuwa naomba Serikali kuititia Wizara ya Afya itupe wataalam na kwa bahati mbaya kabisa Daktari wetu ambaye tulikuwa tunamtegomea Dr. Kimambo amefariki juzi, naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amin*.

Tunaomba tupewe wataalam wa kutosha kwa sababu sasa hivi tuna matatizo makubwa sana na vile vile watumishi kama walivyosema wenzangu watumishi wengi hawajalipwa zile *on call allowance* zao *what is a problem?* Tunaomba watumishi hao wawe *motivate* walipwe hizo fedha zao bila kufanya namna hiyo tunaweza tukapata matatizo makubwa sana.

La mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kufanya mkutano nikiulizwa hivi hela za elimu zimeteremka mpaka kwa Mwenyekiti wa Shule, wakaniuliza hivi kilimo ni uti wa mgongo *where is that money?* Mheshimiwa Charles Keenja, tafuta uwezekano *you are a good guy*, teremsha zile fedha zishuke kule zikafanye kazi *brother, no, it is terrible*, fedha zako bado zina *hang* kule hatuziona kule, hivi mwenzako ametumia njia gani na wengi wanasema kwamba kazi ya elimu wanaiona, kazi ya barabara wanaiona, kazi ya maji wanaiona, kilimo ni uti wa mgongo *where is that money* kwa nini usiziteremshe kule kama unaogopa zisiibiwe mbona za mwenzako wa elimu watu hawajaziiba, teremsha fedha hizo zienda huko na utakuwa umetusaidia sana kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ISSA MOHAMED SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo, kuweza kuchangia katika hoja hii ya Bajeti ambayo ilisomwa siku ya Alhamisi iliopita. Lakini kabla ya yote, napenda niungane na wenzangu kuwapa pole Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji,

Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba wa baba yao uliotokea wiki iliyopita na Mwenyezi Mungu ataiweka roho ya marehemu mahali pema peponi na wao atawapa moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina machache tu ambayo nataka kuyachangia katika hotuba hii ya Bajeti hususan juu ya mambo yanayohusiana na shughuli zote za utoaji mizigo katika bandari zetu za nchi hii. Kwanza, napenda niipongeza Serikali kwa maamuzi yake walioyaeleza katika Bajeti juu ya kuona matatizo ya walipa kodi wengi walikuwa wanaingiza bidhaa ndani ya nchi hii waliyokuwa wakiyapata kwa muda mrefu hususan urasimu na ucheleweshaji wa kutoa mizigo katika bandari za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wengi walikuwa wanapata matatizo makubwa kama alivyoelezea Waziri wa Fedha katika hotuba yake, lakini ikiwa yatasimamiwa kama alivyozungumza Waziri wa Fedha basi napenda niwasemee wafanyabiashara wanaozitumia bandari hizi kwamba watashukuru na watakuwa pamoja na Serikali yao pamoja na kushirikiana kwa hali zote na *TRA* ili kuweza kulipa kodi kama inavyostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu matatizo ya urasimu uliokuwepo ndiyo ulikuwa unawafanya walipa kodi wabuni njia za kukwepa kulipa kodi ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, ikiwa wataondolewa urasimu nafikiri watakuwa walipaji wazuri na kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matatizo yaliyokuwepo bandarini hayasababishwi na *TRA*, matatizo hayo yanababishwa zaidi na vyombo vinavyoshirikiana na *TRA* katika utoaji mizigo bandarini. Kwa mfano, kuna taasisi nyingi ambazo zinatoa ushirikiano na *TRA* kwa mfano, kama *TBS*. *TBS* inayopima kiwango cha ubora wa bidhaa zinazoingia nchini inasababisha mara nyingine ucheleweshaji wa mizigo na hatima yake walipa kodi wanakuwa wanailaumu *TRA* ambapo hapaswi *TRA* kulaumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna tatizo la sheria la uingizaji wa matairi, *importers* wa matairi yakifika matairi yao Dar es Salaam bandarini au *port* za Tanzania yanatakiwa kwanza yachukuliwe na *TBS* kuangalia kiwango cha ubora. Sasa tatizo lililopo *TBS* hawana vifaa vya kupimia matairi kiwango cha ubora.

Kwa hiyo, wanachukua matairi yale *TBS* wanawakabidhi *General Tyre* kwa kupimia viwango vya ubora. Kwa hiyo, wakipeleka kwa *General Tyre* kwa sababu na yeze ndiyo mfanyabiashara wa matairi nchini kwa hiyo, wale wanaoingiza matairi wanakuwa ni maadui zao, kwa hiyo, wanakuwa hawayasimamii vile inavyopaswa, wanayachelewesha chelewesha na kuyafanya urasimu na kuyakalia kwa muda mrefu.

Kwa hiyo, utakuta mwagizaji wa matairi matokeo yake anaweza akaweka matairi bandarini kwa miezi miwili, mitatu, *TBS* bado hawajampa jawabu kwa sababu wale *General Tyre* hawajayapima. Kwa hiyo, mambo kama haya yangeangaliwa kwa sababu

yanapeleke waagizaji wa mali kuilaumu moja kwa moja *TRA* ambapo haistahiki kulaumiwa. Kwa hiyo, Serikali ingeangalia Taasisi hizi ili kuweka mazingira mazuri, watu wasiweze kulalamika kwa kupata usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni hili juu ya *TBS*. Mimi sifahamu *TBS* kama majukumu yake ni kupima viwango vya ubora wa kila kitu kinachoingia katika nchi hii au wana majukumu ya kupima vyakula tu. Kwa sababu sasa hivi kuna utaratibu wa magari yanayoingia Tanzania kupimwa kiwango cha ubora wanasema wanafanya Tanzania isiwe dampo la magari mabovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa toka mwaka 2002 magari yote yanaoingia hususan kutoka Dubai ambapo karibu tunapafahamu, ukinunua gari unastahili kuipeleka kupimwa *TBS* katika *workshop* ya mfanyabiashara binafsi Dubai pale kuikagua na yeze ndiyo anaweza baada ya kuikagua ndiyo mwenye mamlaka ya kutoa *Certificate* ya gari linalostahili kuingia katika nchi hii. Kwa hiyo, kila gari analipwa dola 150 ambapo ni sawa sawa na shilingi 165,000 kwa hesabu ya sasa ya dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukilipa dola 150 ndiyo unapewa kibali cha kuingiza gari Tanzania. Lakini la kushangaza hiyo kampuni kwanza iliyopewa mamlaka hayo haifanyi kazi kama walivyoingia mikataba na Tanzania, kwa sababu kwanza hawaikagui gari kwa kina. Unakwenda mara nyingine unapewa *Certificate* ya kuingiza gari bila gari kukaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ikiwa kila gari tutaitoa Tanzania nchi maskini dola 150 ndani ya nchi maskini tunaipeleka nje bila kurudi dola 150 kwa mwaka mmoja idadi ya magari yanayoingia kwa kiwango cha chini hayapungui magari 20,000 kwa mwaka na kila gari ikiwa italipiwa dola 150 ni dola milioni 3, tunaitoa ndani ya nchi maskini tunaipeleka kwa mtu binafsi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa utaratibu huu kweli nchi hii tutaweza kujikombua na uchumi wetu duni kama huu tulionao sasa hivi ikiwa kwa kila mwaka tutatoa zaidi ya bilioni 3 kuzitoa nje fedha ambazo hazirudi hapa nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nafikiria kwa mtazamo wangu ikiwa kuna lazima ya kukaguliwa magari basi bora Serikali ingeandaa utaratibu wa kukaguliwa hapa ndani. Kwa sababu tuna vyombo vingi hata Jeshi la Wananchi wanacho kitengo cha ufundi wanaweza kukagua wao magari dola 150 tukawalipa wao ikafanya kazi ndani ya nchi hii hii. (*Makofî*)

Chuo cha *VETA* wanao uwezo wa kufanya ukaguzi wa magari ndani ya nchi hii na dola 150 tukawalipa wao ikafanya kazi ndani ya nchi hii hii fedha hiyo. Kwa hiyo, mimi mawazo yangu kama kuna lazima magari kukaguliwa yakiingia nchini basi ni vyema yakafanyiwa ukaguzi ndani ya nchi hii ili fedha tusiitoe nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mdogo lakini nina mambo mengi kidogo lakini nitajitahidi kuongea ambayo nitafanikiwa kuyazungumza. Jambo lingine nataka

nizungumzie masuala ya mabenki. Suala la mabenki kuhusu kukopa kwa utaratibu uliowekwa na mabenki watu wadogo wadogo katika nchi hii hawawezi kukopa, ikiwa mtu atafanikiwa kukopa kutokana na huo mlolongo wa sheria basi ukilinganisha na riba anayotozwa mara nyingi si rahisi mtu kufanikisha kulipa deni analolikopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo nakupa mfano, huu ikiwa utakwenda benki kukopa labda milioni 10 ya kufanya biashara, basi utaambiwa kwanza lete hesabu ya miaka mitatu, ukienda kwa mtaaalamu kufanya hesabu atakwambia anataka *ten percent* ya milioni 10 kwanza unilipe mimi. Kwa hiyo, katika milioni 10 umpe ye ye *ten percent* ambayo ni milioni moja unaanza kuitumia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimaliza utaambiwa lete dhamana yako ifanyiwe *evaluation*, ukimpelekea mtu wa *evaluation* kama dhamana yako ina dhamana milioni 15, unaambiwa toa *ten percent* umpe milioni moja na laki tano. Kwa hiyo, milolongo kama hiyo utajikuta kama unakopa milioni 10 benki mpaka kuzipata basi wewe umeishatumia milioni 3. Kwa hiyo, ukizijumlisha na riba ambayo utatoa wengi wanakuwa hawana uwezo wa kurudisha madeni hapo wanapopata kukopa. Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali iangalie *at least* kupunguza mlolongo wa sheria ili wakimuona mtu anastahili kukopesheka basi wamkopeshe bila vikwazo vingi na milolongo mingi ya gharama kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie nataka nirudie huku huku kwenye magari ili kuifanya Tanzania isiwe dampo ya magari ambayo hayatumiki tena kwa wenzetu je, Serikali isingeona vyema kuweka utaratibu wa mfumo ambaao wanao wenzetu wa Serikali ya Kenya *at least* kuingiza magari kwa kucheleta basi ya miaka sita nyuma, zaidi ya hapo yawekewe kodi kubwa na yawekewe vizingiti yasiingie ili Tanzania isiwe dampo ya magari mabovu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani magari nje si aghali, magari ya mwaka 1988, mwaka huu 2004 ukienda Dubai kununua gari la mwaka 1988 linalingana bei kwa sababu wafanyabiashara wote wanakimbilia kununua magari ya mwaka 1988 kwa sababu ya kusema tutapata unafuu wa kodi Tanzania, kwa hiyo hatimaye Tanzania inakuwa dampo ya magari mabovu ambayo yanahatarisha usalama wa wananchi, yanayumbisha uchumi kwa kutumia fedha nyingi kuagiza vipuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri Serikali ingeliangalia hilo kama Kenya wenzetu sheria yao zaidi ya miaka nane gari haitakiwi tena kuingia, ikiwa utaleta gari lenye miaka zaidi ya nane kodi yake inakuwa kubwa na sisi Tanzania tungefuata mfumo huo ungesaidia zaidi kusonga mbele isiwe leo tunatumia mitumba ambayo wenzetu hawaitaki tena. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo mimi nataka nilizungumzie hapa kidogo ni la malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar, wanalamika kwamba iwapo wanatoa mizigo yao Dar es Salaam kupeleka Zanzibar wanalipia mizigo *THA* kwa tani moja shilingi 6,000 ukienda Zanzibar. Lakini mizigo ule ule ukitoka Dar es Salaam kwenda Mafia au kwenda Mtwara unalipiwa shilingi 500. Sasa hili lipo na linalalamikiwa. Kwa hiyo, ni vyema kulizungumza hapa ili labda Serikali kama mimi

sikuelewa watalitolea ufanuzi na kama ndiyo hivyo ilivyo basi waweke haki sawa kwa kila Mkoa. Sio haki sawa ya *CUF*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie.

Vile vile ningependa na mimi nitoe rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao mpenzi, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Uhai unatoka kwa Mwenyezi Mungu na unarejea kwa Mwenyezi Mungu, wao wametangulia na sisi tunafuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane sasa na wenzangu kuiunga mkono hoja hii iliyoletwa mbele yetu kwa asilimia mia moja. Vile vile kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kazi nzuri walizozifanya.

Lakini pamoja na kuwa Bajeti hii haisisimui kwa sababu zifuatazo, baadhi ya ahadi ambazo zilitolewa huko nyuma zimerudiwa rudiwa katika Bajeti hii na imeipa sura ya *cut and paste budget*.

Pili, mengi yaliyozungumziwa na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, nimesema Waziri wa Mipango nisiseme tena Kugoda nikakosea kwa mara nyingine. Yaliyozungumzwa na Waziri wa Mipango yamerudiwa rudiwa tena kwa kiasi kikubwa na Waziri wa Fedha.

Tatu, Bajeti hii ime-*generalize* mambo mengi sana hasa katika sekta ya kilimo, lakini labda Waziri wa Kilimo na Chakula baadaye atatueleza ana mipango gani kukuza kilimo kwa sababu katika vitabu hivi viwili vyta Bajeti tumeelezwa ya kuwa kutokukua kwa uchumi kumesababishwa sana kwa kuzorota kwa kilimo na tumeshindwa kufikia asilimia 6.3 ambazo zilikuwa zinatarajiwa mwaka huu.

Lakini nne, Bajeti hii haina *vibrancy*, haisisimu, haitekenyi, inakosa *vibrancy*. Namwonea huruma Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu *bottom line* ya Bajeti ambayo inatarajiwa iwe *vibrant* ni Bajeti ambayo ina *economic growth*. *Economic growth* imekosekana. Kwa hiyo, kama ilivyo kwa uchumi kutokua kwa kasi lazima utapata shida kupanga Bajeti ambayo ina mwelekeo wa maendeleo. Lakini niseme kuwa Bajeti hii sio mbaya, Bajeti hii ni nzuri. Uzuri wake ni kuwa imewalenga wanyonge kuwasaidia na ni Bajeti ambayo kwa hakika *is very mild*, haina madhara.

Lakini ningependa nimtahadharishe tu Mheshimiwa Waziri kuwa hili deko ambalo daima tukija hapa kila mwaka tunadekeza *informal sector*. Naomba Bajeti inayokuja na nimeshapata maeleo tayari kutoka kwa wataalamu ya kuwa tuko katika hali ya kupaa uchumi wetu uko tayari ku-*take off* kwa sasa. Kwa hiyo, tusije tena na

dekezo kama hili kwa sababu hakuna nchi ambayo inazungumzia *economic development ikategemea informal sector*. *Informal sector* daima itakuwa inatafunya *formal sector* ambayo hasa ni muhimu katika maendeleo ya uchumi. Najua nasema hili wengine hawatalipenda lakini *that happens to be an economic truth*.

Nimpongeze Mheshimiwa Basil Mramba kwa kazi nzuri sio tu kwa Bajeti hii, nimpongeze vile vile kwa kuwa ni mchapakazi mzuri sana, ameishika Wizara hii vizuri. Nimpongeze yeche na timu yake ikiongozwa na Bwana Gray Mgonja na vile vile nimpongeze Bwana Kitilya kwa kuwa msimamizi mzuri wa ukusanyaji mapato. Si kwa maana ya kukosoa Bajeti hii bali kutaka maelezo. Imeelezwa katika ukurasa wa 34 kuwa utendaji kazi wa *TRA* utaboreshwani ili kutoa huduma bora kwa walipa kodi. Sasa mimi nilikuwa nataka niulize hii huduma bora kwa walipa kodi itakuja kwa sura gani. Kwa sababu mpaka leo mtazamo wa Maafisa wa *TRA* kwa walipa kodi wanamtazama kama adui. *Approach* yao kwa walipa kodi sio kabisa *tax payer friendly* hata kidogo. Nataka hili liangaliwe. (*Makofii*)

Kuna *harassment* kubwa wanafanyiwa walipa kodi pengine huko ngazi za juu hamjui. Mimi niko kwenye Kamati ya Mambo ya Nje mara kwa mara tunawaalika Mabalazi kutoka nje kuja kuzungumza na sisi na wengi wao wanaitaja hii wanasema ninyi ni nchi ya peke yenu ambayo mnawa-*harrass* walipa kodi. Ikiwa mlipa kodi ame-*submit return* zake na zimepitiwa na *Auditor* au *Chartered Accountant* na Ofisi ya *TRA* ikakubali ya kuwa haina makosa wakakubali fedha zije inakuwaje baada ya mwezi mmoja au miezi miwili vijana wanatoka kwenye ofisi zao wanakaa wanazunguka zunguka kwa wafanyabiashara wanapoteza wakati wao. *It is a harassment* ambayo lazima izuiwe. Mtu kwa heshima kabisa akishakubalika kuwa amelipa kodi yake sahihi muachenii aendelee na kazi zake za uchumi na ninyi endeleeni na kazi zenu *TRA*. Mimi nadhani hilo mliangalie.

Kusema ya kuwa malalamiko ya walipa kodi yamepungua isiwe kigezo, si kigezo hata kidogo. Kwa sababu ujambazi hapa watu wameacha kuzungumzia ujambazi. Wamepunguza, haina maana kuwa ujambazi umepungua, ujambazi umezidi. Rushwa tumeacha kuizungumzia watu wamechoka kuizungumzia rushwa lakini rushwa ipo na inaendelea. Kwa hiyo, hiyo isiwe kigezo ya kuwa rushwa imepungua au ujambazi umepungua au kwa sababu walipa kodi sasa hawazungumzii tena juu ya adha iliyopo kwa hiyo, ikamaanisha ya kuwa walipa kodi wameridhika.

Mimi nadhani ingekuwa vyema *TRA* wange-*consult* Kampuni maalum za *private* kwenda kuwahoji walipa kodi katika mazingira ambayo yatakuwa hayawatishi au kuwaogopesha. Nadhani Mheshimiwa Waziri atashtuka kwa malalamiko ambayo atayapata.

Lingine katika hili ni ule utaratibu wa kuweka viwango vya kukusanya kodi katika mikoa. Hii inatoa adha kubwa sana kwa sababu ukimwambia ofisa wako lazima mwezi huu alete *X-price, X-amount of money*, anahangaika kweli kuzikusanya. Kama hapa Dodoma uchumi wetu ni dhaifu lakini unaweka kiwango cha juu kwa hiyo Maafisa wa *TRA* wanazunguka kwenda kukusanya kodi ambayo si halali na wala hawana mahali

popote pa kwenda kushtaki. Kwa hiyo, wanalipa tu ingawa kodi inayolipwa sni ile ambayo si halali na viwango vitazamwe kwa hali ya uchumi wa Mkoa hadi Mkoa. Hilo mimi likifanyika nitafurahi sana kwa sababu kama halitafanyika basi kwa hali hii inayoendelea sidhani tutafika kwenye kujikadiria kodi sisi wenyewe kama ilivyotajwa katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo halipo katika Bajeti hii lakini naomba nilizungumzie ni utaratibu wa Benki Kuu kuwa na matumizi yao wenyewe bila kupitia hapa Bungeni. Hata Rais ofisi yake matumizi yake yanapitishwa hapa Bungeni, lakini *BOT* haipitishwi hapa Bungeni. Laiti ingekuwa fedha wanazotumia *rationally* tunaweza kuwaeleza wananchi zimetumiwa hivi na wakazikubali na ikawa ni halali kabisa watu wangeweza kuelewa. Lakini wananchi hawaelewi.

Kuna jengo linajengwa pale *BOT*. Lilipoanza watu hawakushtuka lakini sasa zaidi linavyopanda mimi kwangu ni *monstrosity* kwa hakika. Lakini watu wanaanza kushtuka nini hii wanahamishiwa *United States Treasury* Dar es Salaam. Haya majengo yanatakiwa na *BOT*. Kweli katika kiuchumi chetu kidogo hiki katika orodha ya nchi maskini sisi wa pili au wa tatu huku chini. Je, tunahitaji kupoteza *millions and millions of dollars* kufanya *extension* iliyokuweko pale? Vijisenti vyetu hivi tunavyohangaika hapa kuzikusanya, wananchi waweze kupewa katika maendeleo yao tunazitoa utadhani kondakta wa daladala. Lakini wao wanatumia wanavyotaka kwa hakika hili mimi silipendi na nadhani lazima tufanye marekebisho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hainiridhishi kabisa matumizi ya *BOT* katika kujijenga wao wenyewe. Sijui labda tunaiga nchi zingine zilizoendelea. Wana majengo makubwa ya kuweza ku-accommodate mambo mbalimbali. Lakini ukienda *London Threadneedle Street* utakuta pale jengo moja linaitwa *Bank of England*. Jengo lile liko pale miaka 600 halijazidishwa chumba wala ghorofa na inahudumia nchi ile uchumi wake kikamilifu kabisa na wamekuwa na miaka kama 200 ya kutawala karibuni nusu ya dunia mimi sielewi lile jengo linajengwa kubwa la namna ile la nini. Wanakuwa na *conference centre*. Inahu *BOT* kuwa na *conference centre* hii? Ni *civic affair. It has nothing to do with the Bank of Tanzania*. Ni njia za kutumia fedha kwa sababu wamepewa ruhusa watumie wanavyozitaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imetajwa hapa kuwa kutakuwa na fedha zitatengwa kwa ajili ya uwanja wa kisasa (*Modern Stadium*). Mimi naipongeza Serikali kulifikiria hilo, *it is long overdue* wakati wake waamuzi waliofanya hivyo wamefanya maamuzi mazuri na ningependa kama siondoki katika utaratibu namwomba Mheshimiwa Basil Mramba atakapofanya *wind-up* atutajie majina ya watu waliofanya uamuzi kutuletea *Modern Stadium* ili tuweze kuapongeza hapa.

Lakini atutajie vile vile majina ya watu waliofanya uamuzi eti *National Stadium* ile iwe kule kule ubavu na *National Stadium* iliyoko hivi sasa. Ni fikra finyu kwa kweli. Katika mji ambao unakua *infrastructure* zimekwisha, *clogg up* pale katika Uwanja wa Taifa ambao unachukua watu 25,000 au 30,000 watu wakitoka pale uwanjani na magari na nini kwa sababu ya *infrastructure* mbovu inachukua karibuni saa tatu.

Leo unakwenda kuweka uwanja mwingine, *Modern Stadium* ya kuchukua watu 60,000 na 70,000 pale pale. Katika mji ambao unapanuka kwa nini usiweke mahali kama Kibaha. *Why?* Kwa nini pale pale? Nchi gani inafanya hivyo? Mimi naomba hilo lifikiriwe tena maana ujenzi haujaanza na wakati upo kubadilisha maamuzi ambayo yalitokana na fikra finyu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho najua wakati wangu ni mdogo nililotaka kuzungumzia ni kuhusiana na moto ilitokea nyumbani kwa Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Ikiwa mwananchi namba moja hana usalama sisi makabwela sijui tutafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, *fire system* na huduma ya Zimamoto tuliyokuwa nayo katika nchi hii daima imekuwa mbovu na watu wanajua hivyo lakini Serikali haijaifanyia kitu chochote. Iliyobaki sisi viongozi mara kwa mara tukiona wale wazimamoto wanakwenda mahali kuzima moto na wanashindwa kuzima moto wanapigwa mawe tunasema wahuni waliowapiga mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, si wahuni walimewapiga mawe. Ni wananchi, *they are making a statement* ya kuwa hawaridhiki na huduma ile. Ni vizuri unajua kugonga gonga kidogo kompyuta unapata faida. Hapa ninalo gazeti ambalo linasema kuwa Serikali inaagiza *fire tenders 13* kwa bei ya *over 7 billion shillings*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, ilikuwa nzuri sana lakini basi nitafanyaje. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na pia hotuba ya Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji.

Naomba nianze kwa kutoa pongezi kwa Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri na kwa kweli kwa Bajeti nzuri inayotoa matumaini makubwa kwa watu wa kipato cha chini. Naipongeza kabisa mwanzoni na naiunga mkono hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu kubwa ni utekelezaji wa yale ambayo tunayaamua kuyatekeleza. Kama walivyosema wengine hata yale ambayo tumeyapitisha na kukubaliana katika Bajeti ya mwaka jana mengine bado hayajatekelezwa. Sasa hii inaleta matatizo. Ni vyema tukajenga tabia ya ufuatiliaji wa hayo tunayoamua na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii nzuri inaweza kwa kiwango kikubwa isifikie malengo yake kama mambo kadhaa hayatakekelezwa. La kwanza ni bei kubwa ya mafuta na umeme. Kama bei ya mafuta ilivyo na jinsi inavyotegemewa kuendelea kupanda haitarekebishwa. Kama bei ya umeme itaendelea kupanda hali ya Bajeti haitatekelezeka na tutapata mapungufu. Kwani gharama za mafuta na gharama za umeme anayekuwa kuzibeba baadaye ni huyu mlaji mdogo ambaye ni wa chini. Wote tumekuwa mashahidi

wa jinsi bei ya usafiri na usafirishaji inavyopanda siku hadi siku kwa sababu hakuna udhibiti wa bei ya petroli.

Miaka iliyopita tulipitisha sheria ya kuanzisha *EWURA* mpaka hivi sasa *EWURA* haijaanza kazi sijui tatizo ni nini. Ni hapo tu *EWURA* itakapofanya kazi ikaanza *ku-regulate* hizi bei ndipo mtu wa kawaida atawea kunufaika na Bajeti kama hii. Ni vyema *EWURA* ikafanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni uingiaji wa fedha haramu nchini katika mzunguko wa uchumi. Nina hakika Waziri wa Fedha anafahamu hili na mipango imeshafanywa chini ya *SADC* baada ya kuliona hili tatizo na hili tatizo la fedha haramu kuzunguka katika uchumi ndilo linasababisha kuleta *distortion* hata katika viashiria vya uchumi. Maana yake unakuja kuta ni fedha zimeingia bila mpangilio na Serikali na *BOT* hawajui. Ni vyema mikakati ikawekwa ya makusudi kabisa kudhibiti hali ya mzunguko wa fedha haramu katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo linaweza kuathiri Bajeti hii nzuri ni rushwa. Rushwa kwa kiwango kikubwa inaweza ku-*erode* yale tuliyotegemea. Wengi wanaweza kusema rushwa ipo au haipo. Lakini kama inazungumzwa tuamini kwamba rushwa ipo. Wakati wa ibada za Pasaka mwaka huu wale waliofutilia wachungaji wote na Maaskofu walizungumzia suala la rushwa kuwako nchini. Hata kiongozi aliyeiwakilisha Serikali kwenye ibada pale Magomeni alizungumza kuwapo suala la rushwa ndani ya nchi yetu. Sasa si kwamba rushwa haipo. Nadhani tukubali kwamba ipo na ni tatizo tuanze kuangalia tutaikabili vipi. Lakini inayonipa matatizo zaidi si kwamba watu hawataji rushwa au hawaamini kwamba rushwa ipo. Ni jinsi Serikali inavyoichukulia rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeomba watu wajitokeze na watu waliojitlea kujitokeza na kutaja majina. Wako waliozungumza juu ya mchezo mchafu, wako waliozungumza baadhi ya viongozi kwamba ni wala rushwa. Hivi kama walisema uongo kwa nini Serikali haisimami na kuwapeleka Mahakamani hawa watu kwa kuwapaka matope viongozi wetu? Ni vyema tuthubutu tukubali kama rushwa ipo na hawa waliojitlea kama ni waongo wachukuliwe hatua za kisheria wafikishwe Mahakamani. Ama sivyo tukinyamaza kama Serikali watu watazidi kuamini kwamba kweli hawa watu ni wala rushwa na itakuwa inapaka doa Serikali nzima, naomba tuanzie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo tumelikuta ni gharama kubwa za huduma ambazo Serikali inalipia bila sababu za msingi. Hii imetokana na baadhi ya watendaji ndani ya Serikali kuwa wao ndio wazabuni wa Serikali. Nashukuru Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, juzi alipokuwa kwenye ziara aligundua kwamba baadhi ya watendaji wa Halmashauri ndio *contractors* katika Halmashauri yake. Sisi huko tulikozunguka tumelikuta huko.

Mimi niliongoza ujumbe kwenda Mkoa wa Mtwara na tulikuta karibu robo tatu ya Ma-*engineer* wa Halmashauri ndio *contractors* wa hizo Halmashauri. Sasa unakuja

kukuta gharama zinapanda na Serikali inalipia gharama kubwa kwa sababu hawa watendaji kwa vyovyyote kwa sababu wanataka fedha gharama za huduma zitapandishwa kwa makusudi. *Supplies Officers* wote ni *suppliers* wa Serikali. Ni vyema Serikali ikaliangalia hili ili isiendelee kulipia gharama za huduma ambazo hazilingani na bei halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kukubali tena kuwaingiza kwenye mpango wa malipo hawa wastaaifu. Ni kweli ni wengi walikuwa wameadhirika na nina hakika kwa nia nzuri ya Serikali inaweza pia kwa kuwa wameshaanza kuwaorodhesha bila shaka wanaweza kuamua kuanza kuwalipa kuanzia Julai badala ya Januari mwakani. Lakini hawa ni wachache wako wale ambao kwa makusudi kabisa hawakuwa tayari kustaaifu ila kwa sababu ya mfumo mpya wa uchumi wakalazimika kustaaifu kutoka kwenye Mashirika ya Umma na hili ni kundi lingine. Wengi wao walikuwa hawajafikia hiyo miaka 55 ya lazima kustaaifu. Lakini wale waliokuwa wa Mashirika ya Umma kwa bahati mbaya hata wale waliokuwa wameanza kupata pensheni sasa wamefutiwa hiyo pensheni. Tunaiomba Serikali ifikirie upya uamuzi huu ili na wao waliokuwa kwenye pensheni kuitia *PPF* waendelee kupata pensheni zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika uchumi wetu. Kwa kweli tunapozungumzia kuondoa umaskini katika nchi hii tunazungumzia kilimo. Kwa sababu kilimo kinatoa pato kwa zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wetu. Gazeti la *East African* la leo tarehe 14 Juni, 2004 limeandika na naomba ninukuu: “*The agriculture is the backbone of economy, song has been sung for ages, but go to the countryside what do you see? Peasant farmers scratching the land with primitive tools.*” Hii ndiyo hali halisi hatujawekeza kiasi cha kutosha katika kilimo chetu. Kilimo chetu ni cha wakulima wadogo wadogo hawa wakulima wadogo wadogo bado hatujawawezesha jinsi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii mwaka jana tulipitisha shilingi bilioni 31.5 mwaka huu Bajeti ni ya bilioni 29 imepungua kwa bilioni 2.5. Sasa sijui tunapiga hatua au tunarudi nyuma. Inabidi tukazanie kilimo zaidi kuliko kitu kingine chochote. Lakini kwa kuwa haiwezekani huyo mkulima wa kawaida kijijini kukopeshana na haya Mabenki nafikiri ni wakati muafaka sasa Serikali kwa makusudi kabisa ikaanza kuzi-support zile *SACCOS* ambazo zinaweza kumkopasha mkulima kule kijijini.

Mkulima wa kawaida hawezи kwenda *EXIM Bank*, mkulima wa kawaida hawezи kwenda *CRDB*. Lakini kuitia *SACCOS* zake kule Vijijini kama Serikali kwa makusudi kabisa inaweza kuziunga mkono ikapeleka fedha huko mwananchi mkulima wa kawaida anaweza kwenda akakopa. Ni vyema basi fedha ambazo tunazitenga kwa ajili ya kukopeshi wakulima badala ya kuziweka kwenye Mabenki makubwa, tuimarishe *SACCOS* tulizonazo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya kilimo mwaka jana tulipitisha kwamba kila mkoaa uchague zao moja la biashara na zao moja la chakula kwa ajili ya kuwa supported na Serikali. Ulikuwa ni uamuzi mzuri. Ebu tufanye tathmini huu uamuzi umeleta impact gani kwenye kilimo chetu. Kwa sababu utajikuta tumetawanya fedha huku na huku

badala ya kuziweka sehemu moja zikaleta *impact* kubwa tukawakopesha wakulima wakubwa wanaojitokeza wakaweza kuendeleza mabonde. Ni fedha ambazo tumetawanya nchi nzima na *impact* yake ni ndogo sana. *I challenge* Waziri kabisa afanye tathmini aone, hakuna *impact* ambayo tunaweza kujivunia.

Mimi nashauri kwamba hizi fedha pamoja na nia nzuri tuweze kuziweka kwenye Mfuko Maalum tutafute miradi ambayo itakuwa ni ukombozi kwetu ya kilimo ili huko ndiko zielekezwe badala ya kuzisambaza nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu tunalima kahawa na tumeambiwa kwamba kuna fedha za *STABEX* tunaomba kufahamu hizi fedha hasa ziko wapi? Ziko Wizara ya Kilimo na Chakula, Ujenzi au ziko Hazina ili tujue utaratibu wa kuanza kuchukua. Maana yake ahadi ya kwamba barabara zitakazoelekea kwa wakulima wa kahawa zitatengenezwa katika jimbo langu la Buyungu bado barabara hizo hazijatengenezwa na ningependa kujua hizo fedha ziko wapi ili wananchi waweze kuanza kuzichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. AMANI W. A. KABOIROU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niwapongeze watoa mada hii ya Bajeti na Mipango ya Maendeleo, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kazi nzuri ambayo naamini wengi wa Watanzania wameifurahia. Lakini vile vile, nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba uliowapata na tuombe tu kwamba wawe na subira katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kusema. Kama nilivyosema, Bajeti hii sasa inaonekana kidogo inawajali Watanzania hasa kwa kuzingatia kuwa kwa kweli uchumi wa nchi ni pale tu unapo-*balance production* na *consumption* na uki-*balance* vitu hivyo utajikuta unaendelea *whether unapenda au hupendi na huwezi ku-balance production* na *consumption* kama hutumii nguvukazi na ukweli unabakia pale pale kwamba kwa nchi kama Tanzania na nchi zingine za *third world* ajira kubwa iko katika kilimo. Sasa ni vizuri kuangalia watu wanajihuisha huko ili waweze *ku-produce* na kwa maana hiyo kuruhusu ulaji wao uwe wa kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kabla ya lolote nimnukuu Mheshimiwa Basil Mramba, kwenye hotuba yake kifungu cha 53 *page* 64 na 65, anasema: "Mheshimiwa Spika, katika yote haya mafanikio halisi ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini yatapatikana pindi tutakapoweza kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati."

"Pili, tunahitaji kujenga uwezo wa utaalam ambao ni lazima katika dunia hii ya utandawazi. Tatu, kwa kuwa Wananchi wengi wanaishi vijiji na wanategemea kilimo kwa chakula na ajira ni lazima mkakati wetu wa kuinua kilimo uwe imara zaidi na uunganishe kilimo, viwanda na biashara ndipo tutaweza kugeuza Sekta hiyo iwe ya kisasa. Pengine tuna haja ya kuangalia tena vipaumbele vyetu ili tupate tija ya uhakika kwa kutumia uwezo mdogo tulionao wa fedha kwa maeneo machache kwanza kuliko

kugawa kidogo kidogo bila mafanikio ya maana. Nitafurahi kupata ushauri wa Waheshimiwa Wabunge juu ya wazo hili wakati wa mjadala wa hoja hii.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nashukuru kwamba ameomba ushauri huu. Nasema kwamba *may be* wakati wa mjadala ya Bajeti siyo muafaka sana, labda wigo huu ungepanuliwa ili watu wakawa wanakutana hata kabla na kuweza kopenyeza mawazo huko kwa hao wanaotengeneza Bajeti. Lakini mimi nasema, *hypothetically* kama Mheshimiwa Basil Mramba angepewa trilioni 15 kwenye Bajeti hii, nadhani tusingekuwa hapa tunabishana kuhusu lolote kwa kweli. Lakini tunabishana kwa sababu kuna trilioni 3.3 na Serikali yenyewe inakiri kwamba hiyo ni asilimia 13.3 ya Pato la Taifa. Sasa, sijui mchawi ni nani hapa! Sote tunajua kabisa hiyo ni asilimia 13.3 ya Pato la Taifa na kwa maana hiyo ni kwamba, sasa Serikali imeshindwa kukusanya pesa kwa sababu kuna asilimia 83 zinalea huko. Mimi nastaajabu! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa basi utaratibu wa kukusanya hayo mapato ambayo yapo, mengine ndiyo kama hayo tumeambiwa anakuja mtu anawekeza kwenye mgodi anaondoka na shilingi 97 katika kila 100 anayozalisha na sisi tunachekelea na hawa waliosaini mikataba hiyo hawajakamatwa tukawafikisha kwenye Tume kama ambavyo wenzetu Kenya wanafanya sasa. Waje tuwaulize, bwana ilikuwaje, mlikutana wapi, ilikuwa baa au hotelini, hivi ilikuwaje wewe ukubali jambo hili wakati unajua Botswana wanapata asilimia 40, wangetuambia. Lakini wanatembea na sisi tunapigizana kelele hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia asilimia 40 ingekuwa ni pesa nyingi sana kwa sababu tumeona Pato letu la Taifa limeongezeka kutola Dola milioni 619 mpaka milioni 917 kwa ukuaji wa madini na siyo zaidi ya asilimia 26. Je, tungepata asilimia 40 ya pesa hizo ingekuwa? Naamini tungekuwa kwenye trilioni 5 ya shilingi za Tanzania na kwa hiyo tungekuwa na uwezo wa kuwahudumia hao wakulima wetu tunaowaonea imani sana na kufanya mengine mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *paragraph* hii inatuambia kabisa tuunganishe miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati. Ninashukuru Mheshimiwa Basil Mramba ameliona hilo kwamba nishati ni miundombinu au ni sehemu ya muundombinu amba ni muhimu sana. Kwa bahati mbaya sana hata katika Bunge letu hatujaiweka nishati chini ya Kamati ya Miundombinu tunadhani labda ni kitu tu kiko hewani, lakini kwa kweli ni mhimili mkubwa sana katika miundombinu. Tungekuwa na pesa hizo tunazopoteza tungeweza kufanya mengi, lakini kwa sababu hatuna sasa tunakutana kila mwaka kubishana, kuulizana, kutiana vidole machoni kwa sababu tu tumeshindwa kukusanya pesa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hapa katika Bajeti ukurasa wa 71 unasema: “Ushuru wa bidhaa ya petroli asilimia 8 mwaka 2003/2004, 2004/2005 ushuru wa bidhaa ya petroli asilimia 8.” Ni muujiza!

Kwanza ni lazima kutakuwa na mitambo mingi mipya na hata Bajeti inaruhusu mitambo hiyo sasa iingizwe bila kodi na kadhalika. Uzalishaji utaongezeka, kwa hiyo, mafuta mengi yatatumika na kuwakomesha wezi wa mafuta tunaweka *flow meters* pale

bandarini, nadhani ni bilioni kama 7 hivi. Tumeambiwa kwamba mitambo hiyo itakuwa imekamilika mwezi wa 7 au labda mwezi wa 9.

Sasa unajiuliza, ni kwa nini tunatumia bilioni zetu 7 au labda hata chache kutengeneza *flow meters* na kuagiza na nini, wakati huko tayari kuna matatizo? Lakini tuseme kwamba, ndio hivyo itakuwa mwezi Julai, *flow meters* zitaaanza kufanya kazi. Sasa tunaziwekea nini kama mapato yetu yatakuwa *stagnant?* Kwa nini una-*invest* kwenye kitu hewa? Ningedhani unataka u-*invest* pesa zako mahali ambapo zitarudisha, kunakuwa na *multiplier effect* ndio *economics*. Lakini sasa Serikali inachukua pesa zetu ambazo zingejenga barabara yangu ya kutoka Kigoma hadi Tabora kwa kiwango cha lami wanaziweka pale bandarini Dar es Salaam halafu hawapati kitu! Hiyo ni raha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kusema hapa na sisemi kama utani. Mheshimiwa Mjumbe mmoja amesimama na kusema kwamba labda Mashirika binafsi yapewe uwezo wa kuwafuatilia walipakodi ili wasiwe *harassed* na *TRA*. Lakini mimi nimesema tubinafsish *TRA*. Huwezi wewe ukawa na daladala ambayo kila mtu anajua inamletea shilingi 10,000/= kwa siku wewe unapata shilingi 3,000/= na unaona raha tu! Si utampa dreva mwengine bwana na kondakta mwengine wakusanye hizo pesa. Kama huyu hawezi kukusanya shilingi 10,000/= na ni daladala yako wengine wanapata shilingi 10,000/= kwa siku wewe unafurahi nini sasa? Ndiyo *TRA* hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema labda tuanzie hata kwenye Kitengo cha Ushuru pale forodhani au bandarini, kuna ubaya gani? Hivi leo Serikali yenewe sasa inahusisha Makampuni binafsi katika ulinzi hata wa Wizara, siyo lazima Polisi tena, si inaruhusiwa kabisa! Kuna watu wanapewa tenda za kusafisha ofisi za Serikali, watu binafsi. Sasa kwa nini hii ya ukusanyaji pesa liwe tatizo hapa na sisi tukae tukikubali tu kwamba, aah, bwana tutaongeza wataalam. Tunajuaje kama hakuna wataalam? Kama tumeweza kuleta wachimba dhahabu kutoka Australia na Canada basi tufanye na kwenye ukusanyaji wa pesa kwa sababu ni utaalam unaotafutwa hapa. Lakini hatuwezi kwa kweli kukaa hapa na kila siku kujadili kitu kwa sababu tu hatuna pesa mfukoni

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, mipango yetu mingi haitekelezwi na tumeambiwa kuna *reserve* kubwa sana huko Benki ya Tanzania shilingi trilioni 1.7 na kidogo zimekaa. Tunafahamishwa kwamba, sasa Tanzania bwana ina uwezo wa kujinunulia bidhaa zake zote kwa miezi sita bila matatizo. Sijui hiyo *formula* aliitoa nani, ni ya Gavana Balali au ndio *International Economics*, kwamba wewe unakaa hapa watoto wako wanalala na njaa, umeficha pesa unasema: “Hizi bwana, mwaka kesho nitanunua gari jipya.”

Hivi ni nchi gani hiyo imeshakaa miezi sita haijapata kipato ila wanatumia tu akiba yao! *You wonder*, ni nchi gani hii? Nani amesema hizo pesa zifungiwe kwa miezi sita wakati wananchi wanateseka? Watuambie bwana, sisi wengine hatukusomea *economics*, labda Waheshimiwa wa *economics* mtatuambia sisi wengine tunaona tu ajabu kwamba hatujaona vitu vya namna hii! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninastaajabu, tunajifunga mikono tunashindwa kutumia raslimali zetu eti tunapeana nguvu tunasema: "Miezi sita tutakuwa hatuna tatizo hapa." *In six months we may be dead!* Zitumike pesa hizo, ndiyo maana ya kuchuma, ndiyo maana ya kuweka akiba, maana yake ni kwamba itumike pale ambapo mna shida. Si hapa Mheshimiwa Basil Mramba anasema miundombinu ya reli, ya nini ya nini, nenda basi pale *Tanzania Railway Corporation* uone mashine mbovu, halafu mtu anakwenda kule anawaambia watu: "Ooh jamani, tumepta wafadhili watakarabati mabehewa yetu 54." Kwa nini mfadhili aje kukarabati mabehewa ambayo kila siku wewe unapata pesa na ziko benki? Unangoja ukununue nini? Au ndiyo hivyo vipodozi alivyosema Mzee Edson Halinga? Binafsi sielewi ni kitu gani kinakwenda kununuliwa na hizo pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi nikasema mengi kwa sababu nimeshakubali kwamba angalau sasa hivi tunaona Serikali ya wenzetu imeanza kuwa na imani na watu wadogo wadogo, kuwapa pesa kidogo, kuondoa makodi ya ajabu ajabu, leseni zisizokuwa na kichwa wala miguu, vyote hivi kwangu vinanifurahisha. Lakini ningependa niseme moja tu kwamba, kama nishati ni muundombinu muhimu na kama sisi Tanzania tunatumia bilioni 3 na kidogo na ikija hiyo Songas itakuwa bilioni 5.5 *ku-subsidize TANESCO, it is high time.* *TANESCO* nao wa-*subsidize* kule ambako dhahiri hakuna umeme kama Mkao wa Kigoma, walete majenereta ya kutosha kwa sababu sisi tunatumia pesa na hii ni pesa ya walipakodi wa nchi nzima, haiwezekani. Sisi tunasema: "Ooh bwana, unajua kikiharibika kitu Dar es Salaam watu wanapata shida sana." Ila wale watu wa Kigoma sijui ndiyo nani!

MBUNGE FULANI: Wanyamulenge. (*Kicheko*)

MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU: Nimeambiwa Wanyamulenge, lakini mimi naona kama hili ni jambo la ajabu sana. Kuna watu karibu milioni 2 pale Mkoani, kweli tuko katika mwaka 2004 tunakwenda 2005 mnatuambia sisi tungoje tu! (*Kicheko*)

Leo nilikuwa nampigia simu Mwenyekiti wangu wa Halmashauri nimemkosa mara tatu, kanipigia nikiwa hapa nimetoka nje nikamuuliza: "Mbona nimekupigia bwanu, lakini sikupati?" Akasema: "Bwanu, umeme hakuna huku." Sisi tunaishi hivyo, *TANESCO* tunawa-*subsidize* Dar es Salaam na kwingineko, tunataka kama ukweli ndiyo huo kwamba nishati nayo ni muundombinu muhimu katika kuwalettea wananchi ufanisi na huwezi kuwasaidia hawa wakulima na wavuvi wadogo wadogo kama hawana nishati, kama hawana umeme wa uhakika kule Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono *speech* hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, muda wa shughuli za Bunge umekwisha. Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho Saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.43 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 15 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi*)

